ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID - SPIKA

1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/	-	Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri Ofisi ya Rais Mwenyekiti wa Nchi, na wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri Ofisi ya Rais Mikoa na Tawala za Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala

Bora /Jimbo la Makunduchi

8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed - MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais

9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed - MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge

10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo - MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki

11. Mhe. Riziki Pembe Juma - MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake

12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali - MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais

13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume - MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais

14. Mhe. Rashid Ali Juma - MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani

15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed - MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais

16. Mhe. Maudline Cyrus Castico - MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais

17. Mhe. Salama Aboud Talib - MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake

18. Mhe. Juma Ali Khatib - MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais

19. Mhe. Said Soud Said - MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais

20. Mhe. Khamis Juma Mwalim - Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe

21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga - Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais wa Zanzibar/ Jimbo la Mwera

22. Mhe. Shamata Shaame Khamis - Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ / Jimbo la Micheweni

23. Mhe. Harusi Said Suleiman - Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete

24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri - Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani

25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum - Naibu Waziri wa Ujenzi,

Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi

26. Mhe. Chum Kombo Khamis - Naibu Waziri wa Habari,
Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake

27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman - Naibu Waziri wa
Uwezeshaji,Wazee,
Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake

28. Mhe. Lulu Msham Abdalla - Naibu Waziri wa Kilimo,
Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake

29. Mhe. Juma Makungu Juma - Naibu Waziri wa Ardhi,
Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini

30. Mhe. Abdalla Ali Kombo - Jimbo la Mwanakwerekwe

31. Mhe. Abdalla Maulid Diwani - Jimbo la Jang'ombe

32. Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil - Uteuzi wa Rais

33. Mhe. Ali Khamis Bakar - Jimbo la Tumbe

34. Mhe. Ali Salum Haji - Jimbo la Kwahani

35. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) - Jimbo la Kijitoupele

36. Mhe. Ame Haji Ali - Jimbo la Nungwi

37. Mhe. Amina Iddi Mabrouk - Nafasi za Wanawake

38. Mhe. Asha Abdalla Mussa - Jimbo la Kiwengwa
39. Mhe. Bahati Khamis Kombo - Jimbo la Chambani
40. Mhe. Bihindi Hamad Khamis - Nafasi za Wanawake
41. Mhe. Hamad Abdalla Rashid - Jimbo la Wawi
42. Mhe. Hamida Abdalla Issa - Nafasi za Wanawake
43. Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Shaurimoyo
44. Mhe. Hassan Khamis Hafidh - Jimbo la Welezo
45. Mhe. Hidaya Ali Makame - Nafasi za Wanawake
46. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa) - Jimbo la Mtoni
47. Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Paje
48. Mhe. Khadija Omar Kibano - Jimbo la Mtambwe
49. Mhe. Machano Othman Said - Jimbo la Mfenesini
50. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti - Jimbo la Mtopepo
51. Mhe. Makame Said Juma - Jimbo la Kojani
52. Mhe. Maryam Thani Juma - Jimbo la Gando
53. Mhe. Masoud Abrahman Masoud - Jimbo la Bububu
54. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Jimbo la Chumbuni
55. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Jimbo la Mtambile

56. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Jimbo la Mpendae
57. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
58. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
59. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
60. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
61. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
62. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
63. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
64. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
65. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
66. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
67. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
68. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake
69. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Jimbo la Magomeni
70. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Nafasi za Wanawake
71. Mhe. Said Omar Said - Jimbo la Wingwi
72. Mhe. Said Hassan Said - Mwanasheria Mkuu
73. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma - Nafasi za Wanawake

74. Mhe. Salma Mussa Bilal - Nafasi za Wanawake
75. Mhe. Shaib Said Ali - Jimbo la Chonga
76. Mhe. Simai Mohammed Said - Jimbo la Tunguu
77. Mhe. Sira Ubwa Mamboya - Uteuzi wa Rais
78. Mhe. Suleiman Makame Ali - Jimbo la Ziwani
79. Mhe. Suleiman Sarahan Said - Jimbo la Chakechake
80. Mhe. Tatu Mohamed Ussi - Nafasi za Wanawake
81. Mhe. Ussi Yahya Haji - Jimbo la Mkwajuni
82. Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Nafasi za Wanawake
83. Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Nafasi za Wanawake
84. Mhe. Yussuf Hassan Iddi - Jimbo la Fuoni
85. Mhe. Zaina Abdalla Salum - Nafasi za Wanawake
86. Mhe. Zulfa Mmaka Omar - Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem - Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Nane - Tarehe 16 Februari, 2018

(Kikao kilianza saa 3:00 Asubuhi)

DUA

Mhe. Naibu Spika, (Mgeni Hassan Juma) alisoma Dua

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Naibu Spika**,** Waheshimiwa Wajumbe Katika Kikao cha Baraza la Wawakilishi cha tarehe 12 Februari, 2018, Mhe. Hidaya Ali Makame aliuliza swali la nyongeza kwa Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi na kuahidiwa kujibiwa kwa maandishi. Sasa namuomba Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi asome jibu la swali la nyongeza lililoulizwa na Mheshimiwa mjumbe huyo.

Mhe. Naibu Waziri ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe.Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Hidaya Ali Makame swali lake alilouliza la maandishi kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, Wakati ninajibu swali Namba 57, niliulizwa swali la nyongeza na Mhe. Hidaya Ali Makame aliyetaka kujua kuna *"power tillers'* 50 ambazo zimetolewa kwa Jumuiya za Wakulima. Sasa angependa kufahamu hizi jumuiya za wakulima ambazo zimepewa *"power tillers"* hizo. Jibu la suala hilo ni kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika**,** Jumla ya *"power tillers"* zilizogaiwa kwa Jumuiya za wakulima ni 50 (Unguja 43 na Pemba 7) kwa jumuiya 17 ambapo (10 Unguja na 7 Pemba).

Mhe. Naibu Spika, ningeomba kuzitaja Jumuiya hizo. Aidha, mgao ulikuwa kama ifuatavyo:-

S/ NO	**JINA LA JUMUIYA**	**IDADI**	**SEHEMU**
1.	Jumuiya ya Umwagiliajimaji Kibokwa.	7	Unguja
2.	Jumuiya ya Umwagiliajimaji Kianga.	1	Unguja
3.	Jumuiya ya Umwagiliajimaji Uzini	2	Unguja
4.	Jumuiya ya Umwagiliajimaji Koani.	1	Unguja
5.	Jumuiya ya Umwagiliajimaji Cheju.	8	Unguja
6.	Jumuiya ya Umwagiliajimaji Mwera.	5	Unguja
7.	Jumuiya ya Umwagiliajimaji Ubago.	1	Unguja
8.	Jumuiya ya Umwagiliajimaji Bumbwisudi.	9	Unguja
9.	Jumuiya ya Umwagiliajimaji Mtwango.	7	Unguja
10.	Jumuiya ya Umwagiliajimaji Kizimbani.	2	Unguja
11.	Jumuiya ya Umwagiliajimaji Mangwena.	1	Pemba
12.	Jumuiya ya Umwagiliajimaji Weni.	1	Pemba

13.	Jumuiya ya Umwagiliajimaji Tungamaa.	1	Pemba
14.	Jumuiya ya Umwagiliajimaji Kinyakuzi.	1	Pemba
15.	Jumuiya ya Umwagiliajimaji Saninga	1	Pemba
16.	Jumuiya ya Umwagiliajimaji Tibirinzi	1	Pemba
17.	Jumuiya ya Umwagiliajimaji Makombeni.	1	Pemba

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

HOJA ZA KAMATI

Mhe. Yussuf Hassan Iddi (Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo): Mhe. Naibu Spika, naomba kuweka Hati Mezani Muhtasari wa Ripoti ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa mwaka 2017/2018. Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 45

Kupandishwa Vyeo Watumishi wa Idara Maalum za SMZ

Mhe. Omar Seif Abeid -Aliuliza:

Kwakuwa programu ya usimamizi na utumishi wa Idara Maalum za SMZ moja kati ya majukumu yake ni kutoa miongozo ya ajira, kupandisha vyeo na kuongeza muda wa utumishi, na kwasababu wapo vijana ambao wameshakwenda kwenye kozi mbalimbali

kutoka 2014 na bado hadi leo hawajapandishwa vyeo kwa mujibu wa kozi walizosomea.

a) Je, ni lini askari na maafisa ambao wameshamaliza kozi watapandishwa vyeo vyao.

b) Je, ni watumishi wangapi waliomaliza muda wao wa kazi waliongezwa muda na fani zao ni zipi.

c) Je, mtu ambae alistaafu na akapewa mkataba wa muda wa miaka miwili anastahiki kuongezwa muda kama huo mara ngapi kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Omar Seif Abeid swali lake Nam. 45 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Naibu Spika, kupandishwa cheo ni hatua muhimu katika kumuendeleza mtumishi pamoja na kumpa motisha katika utendaji wake. Askari au maafisa hupandishwa vyeo katika kutimiza matakwa ya kimuundo ya kikosi husika.

Mhe. Naibu Spika, ziko sababu mbalimbali zinazopelekea askari kupadishwa cheo katika Idara Maalum za SMZ miongoni mwa sababu hizo ni pamoja na mahitaji ya kimuundo wa kikosi husika, bajeti ya kikosi, utangulizi *(seniority),* mahitaji maalum ya kikosi, kuhudhuria na kufaulu kozi na muda wa kukaa na cheo.

Mhe. Naibu Spika, suala la kuhudhuria kozi ni utartibu wa kila siku kwa maskari na maafisa wa Idara Maalum.

Kumaliza mafunzo sio kigezo pekee kinachotumika katika kupandisha cheo kwa askari, pia kuna mazingira mbali mbali ya kuzingatia kabla ya askari kupandishwa cheo kama yalivyoelezwa hapo juu.

Mhe. Naibu Spika, hivyo, maaskari na maafisa wa Idara Maalum watapandishwa vyeo endapo mazingiria ya kufanya hivyo yataruhusu pamoja na kutimiza vigezo vyengine.

b) Mhe. Naibu Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 22(1) cha Sheria ya Utumishi wa Umma Namba 2 ya mwaka 2011 Afisa wa Idara Maalum za SMZ anaweza kuongezewa muda wa utumishi usiozidi miaka miwili endapo itaonekana kuna haja ya kufanya hivyo kwa lengo la kutoa ujuzi zaidi. Mhe. Naibu Spika, kabla ya kuongezwa utumishi taasisi husika ni lazima ithibitishe kwa tume kuwa kuondoka kwake kwa afisa huyo kutaleta athari katika utekelezaji wa majukumu ya idara husika.

Mhe. Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Mjumbe aridhike kwamba wapo maafisa wa Idara Maalum za SMZ waliongezwa muda, lakini aridhike nisimtajie idadi hapa ndani ya Baraza lako Tukufu. *(Makofi)*

c) Mhe. Naibu Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 60 cha Sheria ya Utumishi wa Umma, afisa aliyestaafu kazi anaweza kuajiriwa kwa mkataba na muda tofauti. Aidha, kifungu cha 26(1) cha Kanuni za Tume ya Utumishi za Idara Maalum za mwaka 2007 zinaelezea utaratibu unaotumika kwa afisa aliyeajiriwa kwa mkataba katika Idara Maalum, maafisa hawa huajiriwa baada ya kustaafu kwa lengo la kutoa utaalamu ambao umekosekana katika idara husika.

Mhe. Naibu Spika, Sheria ya Utumishi na Kanuni zake hazijaweka ukomo wa mara ngapi mtumishi anaweza kuajiriwa kwa mkataba, suala la msingi ni uwezo wake wa kutoa ujuzi kwa wengine. Mhe. Naibu Spika, nakushukuru.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza lenye kifungu (a) na (b)

Kwakuwa muongozo wa Utumishi wa Idara Maalum ya SMZ unasema kuwa askari mwenye elimu ya *degree* au ya *diploma* anastahiki kuwa cheo fulani kimeanishwa na kwasababu wapo askari katika Vikosi vya JKU, KMKM na KVZ ambao mpaka leo hawajapandishwa vyeo na wenzao Kikosi kama cha Zimamoto na Uokozi pamoja na Kikosi cha Chuo Cha Mafunzo wao wamepandishwa vyeo sasa mimi nilitaka kujuwa kwasababu wizara ni moja.

a) Ni kwasababu gani zilizowafanya hawa wakaongezwa vyeo, wakapandishwa wale wengine wasipandishwe.

b) Pili naomba kufahamu kuwa je kufanya hivyo, wizara inapofanya hivyo haioni kwamba inawavunja moyo wale wangine ambao walikwenda kwa pamoja vikosi vyengine vikapandishwa vile vyengine wasipandishwe vyeo.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Omar Seif Abeid swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Naibu Spika, nadhani katika jibu langu la msingi nimeeleza bayana kwamba suala la elimu si kigezo pekee ambacho kinaweza pia kikamfanya pia kwamba askari wetu

kuweza kupandishwa cheo. Mhe. Naibu Spika, nimesema kwamba suala la kupandishwa cheo kunazingatiwa mambo mengi yaani vigezo vingi, kwahiyo inawezekana kwamba askari taaluma yake ni kubwa lakini kuna mambo mengine yamekosekana hakutowi sababu au hakutomfanya kuweza kupandishwa cheo kama vile ambavyo angehitaji yeye kuweza kupandishwa cheo.

b) Sababu ya kuwavunja moyo ama kutokuvunjika moyo hiyo inawezekana ni hulka, lakini kwa mujibu wa utaratibu wa kijeshi wao wanafahamu ni namna gani vyeo vinaweza kupatikana kwa hiyo kama mtumishi ambae anauzalendo na inaijuwa kazi yake siamini kwamba anaweza kuvunjika moyo kama endapo hajapandishwa cheo ahsante.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, na mimi nakushukuru kunipa nafasi hii kwa kumuuliza swahibu wangu Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ swali dogo la nyongeza kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ alivyokuwa akijibu swali la msingi la Mhe. Omar Seif Abeid alieleza kwamba ni kweli wapo askari ambao idadi yake amesema hawezi kuitaja hapa Barazani ambao wameajiriwa kwa mkataba sasa swali langu liko hapa

a) Je, hatuoni kwamba wizara inashindwa kuwapatia taaluma askari wake, ili kuweza kukidhi mahitaji ili pale wale ambao wanostahafu kuweza kukava pengo lao.

b) Je, kama hiyo ni sahihi je hatuoni umuhimu sasa wa kuandaa mafunzo maalum kwa askari wale ambao wanatarajia kustaafu zile nafasi zao zikashikwa na watu wengine.

Kwakweli, Mhe. Naibu Spika, sasa hivi tunavija wengi ambao wamesoma tena wana elimu ya juu wako mitaani na vyeti vyao hawana ajira, kuendelea kungangani askari wameshastaafu wakati tunashindwa kusomesha na kuajiri wengine. Je, hatuoni hii tunawavunja moyo wale wasomi wetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Hamza Hassan Juma swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, ukweli ni kwamba ushauri wa Mhe. Mwakilishi ambao ameutowa ni muhimu sana, ni dhahiri kwamba kupitia Vikosi vyetu vya Idara Maalum za SMZ tayari mikakati imeshachukuliwa na hilo tayari tumeshalibaini, kwa sasa tunatarajia kwamba huko tunakokwenda haitofikia katika hali kama hiyo ambayo imeweza kujitokeza huko nyuma. Kwahiyo ukweli ni kwamba juhudi zinaendelea kufanyika na suala la mafunzo ni jambo muhimu na sio kwa vikosi vyetu tu hata kwenye taasisi nyengine. Hivyo, niseme kwamba ushauri huu tunaendelea kuuchukuwa vilevile Mhe. Mwakilishi afahamu kwamba juhudi hizo tayari tumeshaanza kuzifanyia kazi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii kutoa majibu ya nyongeza kwa Mhe. Hamza Hassan Juma swali lake lenye (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, kwanza nataka nichukuwe nafasi hii kumshukuru au kumpongeza Mhe. Naibu Waziri, kwa kujibu majibu mazuri sana ambayo yamejibiwa kwa mujibu wa utaratibu wa uwendeshaji wa taasisi zenye taathira ya kijeshi kwa hiyo

hongera sana Naibu Waziri kwa majibu ambayo umejibu kwa niaba yangu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, lakini nataka niseme Afisi yetu ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Idara Maalu za SMZ haijashindwa kabisa kuwapa mafunzo vijana ambao wanahitajika kuendelezwa katika Idara zetu Maalum. Lakini Afisi yetu pia ina mpango madhubuti wa kuandaa mafunzo, ili kuwaendeleza vijana hawa na kila baada ya muda nadhani Mhe. Mwakilishi nishahidi anashuhudia kwamba viongozi mbalimbali wa serikali wanakwenda kufunga mafunzo ya uaskari.

Mhe. Naibu Spika, kupandishwa cheo kwa askari hakuhusiana na suala la kuwangezea wapiganaji ambao wana ujuzi maalum katika Idara Maalum za SMZ. Kwahiyo, uaskari sio usomi peke yake lakini uaskari ni *training*, kwa maana ya mafunzo mtu anapoitwa *captain* katika uaskari maana huyo ni *captain* mpaka afe kinachothaminiwa pale ni ule u-*captain* na u-captain huwezi kuwa *captain* huwezi kuwa kanali huwezi kuwa meja huwezi kuwa komodoo kama hujawa na *training* huwezi kuwa CDR kama hujawa na *training*. Kwa maana hiyo, kinafanya serikali iendelee kuwaajiri wale askari wa Idara Maalum kwa mkataba kwa maana ya kutowa *suspicion plan*, *suspicion* kwa watumishi wengine au wapiganaji wengine ambao wamo ndani ya Idara Maalum. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwa hiyo nataka nilihakikishie Baraza lako Tukufu kwamba kwanza afisi yetu haijashindwa kuandaa *training*, tunaendelea kuandaa *training* na askari hivi sasa kuna *training* ambazo wanazipata na kwenda mafunzo sio kigezo pekee cha kuweza kupandishwa cheo. Kupandishwa cheo kama alivyosema Naibu Waziri kunatokana na muundo na ukubwa wa kikosi na mahitaji ya kuwepo hicho cheo chenyewe na uwezo wa kuweza kukitumikia hicho cheo chenyewe, unaweza ukaenda *training*

lakini kama haja ya kupandishwa cheo haipo huwezi kupandishwa cheo. Mhe. Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Hamad Abdalla Rashid: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa nafasi hii ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri na mimi ningekuwa na swali dogo la nyongeza la kumuuliza lenye kifungu (a) na (b)

a) Mhe. Naibu Waziri, katueleza wazi hapa kwamba kupandishwa cheo kwa askari hawa kigezo cha kwanza ni mafunzo, lakini cha pili kuna vigezo vyengine ambavyo bado sijavisikia vizuri. Mimi naomba nijue ni vigezo gani hivi vyengine.

b) Katika askari wanaoajiri wa kwa mkataba wa miaka miwili hawa je wanastahiki kupandishwa cheo ndani ya miaka miwili. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, (OR), Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, nilipokuwa nikitoa majibu Mhe. Mwakilishi aliweza kusikia lakini kwa ufupi alisema kwamba yeye anataka kujua zaidi kwa undani. Naomba nitoe mfano mdogo tu sana kwa sababu sikutaka kueleza kama nilivyosema kwa undani zaidi. Mhe. Naibu, kiufupi kwa mfano miongoni mwa vigezo anaweza awe amefikisha kiasi asipungue miaka minne kwa utumishi wake, vilevile katika masuala mengine kama alivyotangulia kusema Mhe. Waziri kuna kozi lazima azipate. Kwa mfano, kama KVZ aende kozi ya uongozi mdogo na pia nafasi nyengine ikiwepo

katika sehemu ambayo anaifanyia kazi kama kuna haja kwamba kuna mtu anahitajika kupandishwa cheo, basi nadhani inaweza ikawa ni sehemu ikatoa fursa hiyo.

Mhe. Naibu Spika, jengine kubwa zaidi katika utumishi suala kubwa ambalo tunaweza kuangalia kama Mhe. Waziri alivyotoa ufafanuzi ni suala la nidhamu inaweza ikafanya kwamba iwe ni sababu pia. Kwahiyo, inawezekana kwamba amesoma vizuri, ametumikia muda wa kutosha lakini hatimae kwamba kama nidhamu na cheo kama alivyosema Mhe. Waziri kuwa haiendani na hicho cheo hawezi kupata cheo katika vikosi vyetu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, naomba tujue tu kwamba maaskari wetu wote kiufupi kwa ujumla wanahitaji kupandishwa vyeo. Lakini ukweli ni kwamba lazima waweko wenye vyeo na waliokuwa hawana vyeo ndio kutakuwa kuna uongozi. Kwahiyo, jambo la msingi Waheshimiwa Wajumbe naomba turidhike kwamba watendaji wetu wote wanahitaji vyeo, lakini hatuna vyeo na hivyo vyeo ni kwamba ni kundi dogo la watu wachache ambao wanahitaji kuendelea kuongoza wenzao. Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana ahsante.

Nam. 39

Watoto Wanaoishi Katika Mazingira Magumu

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza:

Kwenye hotuba ya bajeti ya mwaka 2016/2017 Mhe. Waziri wa wizara hiyo alieleza kwamba serikali imeanzisha mpango wa utambuzi wa watoto wanaoishi katika mazingira magumu, kwa shehia mbalimbali za Unguja na Pemba jambo ambalo linaweza kuleta mafanikio makubwa ya kupunguza idadi ya watoto wanaozurura ovyo mitaani na kutumikishwa kwa malipo madogo.

(a) Je, baada ya kuwatambua vijana hao serikali imechukua hatua gani za kuzisaidia familia zenye watoto hao, ili kuepukana na kuishi katika mazingira magumu ambayo wanaishi nayo hivi sasa.

(b) Je, ni familia na watoto wangapi ambao wapo kwenye familia zinazoishi katika mazingira magumu kwa shehia zilizofanyiwa uchambuzi kwa Unguja na Pemba.

(c) Je, ni utaratibu upi unaotumika kuzitambua familia hizo hadi kufikia Novemba, 2017 ni familia ngapi zimeshatambuliwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto - Alijibu:

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, awali ya yote kwanza naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema ambaye na yeye anaendelea kutupa pumzi zake na asubuhi hii tukaweza kukutana hapa tukiwa wenye afya na wenye bashasha tele.

Baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu Mhe. Naibu Spika, sasa kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 39 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Baada ya utambuzi wa watoto, serikali inachukua hatua ya kuwaunganisha watoto hao na huduma mbalimbali kama skuli, afya, ushauri nasaha kwa mujibu wa mahitaji ya watoto hao. Kuna miradi imeanzishwa na wadau mbalimbali ndani ya shehia ambayo inawawezesha kaya hizi kiuchumi na kuwapatia mafunzo ya ujasiriamali na mitaji midogo midogo kwa kutumia orodha ya watoto waliotambuliwa na wana shehia kwenye mazingira magumu. Idara pia inasaidia baadhi ya kaya zilizotambuliwa

kwenye shehia kwa kuwapatia kisaidizi cha fedha kila mwezi, ili kusaidia mahitaji madogo madogo.

(b) Mhe. Naibu Spika, kwa kipindi cha mwaka wa 2016/2017 jumla ya watoto 273 (wanawake 133 na wanaume 140) walitambuliwa kama ni muendelezo kutambua watoto katika shehia sita (6) ambazo ni Shehia ya Wazee, Jang'ombe, Mwembemakumbi, Magomeni, Nyerere na Kidongo Chekundu.

(c) Mhe. Naibu Spika, utaratibu unaotumika ni kwa mashirikiano na wana kamati wanaotoka kwenye shehia husika, shehia hizi zinaunda kamati kushughulikia watoto wenye mazingira magumu. Kamati hizo hupewa mafunzo ya siku mbili hadi nne na jinsi ya kuwatambua na kuwasajili watoto wa shehia husika kwa kutumia muongozo ulioandaliwa na mashirikiano na wadau. Ndani ya mafunzo hayo yenye kutumia vigezo vinavyokubalika na wadau kuna zoezi la kutambua watoto hao kwa ushiriki au usimamizi wa idara. Hadi Disemba, 2017 jumla ya watoto 22,143 wameshatambuliwa Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na wingi wa watoto hawa wenye mazingira magumu natoa wito kwa Waheshimiwa Wawakilishi na Wabunge kusaidiana na serikali kuhakikisha wanazitambua kaya hizi zilizopo ndani ya majimbo yao na kuzisaidia. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri ambapo wanafanya kazi hiyo wizara inajitahidi kufanya kazi hiyo, lakini kutokana na wingi wa shehia hizi na wameeleza kwamba ni kwa upande wa Unguja. Sasa nilitaka nijue kwa kule Pemba wana mpango gani kwanza wa kuzitambua hizi familia zenye watoto masikini. Vilevile, nataka kujua utaratibu gani wa jumla kwa

Unguja na Pemba utakaotumika, ili kuwajumuisha hao watoto wote kuzitambua zile familia na kuweza kujua takwimu sahihi. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza. Swali lake la mwanzo limegusia kuhusu kuwatambua watoto waliokuwepo Kisiwani Pemba. Mhe. Naibu Spika, ni kwamba tunapofanya utafiti huwa tunafanya visiwa vyote viwili Unguja na Pemba, kwa maana hiyo hata Pemba tumeweza kufanya utafiti huo.

Mhe. Naibu Spika, na swali lake kuhusu wizara kuwa na utaratibu mahsusi kuzitambua shehia zote za Unguja na Pemba. Mhe. Naibu Spika, ni kwamba bado wizara haijasita utaratibu ulioanza tangu mwaka 2009 na bado tunaendelea na kuhakikisha tunaweza kuzitambua shehia zote za Unguja na Pemba ambazo watoto wanaoishi katika mazingira magumu zipo. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Bihindi Hamad Khamis: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri kwanza nikupongeze kwa kujibu maswali yako kwa ufasaha na utulivu. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Naibu Waziri amesema kwenye swali lake mama kuwa amefanya utafiti shehia sita za Unguja. Je, Pemba ni shehia ngapi ambazo umezifanyia utafiti Wilaya ya Mkoani, Wilaya ya Chake-Chake, Wilaya ya Wete na Wilaya ya Micheweni.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la

nyongeza. Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa Pemba shehia ambazo tumeweza kuzifanyia utafiti ni kama ifuatavyo.

Ni Shehia ya Pujini, Wawi, Tibirinzi, Chanjaani, Wara, Kichungwani, Msingini, Ziwani, Chachani na Mjini Ole. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kunipatia nafasi hii nikaweza kuuliza swali moja la nyongeza.

a) Mhe. Naibu Waziri katika majibu yako mama ulisema kama mnashirikiana na wadau. Hivyo, nataka kujua hawa wadau ambao wanashirikiana nao katika kusadia watoto ambao wanaishi katika mazingira magumu.

b) Je, hizo fedha ambazo idara inasaidia zinatoka kwenye kifungu gani cha fedha.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Ni kweli katika jibu langu mama nimesema kwamba kuna wadau ambao tunashirikiana nao katika kuhakikisha hawa watoto wenye mazingira magumu wanapata kisaidizi. Mhe. Naibu Spika, wadau hawa ambao tunashirikiana ni *TASAF*, *PACT* na Kizazi Kipya.

b) Mhe. Naibu Spika, kuhusu hiyo fedha aliyotaka kujua ni kwamba tunawasaidia watoto wanaishi katika mazingira magumu. Napenda kumjibu kwamba kifungu kile tunatenga bajeti maalum

kwa mujibu wa *OC* zetu. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Nam. 33

Ahadi ya Kujenga Hospitali Binguni

Mhe. Simai Mohammed Said - Aliuliza:

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, lakini bado napata kigugumizi hapa, Mhe. Hamad Abdalla Rashid anashindwa kuelewa kwamba ulimkusudia Mhe. Mussa Foum Mussa wa Kiwani au Mhe. Mussa Ali Mussa.

Katika utekelezaji wa Ilani ya CCM 2015 – 2020, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliahidi kujenga hospitali Binguni.

(a) Je, ni hatua gani ambazo zimefikiwa hadi hivi sasa.

(b) Ni utaratibu upi utakaotumika na Wizara ya Afya kuhakikisha ajira zitakazotoka na ujenzi huo zitawanufaisha wananchi wa eneo husika hasa maeneo ya Dunga, Mtakuja, Binguni na Tunguu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 33 lenye vipengele (a) na (b) kwa pamoja kama hivi ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika, ni kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya uongozi wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein katika kutekeleza Ilani ya

CCM ya mwaka 2015-2020 iliahidi kujenga hospitali kubwa na ya mfano kule Binguni.

Mhe. Naibu Spika, napenda kumthibitishia Mhe. Mwakilishi, wananchi pamoja na Baraza lako tukufu kwamba dhamira hiyo njema ya serikali bado ipo na hatua iliyofikia katika ujenzi huo ni kufanyika kwa *feasibility study* inayofanywa na wataalamu kutoka Netherlands. Pia wizara iko katika hatua ya kuzungusha nguzo kwenye eneo lote na kuweka mabango ya matangazo yanayoonesha umiliki, ili kuepusha uvamizi wa eneo hilo.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu suala la utaratibu gani utakaotumika na Wizara ya Afya kuhakikisha ajira katika ujenzi huo zinawanufaisha zaidi wananchi wa eneo husika. Naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kwamba wizara itamshauri na kumshajihisha mkandarasi atayeshinda tenda ya ujenzi wa hospitali hiyo kuwaajiri mafundi wataalamu tulionao hapa Zanzibar kwanza, na kuwapa kipaumbele zaidi wanaotoka katika maeneo ya Dunga, Mtakuja, Binguni na Tunguu.

Aidha, kwa vile kazi za zitakazotokana na ujenzi wa hospitali hiyo kama kazi za kibarua na kadhalika wizara yangu itamtaka mkandarasi huyo kuwapatia wananchi wa vijiji vilivyoanishwa kwa mujibu wa makubalina yatakayofanyika. Tunawaomba wananchi muendelee kuiamini serikali yenu pia mtoe mashirikiano wakati utakapowadia. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi kumpongeza sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu mazuri ambayo ameyatoa. Mhe. Naibu Spika, naomba niulize swali dogo la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

a) Mhe. Naibu Spika, kwakuwa eneo hili la Binguni tayari hivi sasa kuna ujenzi umekuwa unaendelea na taasisi ambayo

isiyokuwa ya kidini, isiyokuwa ya kiserikali ni raia kutoka nchi ya Kuwait na majengo tayari yameshasimama. Je, serikali imejipanga vipi kuhakikisha kwamba hawa watu ambao wanafanya kazi katika kusaidia jamii na ujenzi uliofanyika wanalipwa fidia yao, ili kuhakikisha kwamba hawaleti mzozo au mgogoro baina ya taasisi hii na serikali.

b) Kwakuwa eneo hili la Binguni wananchi wengi maeneo haya wanategemea kilimo hasa katika maeneo ya Binguni, Mtakuja, Dunga Kiembeni mpaka huku maeneo ya Tunguu. Je, serikali imejipangaje kuhakikisha kwamba takataka na uchafu wote utakaotokana na hospitali hii hautakuwa kero na kuweka maradhi katika maeneo hasa wananchi kwenye hii Wilaya ya Kati na katika vijiji ambavyo vipo katika eneo hilo la Binguni. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi naomba kumjibu swali lake la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, taasisi ambayo imejenga pale ni taasisi ya *Africa Muslim Agency* na ni kweli kwamba wamejenga katika hatua kubwa na nzuri. Hivyo, kutokana na hatua ile ambayo wamefikia kwanza nataka nimuhakikishie kwamba serikali yetu ni sikivu inajua hasara na faida ya kila taasisi. Kwahiyo, itakaa na ifanye mazungumzo na taasisi hii na hatua hiyo imeshaanza ya kupanga mipango ya kukaa nao na kufanya mazungumzo nao. Kwa vyovyote vile itakavyokuwa basi serikali itafanya makubaliano yenye manufaa kwa pande zote mbili. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Mwakilishi aondoshe wasi wasi kwamba taasisi ile haitapata hasara na ni taasisi kwa kweli tunayoiamini, ni taasisi ya kizalendo ambayo inajitolea kufanya kazi kwa kuwasaidia wananchi wenzangu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kuhusu swali lake la hofu ya takataka pamoja na mambo mengine ambayo hayastahili kuwasumbua wananchi wa eneo lake la Tunguu katika hospitali ile. Mhe. Naibu Spika, hospitali hii itajengwa kitaalamu sana na tunakuhakikishia kwamba takataka zote zitakuwa zinadhibitiwa katika sehemu maalum. Kutakuwa kuna *incinerator* zisizopungua mbili ambazo zitahifadhi takataka hizo ili zisiwasumbue wananchi wa vijiji vya karibu.

Mhe. Hamida Abdalla Issa: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kuniona pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri ningependa kumuuliza swali moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

a) Mhe. Naibu Spika, katika majibu mama ya Mhe. Naibu Waziri alidhihirisha kwamba katika hilo eneo la Binguni mmeshafanya *feasibility study*. Je, ni utaratibu gani uliotumika katika kumpata mtaalamu huyo ambaye amefanya hiyo *feasibility study*.

b) Je, ni gharama ya kiasi gani cha fedha iliyotumika katika *study* hiyo. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, wizara yetu ina wataalamu mbali mbali kwa vile tunajikita katika kujenga majengo mbalimbali ya hospitali pamoja na vituo vya afya, basi tuna utaratibu maalum ambao unatuwezesha kupata wataalamu wa kufanya *feasibility study* pamoja na mambo mengine katika vituo vyetu vya afya pamoja na hospitali. Kwahiyo, utaratibu huo ndio uliotumika wa kumpata huyu kutoka Netherlands.

Kuhusu swali lake jengine gharama ambayo itapatikana hapa mpaka sasa bado haijajuulikana kwasababu bado anaendelea na

kazi hiyo na mara atakapomaliza tutajua kwamba tumegharimika kiasi gani na tutamjuilisha Mhe. Mwakilishi kwa maandishi.

Mhe. Machano Othman Said: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kuniona na kunipa fursa ya kuuliza swali lenye (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Katika majibu ya Mhe. Naibu Waziri alisema alikiri kwamba eneo hilo kuna ujenzi wa *Africa Muslim Agency* na alisema kwamba serikali ni sikivu watakaa kuzungumza, swali langu lipo hapa. Je, hawa *Africa Muslim Agency* walipokwenda kujenga hii Wizara ya Afya ilikuwa haina *title deed*, na kama anayo kwa nini wakawaruhusu wakajenga.

(b) Katika nia njema ya Mhe. Rais wa Zanzibar ya kutoa huduma bora za afya kwa wananchi. Mhe. Rais alitembelea katika awamu yake ya kwanza eneo la Mbuzini ambako kunajengwa hospitali na alitoa maagizo kwamba hospitali ile imalizwe iwe ya Wilaya ya Magharibi 'A', lakini sasa zaidi ya miaka saba bado iko vile vile. Je, bado Wizara ya Afya lile eneo la Mbuzini liko kwao au wamelirejesha Tawala za Mikoa? Kama hawajalirejesha ni lini wananchi wengi wa Wilaya ya Magharibi 'A' watarajie kwamba hospitali ile itamalizwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake lenye (a) na (b) kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu *African Muslims Agency* walipoingia kujenga katika eneo lile kwamba Wizara ya Afya hatukufahamu tulikuwa wapi.

a) Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu kwamba, eneo lile walipoingia *African Muslims* Wizara ya Afya tulikuwepo lakini

kutokana na kasoro chache ndogo zilizotokea baina ya taasisi ambayo inatoa Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira pamoja na Serikali ya Mkoa kidogo ilileta sintafahamu na taasisi ile ikafika mpaka hatua ya kujenga majengo yale, baadae tulipoligundua hilo kwamba kuna sintafahamu kidogo basi taasisi hizi tatu zilikaa, yaani Wizara ya Afya, Wizara ya Ardhi pamoja na Mkuu wa Mkoa wa Kusini, tukazungumza pamoja na kupanga ndio hatua zikaanza kuchukuliwa.

Mhe. Naibu Spika, tulishindwa kuchukua hatua kali hasa kwa vile *African Muslims Agency* ni taasisi ambayo iko karibu sana na wananchi na ni taasisi ya kizalendo, tukaona tusi-*force* katika kukosea kwake hakukosea sana, ilikuwa yumo katika mipango ya kutaka kuwasaidia wananchi.

b) Kuhusu Kituo cha Mbuzini Mhe. Naibu Spika. Wizara ya Afya inakitambua kile kituo na kimo katika mpango mkuu wa kukimalizia. Labda niseme kwamba, tumekwama kitu kidogo ambacho kinatusumbua, lakini *finally* kinaweza kikawezekana kwa uwezo wa *Allah*. Kila taasisi ambayo tunaipeleka ili isaidie kumalizia pale basi wanataka waanze mwanzo, wanataka wavunje lile jengo ili waanze tangu *foundation* kujenga katika *plan* nyengine. Hili linatufanya tuwe wagumu kuwaruhusu kufanya hivyo na naona *finally* tunaweza tukashirikiana na Tawala za Mikoa ili kuweza kujua tunalimalizaje jengo lile. Hatutaacha nguvu za wananchi zikapotea tunamhakikishia kwamba kile kituo mwisho wa siku tutahakikisha kinafanya kazi kwa wananchi.

Nam. 8

Mpango Bora wa Ujenzi Maeneo ya Fumba

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza:

Kwakuwa, wizara ina programu ndogo ya upangaji wa matumizi bora ya ardhi na kwasababu maeneo ya Kombeni, Kisakasaka, Dimani, Nyamanzi hadi Fumba ni maeneo ambayo ujenzi wake ni wa kisasa lakini bado kuna tatizo la kujenga majumba bila ya kufuata mpango bora wa upangaji wa miji.

(a) Je, wizara ina mpango gani wa kusimamia ujenzi kwa maeneo hayo, ili kuhakikisha kwamba maeneo hayo yamepimwa na ili watu waweze kujenga nyumba zao kwa mujibu wa maelekezo ya upangaji bora wa mji, ili kuepuka ujenzi holela kwa maeneo hayo.

(b) Je, wataalamu katika sekta ya upangaji wa matumizi bora ya ardhi wana utaratibu wa kuyakagua maeneo hayo, ili kutoa taaluma za aina ya ujenzi na upangaji wa miji kwa eneo hilo ukitilia maanani kwamba maeneo mengi ya huko yanajengwa miji mikubwa ya kisasa.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 8 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, ni kweli kuwa maeneo ya Kombeni, Kisakasaka, Dimani, Nyamanzi hadi Fumba ni maeneo ambayo ujenzi wake ni wa kisasa zaidi, lakini bado kuna tatizo la kujenga nyumba bila ya kufuata mpango bora wa upangaji wa miji. Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kupitia programu ndogo ya Upangaji wa Miji na Matumizi Bora ya Ardhi, ilikwishaandaa Mpango Mkuu wa Matumizi ya Ardhi ya Mji wa Zanzibar na kuidhinishwa na serikali mwaka 2015.

Mpango huo ambao unajumuisha ukanda wa Kisauni hadi Fumba umeanza kutayarishiwa mipango midogo midogo ya kina ya matumizi ya ardhi, ambapo utekelezwaji na usimamizi wake unafanywa kwa pamoja na mamlaka husika na uendelezaji wa maeneo hayo kama vile Baraza la Manispa ya Magharibi B', Mamlaka ya Ukuzaji Vitega Uchumi, Kamati ya Udhibiti, Uendelezaji wa Ujenzi (*DCU*) na Kamisheni ya Ardhi. Hivi sasa maeneo hayo ujenzi holela umeanza kudhibitiwa na wahusika kuchukuliwa hatua za kisheria.

(b) Mhe. Naibu Spika, mbali na wataalamu wa sekta ya upangaji wa miji na matumizi bora ya ardhi, lakini pia *DCU* inaundwa na sekta za kitaalamu za Ujenzi, Mazingira na Miundombinu wana utaratibu wa kila wiki wa kuyakagua maeneo hayo, ili kutoa taaluma za upangaji wa miji na aina ya ujenzi kwa maeneo mbali mbali ya Mji wa Zanzibar na kudhibiti ujenzi holela. Ahsante sana.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa ruhusa ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali dogo la nyongeza lenye kifungu a na b. Kwakuwa amekiri kwamba maeneo hayo ujenzi wake ni wa kisasa na kila mtu anafahamu hivyo. Kwakuwa ameeleza kwamba hii *DCU* inaundwa na wataalamu wa mambo ya ujenzi.

(a) Kwahiyo, nataka kujua ni lini hao *DCU* ambao wameundwa na hao wataalamu walifika kwenye hayo maeneo, ili wakabaini kwamba ujenzi huo hauendelei.

(b) Ni lini timu hiyo ya wataalamu wataungana na uongozi wa Dimani kama vile Mbunge, Mwakilishi, Diwani na Masheha wa maeneo hayo, ili kuwasikia wananchi wakawapa taaluma juu

ya matumizi bora ya ardhi ambapo yale mashamba ni yao ya asili wakaweza kupanga miji na kuweza kupanga utaratibu mzuri wa majengo ambayo yatasaidia na yatapendesha miji hiyo kwa maslahi yao na ya taifa kwa jumla. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

(a) Mhe. Naibu Spika, ni kwamba kila siku ya Alkhamisi hawa wana utaratibu wa kutembelea maeneo kwa ajili ya kukagua, kutoa taaluma, ushauri na kuchukua hatua.

(b) Lakini utayari wa *DCU* ipo tayari siku zote kushirikiana na waheshimiwa hasa hao aliowataja wa Jimbo la Dimani, lakini na wengine wote, wadau wote. Kwahiyo, naomba mashirikiano ili kufikia hilo lengo ambalo tunalitamani sote Mhe. Mjumbe. Ahsante sana.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii na mimi niulize swali la nyongeza kwa Mhe. Naibu Waziri. Pamoja na majibu mazuri aliyojibu naomba nimuulize swali lenye (a) na (b).

(a) Kwakuwa sambamba na kupima na kusimamia ujenzi wa maeneo ya waliyopimwa kwa ujenzi wa nyumba za kuishi. Je, wataalamu wa Sekta ya Upangaji wa Matumizi Bora ya Ardhi wanalizingatia suala zima la kujenga maeneo ya viwanja vya michezo pamoja na nyumba za ibada, kwa ajili ya watoto wetu pamoja na sehemu za ibada ambazo zimezunguka maeneo hayo.

(b) Je, kamati hii ya udhibiti uendelezaji wa ujenzi ya *DCU* na Kamisheni ya Ardhi inafanya kazi kwa maeneo ya ujenzi

wa miji wa Zanzibar tu au hata Pemba inafanya kazi katika kusimamia vijiji na miji inayoanza kujengwa katika maeneo hayo. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, minong'ono mpunguze. Mhe. Waziri majibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante, Mhe. Naibu Spika, suala (a) sikulipata vizuri, sasa sijui nijibu hili ama utampa nafasi arejee ili nipate kusikia vizuri.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Mhe. Naibu Spika, ni yeye kwasababu hakulipata vizuri ni kutokana na minong'ono ambayo imekithiri Barazani. Naomba tuwe watulivu Waheshimiwa Wajumbe.

Swali langu ni kwamba, sambamba na kupimwa na kusimamia ujenzi wa maeneo yaliyopimwa ya ujenzi wa nyumba za kuishi. Je, katika kusimamia huko wanazingatia kuweka maeneo ambayo yatatumika kwa viwanja vya michezo kwa watoto wetu pamoja na nyumba za ibada.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:

(a) Mhe. Naibu Spika, ni kwamba inazingatiwa kuweko kwa viwanja vya michezo.

(b) *DCU* inatakiwa ifanye kazi mote Pemba na Unguja na sasa wapo katika hatua za kuchukua picha kwa ajili ya kupanga miji ya Pemba. Ahsante sana.

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kuniruhusu kuuliza swali dogo la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, kabla sijauliza swali la nyongeza nilikuwa nina neno dogo tu la kuwataka washabiki na wanachama wenzangu wa Timu ya Simba tulie kutokana na matokeo mabaya ya jana ya *draw* na tujue kwamba kuteleza sio kuangauka. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, baada ya taarifa hiyo ndogo tu nataka nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri nataka nimueleze kwamba, mara nyingi wanaojenga ujenzi holela ama wanaovamia maeneo yasiostahiki ni wanyonge ambao wamekata tamaa ya kupatiwa viwanja rasmi katika maisha yao na huwa wanatangatanga kwa muda mrefu na kufikia pahala kukata tamaa.

(a) Je, Mhe. Naibu Waziri ni lini wizara yake itakamilisha kupima viwanja ilivyovitaja kwenye bajeti ya mwaka 2017 na 2018.

(b) Katika Sherehe za Mapinduzi katika hotuba ya Mhe. Rais kupitia wizara yake ilizungumza kwamba wana mipango ya kugawa viwanja hivi karibuni visivyopungua 1,400. Nataka kujua utekelezaji na hatua ya viwanja hivyo wameshavipima na vingapi wameshavigawa.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumuweka sawa kwanza maelezo aliyoyatoa Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Kwahani kuhusu Mhe. Rais katika hotuba yake ya tarehe 12 Januari. Amesema Wizara ya Ardhi itatoa jumla ya hati 1,400 hakuzungumza suala la ugawaji wa viwanja, alizungumza itatoa jumla ya hati 1,400. Kwahivyo, kwanza kabla Naibu Waziri hajajibu nilikuwa naomba niweke kumbukumbu sawa. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Naibu Spika, baada ya ufafanuzi wa Mhe. Waziri naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

a) Kwanza naomba kumfahamisha kwamba wanaojenga kiholela sio masikini tu, bali anayejenga holela ni wale wote ambao hawafuati utaratibu aidha tajiri ama masikini na sheria ipo kwa wote, tunachokiomba ni mashirikiano.

b) Kwamba lini vitapimwa viwanja? Niseme kwamba tutaendelea na utaratibu na vikiwa tayari basi tutajuilishwa. Lakini kwa upande wa Pemba tumesema vishakuwa tayari, vishapimwa lakini tunapima na kwa upande wa Unguja. Lini basi, nitakaa na Mhe. Waziri kuona lini vinapimwa viwanja hivyo. Ahsante sana.

Nam 26

Uimarishaji wa Usafiri kwa Barabara ya Unguja Ukuu – Uzi

Mhe. Simai Mohamed Said - Aliuliza:

Katika majumuisho ya bajeti ya mwaka 2017/2018, Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji ilijipanga kupata mshauri, ili kuondoa kero kwa wananchi wa Kisiwa cha Uzi katika kuimarisha barabara ya kutoka Unguja Ukuu kupitia kwenye mikoko kuelekea Uzi.

Ni hatua gani zimefikiwa na hadi sasa ni maamuzi yepi yamechukuliwa na serikali.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 26 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, wizara yetu kupitia Idara ya *UUB* kwa kushirikiana na wananchi wa Uzi tuliweza kufanya kazi za ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha kokoto na zege hadi hapo ilipofikia, ili iweze kupitika wakati taratibu za kuipatia ufumbuzi wa kudumu namna gani ya kuitengeneza barabara hiyo zinaendelea. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Simai Mohamed Said: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. Kwanza nitoe masikitiko yangu juu ya majibu haya ambayo wananchi wa Kisiwa cha Uzi wamepatiwa hapa. Kwa sababu majibu haya ukiyaangalia hayana takwimu, hayana idadi, hayana fedha, nashindwa hata kuuliza swali la nyongeza. Haya labda niulize tu swali dogo la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Kisiwa cha Uzi kinategemea hii barabara, ili uweze kuvuka pale maji yanapotoka, lakini maji yanapojaa inabidi aidha uchukue kihori au upande boti wende zako uweze kuvuka. Hadi leo kwa takwimu nilizokuwanazo mimi ninazozijua ni waziri mmoja tu ambaye amefika Kisiwa cha Uzi kwa ziara rasmi ni Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto.

Je, ni lini mawaziri wengine watafanya ziara rasmi katika Kisiwa cha Uzi, ili kuwasaidia wananchi wetu hawa wa kisiwa hiki. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Simai Mohamed Mhe. Waziri huyu ni Mhe. Waziri wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji yeye hahusiki na mawizara yote, unapouliza lini mawaziri

watafanya ziara unakusudia mawizara yote au unakusudia *specifically* kwa wizara hii.

Mhe. Simai Mohamed Said: Mhe. Naibu Spika, hata waziri mwenye dhamana na wizara hii hajawahi kufika kisiwa cha Uzi na barabara majibu niliyopewa haya nashindwa hata kuuliza swali la nyongeza. Kwasababu barabara hii imekuwa kero kwa miaka mingi nenda rudi, sasa hivi wanajenga barabara hapo kwa kokoto anasema sio serikali ni yeye anayejenga. Sasa ukiangalia haya majibu ni mistari mitatu yanakwenda sambamba na swali nililouliza. Najua waziri mwenye wizara hii anatumia *model* ya Uingereza ni *West Minister* na Naibu Waziri yeye ndio anajibu kila kitu. Kwahivyo, bora nimuulize kwa Kingereza tu kwasababu Waziri Muingereza, anatumia Bunge la Uingereza.

Mhe. Naibu Spika: Sawa tumekuelewa Mheshimiwa. Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji nimjibu Mheshimiwa ifuatavyo. Kwanza serikali inafanya kazi kwa pamoja kwa hivyo waziri yeyote anapotembelea pahala huwa amekwenda pale sio tu kwa wizara yake lakini kwa niaba ya serikali. Mimi mwenyewe binafsi nimeshafika Uzi nimetembelea, nimeona mazingira yalivyo, uchafuzi wa mazingira, matatizo ya barabara nimeyaona na tumewasiliana na mwenzangu kumueleza kwamba kuna haja ya kukaa pamoja kuona ni kiasi gani tunaweza kutatua tatizo la barabara ya Uzi. Kwa hivyo, sisi kama serikali tunafanya kazi kama timu. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, awali ya yote napenda kulitaarifu Baraza lako tukufu kwamba, kwa mujibu wa swali

alivyouliza Mhe. Simai Mohamed hakutaka kujua kiwango cha kiasi gani na swali limefahamika wazi.

Lakini sasa napenda kumjibu tu kwamba, barabara ile tumeshatembelea mawaziri wengi Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi keshatembelea barabara ile, mimi mwenyewe nimetembelea zaidi ya mara nne barabara ile na nimekwenda kukutana na hao watengezaji wa barabara na shilingi milioni 20 mpaka sasa hivi imetoa serikali kwa ajili ya kuangalia. Kwasababu yale ni mazingira maalum ya Uzi, pale ni sehemu ya maji ya chumvi tumejenga kipande kile ambacho yeye mwenyewe anakijua kwa ajili ya kufanya utafiti ili tuangalie sasa je, ujenzi ule wa zege utaweza kuendelea na utadumu au ujenzi gani? Baada ya hapo sisi tutachukua hatua serikalini.

Nataka kumuarifu tu kwamba yeye pia kafanya kazi kule baada ya Uzi mpaka Ng'ambwa na nimeambiwa lakini wanamuomba vile vile kuna sehemu uendelee kuwaona kwa sababu ile kazi aliyoifanya ni nzuri. Kwahivyo, mimi nataka kumwambia kwamba serikali inafanya kazi na inawajibika wakati wowote na mimi kila wakati nakuwa nazitembelea hizi barabara ikiwemo barabara ile na ni mara nne tokea mimi niteuliwe kuwa Naibu Waziri wa wizara hii. Ahsante Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Naibu Waziri lakini nafikiria kauli yako ile ya mwanzo ya kusema kwamba hajauliza wakati mwengine kwenye majibu Waheshimiwa Mawaziri majibu mengine lazima watu waende *one mail ahead*, haiwezekani yaani hatua zaidi ya ile moja, haiwezekani ujibu kile kile na wakati unajua swali jengine la nyongeza linaweza kuja kama lile. *(Makofi)*

Kwahiyo, Mhe. Mwakilishi hajauliza lakini ni haki kupata na taarifa nyengine ambazo zinahusiana na suala lile. Mimi nafikiria hilo lazima muwe makini Waheshimiwa Mawaziri. *(Makofi)*

Naam! Mhe. Rashid Makame Shamsi.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza suala dogo sana la nyongeza. Lakini nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa majibu sahihi vilevile kwa juhudi za serikali katika kuona kwamba wananchi wa Uzi wanapata ufumbuzi wa barabara yao.

Mhe. Naibu Spika, nimuulize Mhe. Naibu Waziri kwamba katika ujenzi huo na inavyoonekana kwa maelezo ni kwamba ujenzi wa majaribio katika kufanya utafiti. Ni kilomita ngapi ambazo zimejengwa na utafiti huu utachukuwa muda gani mpaka kuweza kupata *solution* la tatizo la wananchi wetu wa Uzi. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji napenda kumjibu Mhe. Rashid Makame Shamsi swali lake kama ifuatavyo:-

Sehemu ambayo tumejenga kwa zege haipungui mita 70 na vilevile kama nilivyosema mwanzo ile lazima barabara ifanyiwe utafiti na kuonekana kwamba je, tukijenga kwa kokoto au kwa zege au kwa lami itaweza kudumu vipi. Kwahiyo, ile ni kama *pilot project* ya pale sehemu tulianza baada ya hapo tutakaa na wale watafiti tutakuja kutoa taarifa kwamba na ule utafiti je, umefanikiwa au tuendelee ya aina gani ya kuijenga ile barabara. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Tunaendelea.

HOJA ZA KAMATI

Ripoti ya Kamati ya Fedha Biashara na Kilimo mwaka 2017/2018

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa nikushukuru sana kwa kuniona leo shingo yako haiumi na vile vile nimesimama kwa kanuni ya 42 fasili ya 9 (a). Mhe. Naibu Spika, jambo ambalo nataka kulisema ni jambo la kuhusu *CT-Scan* ya Hospitali ya Mnazi Mmoja. Kama umeniruhusu naomba niendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe nitakuruhusu lakini naomba kidogo niwatambulishe wageni wetu. Waheshimiwa Wajumbe, leo tuna wageni wetu ambao wageni hao wa Mhe. Mgeni Hassan Juma Naibu Spika, hawa ni vijana wa safari ya CCM 2020 ambao wanatokea sehemu mbalimbali za Tanzania. Jumla yao ni 6 wanaongozwa na ndugu Salum Hamoud Salum. (*Makofi*)

Wengine ni ndugu Ruth Phabian Panhe naomba usimame, Mohd Nassor Khamis, Abdu Wahid Swai, Chiku Marzuk Ali na Barke Haji Mussa. Karibuni sana katika Baraza la Wawakilishi. *(Makofi)*

Mhe. Mohammed Said Mohammed tunaendelea.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Naibu Spika, nilisimama kwa kanuni ambayo niliitaja ya 42 fasili ya 9 (a) kuhusiana na suala zima la *CT Scan* ya Hospitali ya Mnazi mmoja. Nimesimama hoja hiyo sitaki ijadiliwe lakini nataka tamko la serikali, ili kuona jinsi gani wananchi wanapata tamko la serikali hivi sasa.

CT-Scan ya Mnazi Mmoja kiasi cha kipindi cha mwezi mmoja sasa haifanyi kazi na tunajua Hospitali ya Mnazi Mmoja ndio ya

watu masikini, wanyonge wakwezi na wakulima wa nchi hii ambao wanategemea pale. Lakini kwa kipindi kirefu *CT-Scan* imekuwa haifanyi kazi na wanasumbuka kwenda hospitali nyengine bei kubwa sana. Sasa tulikuwa tunataka tu tamko la serikali juu ya jambo hilo. Mhe. Naibu Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri, naona una majibu kabisa.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii na nitaomba nitoe tamko la serikali hapa hapa. Kwa bahati nzuri namshukuru Mhe. Mohamed Said Mohamed kwa kulileta hili.

Lakini jana tamko lilitoka rasmi kwenye vyombo vyetu vya habari kupitia kwa daktari wetu bingwa ambaye sasa hivi ni Kaimu Mkurgenzi wa Hospital ya Mnazi Mmoja anaitwa Dkt Marijani Msafiri alitoa maelezo yote kuhusiana na *CT-Scan* na jinsi hali ilivyo na hatua zinazochukuliwa na serikali, hatua zinazochukuliwa na Wizara ya Feha kupelekwa kwa fedha kwa hao wanaotengeneza mashine hiyo, ili iweze kutengenezwa haraka iwezekanavyo.

Mhe. Naibu Spika, hili nitakuomba wewe na kiti chako pamekuja malalamiko mengi sana kutoka kwa madktari wetu hasa Hospitali ya Mnazi Mmoja kwasababu wamekuwa wakizungumzwa sana hapa Barazani na masuala mengi yalikuwa yakielekezwa kwao, na kwa bahati mbaya kanuni haziwaruhusu wao kuja kujitetea ama kuja kujibu yale masuala na baada yake tunatakiwa sisi viongozi wa serikali tunajibu yale masuala. *(Makofi)*

Kwahiyo, tumeunda utaratibu mpaya kwasababu na wao pia tuliwalamu kwa upande wao kwamba na wao hawatoi taarifa ndio maana Wawakilishi wananchi wanakaa na zile taarifa mpaka

zinafika hapa Barazani kwasababu na wao pia hawatoi yale matamko husika kupitia Vyombo vya Habari,ili kuwaelimisha wananchi pamoja na wagonjwa na wauguzi wao wanaotumia huduma za Hospitali za Hospitali za Mnazi Mmoja.

Mhe. Naibu Spika, tumeunda utaratibu sasa hivi mzuri wa kwamba kila panapotokea suala lolote ambalo linagusa Taifa linagusa wananchi, linagusa wagonjwa, linagusa mazingira yoyote ya hospitali yetu pale ya Taifa ya Mnazi Mmoja basi tamko litatolewa moja kwa moja na wao na kwa nini tumefanay hivyo. Kwasababu kuna sheria mabayo imepitishwa Sheria ya Hospitali ya Mnazi Mmoja ambayo ina bodi yake ina Mwenyekiti wake na sheria ile ilipitishwa humu humu ndani ya Ukumbi wa Baraza la Wawakilishi.

Sheria ile inawataka pia wawe wanatoa taarifa moja kwa moja. Kwa hiyo, tumeunda utaratibu huo ili kusiwe na matatizo au malalamiko kwa upande wa madaktari ambao wanatoa huduma kwa wananchi. Lakini wakati huo huo Waheshimiwa Wawakilishi wanapowasilsiha hoja zao ama masuala ambayo yanawagusa madaktari moja kwa moja kusiwe na mipaka ya kwamba wao hawawezi kuja kujibu zile hoja baada yake hoja zile huwa tunawajibia sisi hapa.

Kwahiyo, utaratibu huo mpya tumeuunda na taarifa iliyotolewa jana naomba niinukuu iliyotolewa jana juu ya *CT Scan* kwamba ni kweli mashine hiyo imeharibika hivi sasa ilikuwa inahitajika dola elfu sitini na sita *invoice* imeshaletwa kutoka *Pacific* Kampuni ya Dar-es-Salaamu na tayari Wizara ya Fedha na Mipango wameshatoa fedha hizo tayari zimeshalipwa pale *Pacific company* ya Dar-es-Salaam wakati wowote mafundi watakuja kutengeneza.

Lakini huo huo muda yaani umri wa matumizi wa mashine hiyo ya *CT-Scan* tayari umeshapita tumepaya *bonus* kwasababu ile

mashine sasa hivi takribani miaka tisa inakaribia miaka kumi na umri ambayo wale *suppliers* waltupa umri wa mashine *life span* au maisha yake ile mashine ni miaka saba. Kwahiyo, tumshapata *bonus* sasa hivi ya miaka miwili tunakwenda kwenye mwaka wa tatu.

Kutokana na hali hiyo, kuna haja ya kubadilisha mashine ile kuleta mashine mpya na hivi sasa serikali katika bajeti yake ya mipango ya bajeti yake kwa mwaka ujao ina mpango wa kununua mashine mpya ya *CT-Scan*. Lakini wakati huo huo jana Dokta Marijani Msafiri ambaye ni Kaimu Mkurugenzi Hospitali ya Mnazi Mmoja alitoa tamko kwamba *MRI* itakuwa inatumika kwa kipindi hichi kufidia *CT-Scan* kwasababu *MRI* ni *more advance* inatoa huduma pana zaidi kuliko *CT-Scan* ingawa hatutakiwi tutumie *MRI* saa zote lakini kwa muda huu wa mahitaji haya maalum *MRI* itaendelea kutumika kwa ajili ya kwamba *CT Scan* haifanyi kazi.

Mhe. Naibu Spika, hilo ndilo tamko rasmi la serikali na jana pia lilitolewa kwenye vyombo vyetu vya habari na mimi naomba nirejee leo mbele ya Baraza lako tukufu na pia kumfahamisha Mhe. Mohamed Said Mohamed na Waheshimiwa Wawakilishi wote pamoja na wananchi. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Afya kwa maelezo yako mazuri. Tunaendelea sasa Waheshimiwa Wajumbe na Ripoti ya Kamati ya Fedha Biashara na Kilimo ya mwaka 2017/2018. Namwita Mhe. Mwenyekiti sasa kwa ajili ya kusoma ripoti.

Ripoti ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo mwaka 2017/2018

Mhe. Yussuf Hassan Iddi (Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha Biashara na Kilimo): Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwanza nikishukuru kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha muhtasari wa Ripoti ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mhe. Naibu Spika, kwa heshima kubwa natanguliza shukurani zangu za dhati kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu ambaye ametujaalia kufika hapa kwa mara nyengine tukiwa wazima wa afya.

Namuomba tena Mwenyezi Mungu akuzidishie wewe Mhe. Naibu Spika, busara, hekma na uadilifu katika kutuongoza na sisi pia atujaalie tuendelee kuwa na nguvu na ari ya kutekeleza vyema majukumu yetu kama tulivyoelekezwa katika sheria na kanuni zetu. Vilevile, sina budi kukushukuru wewe Mhe. Naibu Spika, kwa kunipatia fursa hii kuwasilisha mbele ya Baraza hili Muhtasari wa Ripoti ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kuhusiana na kazi zake zote ilizozifanya tangu ilipowasilisha ripoti ya mwezi wa Febuari 2017, tunaomba kwa ruhusa yako Muhtasari huu usomwe sambamba na Ripoti yetu na ziingizwe kwenye *hansard*.

Mhe. Naibu Spika, kwa namna ya pekee nachukua fursa hii kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein pamoja na Makamu wake wa Pili Mhe. Balozi Seif Ali Iddi kwa ujasiri wa kutekeleza vyema jukumu zima la kuiongoza nchi yetu sambamba na uendelezaji na uimarishaji wa sekta ambazo Kamati yetu inazifuatilia na kuzisimamia.

Mhe. Naibu Spika, kwa dhati kabisa, nitumie fursa hii kutoa shukurani za pekee kwa viongozi na watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi

na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko pamoja na Taasisi zote zilizo chini ya Wizara hizo ambazo Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo inazifuatilia na kuzisimamia kwa mashirikiano makubwa waliyoipatia kamati wakati wa kutekeleza majukumu yetu hadi hii leo kamati yetu ikiwa inawasilisha muhtasari wa ripoti hii mbele ya Baraza lako.

Mhe. Naibu Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wadau na wananchi wote ambao walishiriki kikamilifu pale kamati ilipohitaji kukutana nao, kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake ya msingi, jambo ambalo liliipa faraja kubwa kamati kuona ni kwa kiasi gani wananchi wapo karibu na chombo chao cha Baraza la Wawakilishi na kuthamini juhudi zinazofanywa na Waheshimiwa Wawakilishi wao. Naomba nichukuwe fursa hii kuwaambia kuwa yale yote waliotuachia basi tutayafanyia kazi kwa kadri tutakavyoweza.

Mhe. Naibu Spika, naomba sasa nichukuwe fursa hii kuwashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo pamoja na Makatibu wetu ambao ndio waliofanikisha shughuli nzima kwa ufanisi na umahiri wa hali ya juu. Napenda kuwatambulisha Wajumbe na Makatibu hao kwa kuwataja majina yao kama hivi ifuatavyo:

1. Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Mwenyekiti
2. Mhe. Hamida Abdalla Issa	-	Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Ali Salum Haji	-	Mjumbe
4. Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-	Mjumbe
5. Mhe. Ussi Yahya Haji	-	Mjumbe

6. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Mjumbe

7. Mhe. Hamad Abdalla Rashid - Mjumbe

8. Ndg. Said Khamis Ramadhan - Katibu

9. Ndg. Asma Ali Kassim - Katibu

Mhe. Naibu Spika, Ripoti hii ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo inazisimamia Wizara tatu kama ifuatavyo ni:

1. Wizara ya Fedha na Mipango;
2. Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko; na
3. Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi.

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO

Mhe. Naibu Spika, tuchukuwe fursa hii kumpongeza Dkt. Khalid Salum Mohammed Waziri wa Fedha na Mipango, Katibu Mkuu Ndugu Khamis Mussa Omar, Naibu Katibu Mkuu Ndugu Iddi Haji Makame pamoja na watendaji wengine wa Wizara hii ya Fedha na Mipango pamoja na Afisa Mdhamini wa wizara hii ndugu Ibrahim kwa utendaji wao mzuri katika kutekeleza majukumu yao ya kila siku, Kamati inawaomba sana watendaji hao waongeze zaidi bidii ili kupiga hatua za kiuchumi, kijamii, kisiasa na kiutamaduni.

Mhe. Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kwamba Wizara ya Fedha na Mipango ndio roho ya uchumi wa nchi yetu kwani imepewa jukumu kubwa la kusimamia ukusanyaji wa mapato ya nchi na usimamizi wa matumizi ya fedha za wananchi. Kamati yetu imeridhishwa na juhudi za ukusanyaji wa mapato zinazofanywa na Wizara pamoja na Taasisi zake ikiwemo Bodi ya Mapato ya Zanzibar (*ZRB*) na Mamlaka ya Mapato Tanzania

(*TRA*) jambo ambalo limepelekea kuongezeka kwa makusanyo ya fedha za serikali kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, serikali ilipanga kukusanya jumla ya shilingi 1,059.4 bilioni zikiwemo shilingi 649.4 bilioni zinazotokana na vyanzo vya ndani na shilingi 380 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na shilingi 30 bilioni ni mikopo ya ndani. Hadi kufikia Disemba 2017, jumla ya shilingi 459.47 bilioni zimekusanywa ambazo ni sawa na asilimia 63 ya makadirio ya shilingi 732.87 bilioni ya kipindi hicho na asilimia 42 ya makadirio ya mwaka.

Mhe. Naibu Spika, makusanyo hayo yanajumuisha makusanyo ya vyanzo vya ndani ya jumla ya shilingi 340.30 bilioni na mapato kutoka nje ya jumla ya shilingi 119.17 bilioni. Mapato ya kodi yaliyokusanywa kwa kipindi hiki cha tathmini yamefikia jumla ya shilingi 298.62 bilioni sawa na asilimia 96 ya makadirio ya kipindi hicho ya jumla ya shilingi 311.84 bilioni. Utekelezaji huo umeonesha kukua kwa asilimia 20 kwa mapato ya ndani ukilinganisha ya shilingi 294.59 bilioni ya kipindi kama hicho cha mwaka 2016/2017. Aidha, kwa upande wa mapato ya nje, jumla ya shilingi 119.17 bilioni zimepokelewa zikijumuisha jumla ya shilingi 23.47 bilioni ya ruzuku na jumla shilingi 95.70 bilioni kwa ajili ya mikopo.

Mhe. Naibu Spika, kamati yetu inathamini juhudi hizi za makusanyo lakini naamini kwamba bado tatizo la kuvuja kwa mapato lipo katika maeneo ya ukusanyaji wa mapato na baadhi ya maenei bado hayajafikiwa. Hivyo, kamati yetu inaishauri wizara kupitia taasisi zake za ukusanyaji wa mapato kuondoa muhali na kusimamia matakwa ya sheria, ili kuhakikisha mapato ya nchi hayavuji na kila anayestahiki kulipa kodi anatekeleza wajibu wake na kwa wale wanaokaidi kulipa kodi umefika muda wa

kuwaadhibu kwa kuwatangaza katika vyombo vya habari, ili umma uyatambue makosa wanayoyafanya.

Mhe. Naibu Spika, kufuatia kupitishwa kwa Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Namba 11 ya mwaka 2016 ndani ya Baraza hili, Mamlaka hii inajukumu kwamba la usimamizi, uratibu na uendeshaji wa masuala yote ya ununuzi na uondoshaji wa mali za umma kwa Wizara, Idara na Taasisi zote za Serikali pamoja na Taasisi binafsi zinazofanya manunuzi na Serikali. Kamati imejionea maandalizi ya awali ya Mamlaka hiyo yanaendelea vizuri kwani imefanikiwa kufanya vikao vya kujadili Kanuni ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma, vikao vya kuwatambulisha Wakuu wa Vitengo vya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma, ununuzi wa vifaa vya ofisi, kuandaa Muundo wa Mamlaka yaani *Organization Structure,* kuandaa kazi za kawaida za ofisi.

Hatahivyo, kamati inaiomba serikali kuzitatua changamoto zinazowakabili zikiwemo udogo wa eneo wanalolitumia kwa shughuli za ofisi, ukosefu wa vyombo vya usafiri na kutokuwepo kwa Bodi ya Mamlaka ambako kunakwamisha utoaji wa maamuzi juu ya mambo ya msingi ya utendaji wa shughuli zake.

Mhe. Naibu Spika,Tunaupongeza Uongozi wa Benki ya Watu wa Zanzibar *PBZ* kwa jitihada na mabadiliko makubwa ya kiutendaji hususan kwa kufungua Matawi mapya katika Mtaa mbali mbali ikiwemo Tazara – kule Tanzania Bara, Mtwara pamoja na kufungua kituo cha huduma za kibenki katika eneo la Kiwengwa Mkoa wa Kaskazini - Unguja. Hayo yamefanyika kuhakikisha kwamba wafanyabiashara na wananchi wetu wanapata huduma za kibenki kote nchini kwa urahisi na gharama nafuu zaidi.

Mhe. Naibu Spika,Kamati inaishauri *PBZ* kuhakikisha inafunga Mfumo wake mpya wa yaani *“CORE BANKING SYSTEM”*

utakaokidhi kuwahudumia wateja wengi zaidi kwa muda mfupi ili kwenda sambamba na ongezeko kubwa la wateja kufuatia agizo la Serikali la kufanya malipo ya huduma zake nyingi kama kodi ya uchimbaji wa mchanga, kodi ya nyumba, malipo ya vyeti vya kuzaliwa, mishahara na ulipaji wa huduma za mahakamani kupitia benki moja kwa moja.

Aidha, Kamati inawaomba Waheshimiwa Wajumbe wachukue juhudi za makusudi kuwaelimisha wananchi katika Majimbo yao kuhusu utumiaji wa huduma za Kibenki kupitia mitandao mbalimbali ya simu za mkononi yaani *"INTERNET BANKING*" na huduma za *ATM* ambazo katika maeneo mengi nchini zipo mashine hizo kwani huduma hizo ni rahisi, salama na bora zaidi katika kupunguza msongamano wa watu hususan kipindi cha mwisho wa mwezi ambapo wateja wengi huenda benki kwa ajili ya kuchukua mishahara yao.

Mhe.Naibu Spika, katika suala zima utendaji bora wa majukumu ya kila siku ya Wizara, Kamati inaipongeza Wizara ya Fedha na Mipango kwa ujenzi wa Ofisi yake mpya katika eneo la Gombani Pemba. Ujenzi huo umefikia katika hatua nzuri kwani Kamati imekuwa na kwaida ya kuitembelea eneo hilo kila baada ya muda. Kamati imefanya ziara mara kwa mara katika ujenzi huo na kujionea maendeleo ya ujenzi wa majengo matatu ya Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto pamoja na jengo la Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Aidha, majengo hayo yameshawekewa jiwe la msingi na Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi tarehe 8 Januari, 2018.

Mhe. Naibu Spika, licha ya juhudi za serikali kupitia Mamlaka ya Uchumi *ZIPA* za kuhamasisha na kutafuta wawekezaji kuwekeza nchini lakini inaonekana kuna baadhi ya watendaji na Wananchi bado hawajaielewa kikamilifu dhana hii. Kamati inaishauri *ZIPA*

kuendelea kutoa uelewa kwa wananchi wetu ili dhana na malengo ya kuanzishwa kwa Mamlaka hiyo yaweze kutumia yawekwe wazi na sio tu kwa wananchi wa ndani lakini hata huko nje ya nchi. Aidha, Kamati inatoa wito kwa Wizara ya Fedha na Mipango kupitia *ZIPA* kuandaa utaratibu utakaokua rafiki zaidi kwa Wawekezaji na kuhakikisha utararibu huo hausababishi athari kwa maslahi ya nchi yetu ili kuifanya Zanzibar kupiga hatua kwenye suala la uwekezaji na viwanda vidogo vidogo.

Mhe.Naibu Spika, kamati inaupongeza Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*ZSSF*) kwa kutekeleza Mradi wa ujenzi wa jumba la Treni uliyopo Darajani (*Chawel Building*) kwa kufuata taratibu zote za uhifadhi wa Mji Mkongwe. Mradi huo unatarajiwa kukamilika ndani ya kipindi cha miezi kumi na nane (18) kuanzia Novemba 2016 hadi Mei 2018. Gharama mradi huo zinatarajiwa kuwa ni shilingi 11.2 bilioni. Hadi Kamati ilipotembelea mradi huo, malipo ya jumla ya shilingi 4 bilioni sawa na asilimia 36 ya gharama zote yamefanyika. Ni matumaini ya Kamati yetu kwamba mradi huo utakapokamilika utaimarisha biashara na kuongeza pato la Taifa kutokana na makusanyo ya kodi katika jengo hilo. Aidha kamati inaielekeza *ZSSF* mara baada ya kukamilika kwa ujenzi huo kipaumbele kitolewe kwa wafanyabiashara waliokuwepo awali baada ya kukamilisha taratibu zote za kisheria.

Mhe. Naibu Spika.Kuhusu suala la udhibiti wa mapato kwenye viwanja vya kufurahishia watoto Unguja na Pemba, Kamati imearifiwa kuwa *ZSSF* ina mpango wa kuweka mifumo ya kisasa ya kutumia kadi za kielektroniki katika viwanja vyote vya kufurahishia watoto, ili kuwa na usimamizi mzuri na udhibiti wa mapato. Tunaipongeza sana *ZSSF* kwa juhudi za usimamizi wa mapato katika viwanja vyetu hivyo na tunawaomba waongeze kasi ya ufuatiliaji na usimamizi kwenye miradi mengine ambayo

wanaisimamia ili miradi nayo iweze kumalizika kwa wakati na ilete tija iliyokusudiwa kwa mfuko pamoja na Taifa kwa ujumla. Miradi yenyewe ni Mradi wa nyumba za Mbweni, Mradi wa ukarabati wa jumba la treni na mradi wa ujenzi wa *shopping mall* pale Michenzani.

WIZARA YA BIASHARA, VIWANDA NA MASOKO

Mhe. Naibu Spika, kamati yetu haina budi kuipongeza Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa kujipanga vyema na kuvuka lengo kwa asilimia 163 la makusanyo kupitia vyanzo vyake vikiwemo vya Usajili wa Makampuni, Kazi za Biashara, Usajili wa Majina ya Biashara, Alama za Biashara na Ujira wa kutengeneza nyaraka kwani Wizara kwa kipindi hicho cha miezi sita ilipangiwa kukusanya jumla ya Tzs. 236,201,769 milioni na imefanikiwa kukusanya jumla ya Tzs. 621,897,246 milioni. Aidha, Kamati inaitaka Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko isiridhike na mafanikio hayo yaliyopatikana na badala yake iongeze juhudi katika kuvisimamia vyanzo vyake vya mapato na kuongeza zaidi makusanyo ifikapo mwisho wa mwaka huu.

Mhe. Naibu Spika, wizara hii ni moja katika wizara ambazo imekusanya sekta muhimu sana katika kuimarisha uchumi wa nchi yetu. Ni ukweli usiopingika kuwa nchi nyingi zimeendelea kutokana na kuimarika kwa sekta ya Viwanda na Biashara kwani sekta hizi huinua uchumi wa nchi kwa kasi kubwa sana. Kuimarika kwa sekta hizi hutokana na uwepo kwa Sera na Sheria ambazo zitaweka mazingira mazuri ya kuwavutia wawekezaji kuanzisha viwanda ambavyo baadae hupelekea kuimarika kwa biashara.

Mhe. Naibu Spika,Katika juhudi za kuiendeleza Zanzibar kufikia katika maendeleo ya biashara, Wizara ya Biashara na Viwanda tayari imeshakuwa na Sheria mpya Namba 10 ya 2017 ya

Kuanzisha Baraza la Taifa la Biashara na Kuweka Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo ambayo imepelekea kuundwa kwa Baraza la Taifa la Biashara na tayari Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ameshamteua Katibu Mtendaji wa Baraza hilo. Pamoja na mambo mengine Baraza hilo litakuwa na wajibu wa kuratibu Jukwaa la mazungumzo ya kibiashara baina ya sekta za umma na sekta binafsi ili Wafanyabiashara wetu waweze kupata fursa kisheria ya kukutana na Serikali yao kwa ajili ya kubadilishana mawazo na kuibua maazimio yatakayorahisisha uendeshaji wa biashara Visiwani mwetu kwa maslahi ya pande zote mbili.

Mhe.Naibu Spika,kamati yetu inaipongeza tena Wizara kwa kuhakikisha Sheria Namba 2 ya mwaka 2018 ya Kuanzisha Wakala wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati Pamoja na Kuwezesha Ushajihishaji na Uendelezaji wa Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo (*SMIDA*) imeanzishwa ambayo tayari Wizara imeshaizindua rasmi hivi karibuni. Aidha, ili nchi yetu iweze kupiga hatua za kimaendeleo na kiviwanda, kuwepo kwa *SMIDA* ni jambo la msingi na muhimu kwani kupitia Mfuko maalum wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati unaanzishwa na sheria hiyo utasaidia uendelezwaji wa viwanda viliopo hapa Zanzibar kwa kuwasaidia mitaji kupitia mikopo itakayotolewa kwa wajasiriamali wenye viwanda vidogo vidogo waliokwama kimtaji. Kamati inawataka wajasiriamali kutumia ipasavyo fursa hiyo ili Zanzibar iweze kunyanyuka katika maendeleo ya viwanda.

Mhe.Naibu Spika,kamati yetu inaipongeza Wizara ya Biashara kupitia (*ZSTC*) kwa kuwafariji wananchi ambao walipata ajali kutokana na harakati za kuliokoa zao letu la karafuu. Miongoni mwa faraja hizo ni kuwapatia kifutajasho ambacho husaidia kwa kiasi kikubwa matibabu ya waathirika hao ambapo jumla ya

shilingi 528,309,600 milioni zinatarajiwa kulipiwa kama kifutajasho kwa wahudumiaji wa mashamba ya eka tatu katika Wilaya nne za Pemba. Aidha, Wizara bado inakazi kubwa ya kuhakikisha udhibiti mkubwa wa watoto wadogo waliochini ya umri wa miaka 18 ili wasijihusishe na uchumaji wa zao la karafuu pamoja na kuendelea kutoa elimu juu ya taratibu zinazotakiwa kufuatwa hadi wananchi wetu waweze kupatiwa kifutajasho (*compensation*) baada ya kuanguka katika mikarafuu kwani baadhi ya waathirika hubaki wakisononeka bila ya kupata msaada wowote. Hivyo, Kamati inaishauri Wizara kuviangalia upya viwango vya malipo ya vifutajasho vinavyotumika kwani inaonekana havilingani na wakati tulionao.

Mhe. Naibu Spika, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ilifanya ziara ya siku nne nchini Dubai mnamo tarehe 03 Julai, 2017 hadi tarehe 06 Julai, 2017. Lengo kuu la ziara ilikuwa ni kufuatilia utendaji kazi za Taasisi ya Viwango ya Zanzibar (*ZBS*) kupitia Kampuni ya *"Jabal Kilimanjaro Auto Elect. Mech."* ambayo imeingia Mkataba na Taasisi ya Viwango ya Zanzibar (*ZBS*) mwaka 2016 kushughulikia ukaguzi wa ubora na viwango vya gari zinazonunuliwa na wafanyabiashara nchini Dubai kabla ya kusafirishwa hapa nchini.

Mhe. Naibu Spika,kampuni hiyo ya*"Jabal Kilimanjaro Auto Elect. Mech."*ina Mkataba halali iliyoingia na Taasisi ya Viwango Zanzibar (*ZBS*) pamoja na usajili wa kufanya kazi iliyokusudiwa. Sambamba na hayo, Kampuni inamiliki eneo, vifaa vya kisasa na vya kutosha kufanyia kazi zake pamoja na Wafanyakazi waliopatiwa mafunzo kwani Kamati imebahatika kuona vyeti vya mafunzo waliopatiwa wafanyakazi hao. Kamati inawataka sana Mawakala walioko Dubai ambao wananunua magari nchi za nje kutumia fursa hii ya kufanya ukaguzi wa gari zao kabla ya kufika

Zanzibar ili kuepusha usumbufu na gharama zitakazoweza kujitokeza baadae.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa Tawi la Biashara ya Kimataifa nchini Dubai lililoanzishwa April, 1993 ambalo kiutendaji linasimamiwa na kitengo cha Masoko cha *ZSTC*. Tawi hilo lina Wafanyakazi watatu kutoka nchini India wakiwemo Mhasibu, Mhudumu na Dereva pamoja na Mfanyakazi mmoja ambae huwa anaajiriwa kwa muda kwa ajili ya kutafuta masoko katika kipindi ambacho karafuu zimeingizwa ghalani kule Dubai. Ili kutatua changamoto zinazoikabili *ZSTC*, Kamati inashauri yafuatayo:

a) Kwanza kabisa Wizara itafute njia ya kupunguza gharama za uendeshaji wa Tawi liliopo Dubai pamoja na kumpeleka Mzanzibari atakaekuwa Msimamizi Mkuu wa Tawi hilo ili kuweze kujua mambo yote yanayofanyika na kuweza kuiarifu wizara; (*Makofi*)

b) Wizara ifungue Matawi zaidi katika nchi nyengine zinazotumia karafuu kwa wingi kama vile India iwapo utafiti utakaofanywa utaonesha kama kuna haja ya kuwa na matawi hayo kwa ajili ya kukuza biashara ya karafuu kupitia Matawi yaliyopo nje ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, Serikali imeunda Idara ya Vipimo na Mizani ikiwa na lengo la kuhakiki mizani na vipimo vyote vinavyohusiana na Biashara hapa Zanzibar zikiwemo Mizani zinazotumika madukani, mita za kuuzia mafuta vituoni, mita kubwa zilizopo katika Bohari Kuu za Mafuta (*Flow meter*) ambazo hutumika kwa kuuzia mafuta kwa jumla, uhakiki wa vipimo katika matangi ya kuhifadhia mafuta yaliyopo katika bohari pamoja na vituoni, uhakiki wa mizani kubwa ambazo hutumika kwa kupimia uzito wa mizigo inayopakiwa katika gari

za kubebea mizigo pamoja na kutoa ushauri katika mambo yote yanayohusiana na vipimo katika sekta nyengine zikiwemo afya, teknolojia na mazingira. Kwa kipindi cha Julai - Disemba 2017, Kitengo cha Ukaguzi wa Vipimo na Mizani kimekusanya jumla ya Tzs. 23.7 milioni. Kati ya hizo, Tzs. 18 milioni - Unguja na Tzs. 5.3 milioni - Pemba.

Mhe. Naibu Spika, ingawa watendaji wa Kitengo hiki cha Vipimo na Mizani wanafanya kazi kwa uzalendo wa hali ya juu lakini vifaa wanavyotumia sio vya kisasa na havikidhi mahitaji ya ukaguzi. Aidha, Idara inafanya kazi zake za ukaguzi kwa kutumia gari moja ambayo ni chakavu mno na mara kadhaa hushindwa kutekeleza majukumu yao kutokana na kuharibika mara kwa mara. Sambamba na hilo, Wakaguzi wanafanya kazi katika mazingira magumu kwani hadi sasa Baraza la vipimo ambalo ndilo chombo kikuu cha utoaji wa miongozo ya utendaji wa wakaguzi wa vipimo bado halijaundwa.

Mhe. Naibu Spika, kamati inaiomba Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kuangalia upya muundo wa Kitengo hichi cha Ukaguzi wa Vipimo na Mezani kwa kupitia kitengo hicho kama ilivyo nchi. Kamati inaishauri wizara kuangalia upya muundo kitengo hichi kwani nimebaini kuwa hakuna nchi yoyote duniani inayofanya kazi ya ukaguzi wa vipimo na mezani kwa kupitia kitengo kama ilivyo hapa nchini isipokuwa kuna taasisi maalum yenye mamlaka kamili inayoshughulikia kazi hizo. Aidha, Kamati inaishauri Wizara ianze basi angalau kuwa na Idara ya Vipimo badala ya kuwa na kitengo cha Vipimo chini ya Idara ya Biashara.

Mhe. Naibu Spika, Wakala wa Usajili Biashara na Mali Zanzibar imeanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Wakala wa Usajili wa

Biashara na Mali Zanzibar Namba 13 ya mwaka 2012. Jukumu la msingi la Wakala huu ni kutoa huduma za usajili wa Taasisi za Biashara na Mali kwa wananchi wa Zanzibar na wageni wanaofanya shughuli zao ndani ya Visiwa vya Zanzibar. Wakala tayari imeshaandaa mfumo wa sheria ya usajili wa Taasisi na Mali, Sheria ya Kampuni na sheria ya mfumo wa ufilisi. Kwasasa Wakala inaendelea na kuandaa mfumo wa kusajili biashara *(Bussiness Reformation System*) kupitia mtandao (*online registration*) bila ya kufika Ofisini. Aidha, wakala pia inaendelea na maandalizi ya mfumo wa usajili wa mali zinazohamishika. Lengo la kuwepo mfumo huo ni kuweza kuwasaidia watu waweze kukopesheka kupitia mali zao.

Mhe. Naibu Spika, Wakala huu umejipanga vizuri isipokuwa unahitaji nguvu za pamoja ili kutekeleza majukumu yake kwani bado kuna changamoto zinahitaji kupatiwa ufumbuzi zikiwemo ukosefu wa gari ya kuendeshea shughuli zao. Hadi Kamati inautembelea Wakala huo, kulikuwa na gari moja tu ya Mkurugenzi Mtendaji ambapo kwa mujibu wa sheria wanahitaji kutembelea na kuzikagua Jumuiya za Kiraia (*NGO's*) lakini wanashindwa kutekeleza majukumu. Aidha, Wakala inaufinyu wa nafasi katika Ofisi wanayoitumia pamoja na upungufu wa vitendea kazi na wafanyakazi.

Mhe. Naibu Spika, mnamo tarehe 24 Juni 2017, baadhi ya wajumbe wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo walifanya ziara ya kujifunza kwa kutembelea Mamlaka ya Kusimamia Uzalishaji kwa ajili ya Usafirishaji *'Export Processing Zones Authority'* (*EPZA*) yaliyopo Ubungo Jijini Dar-es-salaam. Lengo kuu la ziara hiyo ilikuwa ni kujifunza namna ya uendelezaji wa maeneo yetu ambayo tumeyatenga kwa ajili ya shughuli za kibiashara kwa Wawekezaji na Wajasiriamali wadogo wadogo.

Mhe. Naibu Spika, kamati iligundua kwamba ili kufikia Zanzibar ya viwanda, suala la urithishaji wa taaluma baina ya kizazi kimoja hadi chengine ni lenye umuhimu wa pekee. Maendeleo ya kweli ya viwanda hayawezi kufikiwa kwa kizazi kimoja pekee, hivyo mipango madhubuti iandaliwe ikiwemo mitaala inayofaa kwa ajili ya uendelezaji wa hatua za kuelekea uzalishaji na usafirishaji kwenye maeneo yetu.

Mhe. Naibu Spika, kufuatia ziara hiyo, kamati inaielekeza Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kuangalia uwezekano wa kuanzisha bidhaa za kipekee yaani *unique products,* ambazo tutazilinda katika soko kwa kuzifanyia *branding*. Kufanya hivyo, kutawavutia wanunuzi wa ndani na nje na kupelekea ongezeko la fedha za kigeni.

Aidha, wizara ijikite katika uanzishwaji wa viwanda ambavyo vitakuwa ni chachu ya kukua kwa sekta za kilimo, ufugaji na uvuvi vikiwemo viwanda vya maziwa, usindikaji wa matunda na samaki, jamu, juisi ni vya kupewa kipaumbele maalum kwa nia ya kuongeza ajira hususan kwa vijana wetu.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie muhutasari wa ripoti yangu kwa wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi.

WIZARA YA KILIMO, MALIASILI, MIFUGO NA UVUVI

Mhe. Naibu Spika, kwa kipindi cha Julai hadi Disemba, 2017 wizara imekadiriwa kukusanya shilingi 3,900,319,400 ambapo hadi Disemba 30, imekusanya jumla ya shilingi 4,916,531,994 sawa na asilimia 126 ya makadirio. Ongezeko hili limetokana na

ukodishwaji wa karafuu na utaratibu mpya wa uchimbaji wa mchanga uliowekwa na serikali.

Mhe. Naibu Spika, ni dhahiri kuwa wizara hii ndio uti wa mgongo wa nchi yetu, uhai wa wananchi wetu upo katika wizara hii. Wizara hii imejumuisha sekta nne muhimu sana katika maisha ya mwanaadamu ambazo ni; sekta ya kilimo, sekta ya maliasili, sekta ya mifugo na sekta ya uvuvi.

Mhe. Naibu Spika, sekta hizi zinahitajika kufanyiwa kazi, kwani wakulima, wafugaji na wavuvi wapate kunufaika na sekta hizi pamoja na wananchi wote, kwasababu kila siku tunakula kwa kupitia kilimo, tunajenga na kupika maliasili, tunawekeza kupitia bidhaa za mifugo na za baharini. Mifano hii ni kuthibitisha kuwa wizara hii ndio uhai wa wananchi wetu na hakuna anaeweza kubeza umuhimu wa kuwepo kwa wizara hii, kwani takriban asilimia 40 ya wananchi wetu inategemea moja kwa moja kipato chao kwa kupitia sekta ya kilimo na zaidi ya asilimia 50 kwa namna moja au nyengine wanategemea sekta ya kilimo, kiuchumi na kiasi cha asilimia 25.7 ya pato la taifa limechangiwa na sekta hizi muhimu.

Mhe. Naibu Spika, suala la kuwepo kwa wataalamu wa kutosha ni jambo lisiloweza kuepukika katika nchi yoyote ambayo inajipanga kupiga hatua ya maendeleo. Moja ya wizara ambayo inatakiwa kuwa na wataalamu wa kutosha basi ni Wizara hii ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, kwasababu wizara hii inatoa huduma moja kwa moja kwa wananchi kupitia sekta zake. Hatahivyo, kamati yetu imebaini kuwepo kwa changamoto ya uhaba wa wataalamu katika wizara hii, jambo linalopelekea malalamiko makubwa kwa wadau wa sekta hizi. Pamoja na jitihada zinazochukuliwa na wizara katika kuhakikisha kuwa inasomesha watumishi wake. Kwahivyo, kamati inaishauri kuweka kipaumbele cha kuwasomesha watumishi wake, ili

kupunguza uhaba wa wataalamu hususan katika kada mabazo ni vigumu kupata wataalamu.

Mhe. Naibu Spika, kamati yetu imeridhishwa na hatua iliyochukuliwa na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi ya kuyakodisha mashamba yote ya serikali ambayo wamiliki wake hawakupatiwa mikataba ya eka tatu. Pia kwa mashamba ambayo wanaostahiki kuyasimamia kwa mujibu wa mikataba ya eka hawapo tena. Katika juhudi za kuyatafuta mashamba hayo, Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi ilikabidhiwa orodha ya mashamba ya eka 8,215 kutoka Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira ambapo baada ya uhakiki iligundulika mashamba halisi yaliyopo ni eka 8,107.

Vilevile, wizara ilipokea orodha ya mashamba ya eka 2,827 kutoka kwa masheha na baada ya kuainisha taarifa hizo za mashamba yatokanayo na madaftari ya wizara inayoshughulikia ardhi na zile za mashamba yatokanayo na orodha za masheha, ilionekana kwamba yapo mashamba 9,982 ambayo baadhi yake yalitolewa mikataba ya eka na mengine hayakuwahi kutolewa mikataba ya aina hiyo.

Mhe. Naibu Spika, hadi kufikia usitishaji wa zoezi la ukodishaji, jumla ya shilingi 2,397,626,000 bilioni zimekodishiwa mashamba ambayo yanategemewa kukusanywa na serikali. Fedha hizo zinatokana na ukodishaji wa mashamba ya eka tatu kwa shilingi 2,072,326,000 bilioni na ukodishaji wa mashamba yanayosimamiwa na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi yaliyokodishwa kwa zabuni kwa shilingi 325,300,000 milioni.

Aidha, hadi kufikia tarehe 19 Januari, 2018 jumla ya shilingi 1,243,048,100 bilioni sawa na asilimia 51.84 ya mategemeo ya fedha hizo ndizo zilizokusanywa. Juhudi zinazoendelea kufanywa

kuhakikisha fedha hizi kwa wale ambao hawajalipa zinalipwa, ni pamoja na kutoa matangazo kwenye radio, pia kuna vikao vilivyofanyika kwa Wakuu wa Wilaya, Mikoa pamoja na waliokodi mashamba, ili kuhakikisha kwamba wanalipa madeni yao wanayodaiwa. Kamati imesikitishwa na kitendo cha kutorudishwa fedha hizo kwa wale waliokodi mashamba ya mikarafuu, na inawataka wananchi waliokodishwa mashamba haya kuhakikisha kwamba wanalipa madeni yao, ili fedha hizi zirudi serikalini kama ilivyokusudiwa.

Mhe. Naibu Spika, jumla ya shilingi 528,309,600 milioni zinatarajiwa kulipiwa kama kifutajasho kwa wahudumiaji wa mashamba ya eka katika Wilaya nne za Pemba katika ukodishaji wa msimu wa mwaka 2017, zikiwemo shilingi 148,456,600 milioni Wete, shilingi 56,074,000 milioni Michweni, shilingi 191,372,000 milioni Mkoani, na shilingi 132,407,000 milioni Chake Chake. Aidha, Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi Ofisi Kuu Pemba, tayari imewasilisha maombi haya ya kifuta jasho kwa wanaohudumia mashamba ya mikarafuu kwa Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya hatua za malipo.

Mhe. Naibu Spika, katika mpango mpya wa kuliendeleza Shamba la Serikali la RAZABA liliopo Bagamoyo. Tayari Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Shirika la Nyumba la Tanzania Bara imeamua kulipima eneo hilo kwa ajili ya kuandaa mpango mpya wa matumizi ya ardhi kulingana na Mpango wa Mji wa Bagamoyo. Hivyo kamati inaitaka wizara ishirikiane na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar kukamilisha mapitio ya '*Memorandum of Understanding'* (*MoU*) ili hatua zinazofaa ziweze kuchukuliwa. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kamati inaipongeza wizara na serikali kwa ujumla kwa maamuzi yake ya busara ya kuupandisha hadhi Msitu wa Kiwengwa kuwa ni miongoni mwa hifadhi tano kubwa kwa

upande wa Kisiwa cha Unguja, zinazoendeshwa kwa mashirikiano ya serikali kupitia Idara ya Misitu na Maliasili zisizorejesheka na vikundi kumi vinavyoizunguka hifadhi hiyo ambavyo ni Pongwe, Kiwengwa, Bambi, Pangeni, Pwani Mchangani, Kandwi, Upenja, Kilombero, Tunduni na Mchangani.

Mhe. Naibu Spika, msitu huo una ukubwa wa hekta 3,406 ambao umepandishwa hadhi na kutangazwa rasmi kuwa Hifadhi ya Taifa mwaka 2002. Hifadhi hiyo ya Taifa ina umuhimu wa kipekee kwani imekusanya viumbe adimu vikiwemo miti, wanyama na ndege kadhaa. Kutokana na kuwepo kwa hifadhi ya msitu wa Kiwengwa, itaiwezesha serikali kulinda, kusimamia na kuhifadhi ipasavyo maliasili na kutunza vyanzo vya maji vilivyomo pamoja na kuendeleza utalii wa kimaumbile kupitia vivutio mbali mbali vikiwemo mapango, wanyama, mila na utamaduni wa wenyeji wa maeneo hayo.
Aidha, serikali kupitia utalii wa kimaumbile, itaweza kupata fedha za kigeni na kuongeza mapato yake kufuatia michango au ada zinazotozwa na wageni wanaoutembelea msitu huo. Kwa sasa watalii wapatao 90 hadi 150 huwa wanautembelea msitu huo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, tunawaomba Waheshimiwa Wajumbe, nao wafanye ziara za kutembelea msitu wa Kiwengwa, ili kuweza kujionea vivutio vilivyokuwemo pale.

Mhe. Naibu Spika, kamati inaisistiza serikali kwamba hadhi iliyopandishwa katika msitu huo iendane sambamba na huduma za hoteli, ili vyakula vya Kizanzibari na vyenginevyo vipatikane kwa watalii wanaofika katika msitu huo. Aidha, wizara ianzishe ‘*zoo’* ya wanyama kwa lengo la kuwafanya wageni wanaoutembelea msitu huo kujionea wanyama mbali mbali wanaopatikana Zanzibar. Kama wizara itayatekeleza haya, hapana shaka mapato ya idara yataongezeka na msitu huo utazidi

kutambuliwa ndani na nje ya nchi yetu. Sambamba na hilo, kamati inaishauri Wizara ya Kilimo, Maliasil, Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango, kuiachia Idara ya Misitu na Maliasili Zisizorejesheka asilimia 30 ya mapato yanayotokana na msitu huo ili yatumike kuuendesha msitu.

Mhe. Naibu Spika, Zanzibar ni kisiwa ambapo wananchi wake pamoja na mambo mengine wanalima mwani kwa ajili ya kujikimu katika maisha yao. Pamoja na juhudi za uzalishaji mwani zinazofanyika, lakini bado wakulima wetu wanasumbuliwa na tatizo la kuwepo kwa bei ndogo ya zao hilo ukilinganisha na nguvu inayotumika katika uzalishaji wake.

Aidha, kilimo hicho kimevamiwa na maradhi ambayo yanawarudisha nyuma wakulima wetu. Sambamba na hayo, wavuvi wetu wanaoanika dagaa wanachangamoto kwa kutumia njia za kizamani za kuanika dagaa, pamoja na kushindilia kwa njia za kienyeji. Hivyo, tunaishauri wizara kuwanunulia wafanyabiashara hao mashine za kukaushia dagaa, ili kuiongezea thamani bidhaa hiyo na kuwawezesha wavuvi na wafanyabiashara wetu kupata faida na walaji kula bidhaa iliyo bora zaidi. Kadhalika, eneo liliopo karibu na shughuli hizo za dagaa hapo Maruhubi, linakabiliwa na tatizo la umwagaji wa maji machafu na kulifanya eneo hilo kuwa hatarishi kwa afya ya wafanyabiashara na walaji wa dagaa.

Mhe. Naibu Spika, tunaiomba serikali ihakikishe rasilimali tuliyonayo ya bahari inatumika ipasavyo kwa lengo la kuimarisha uchumi wa nchi yetu. Tunaamini kuwa Zanzibar inaweza kujiendesha iwapo tutaitumia ipasavyo neema ya bahari aliyotujaalia Mwenyezi Mungu, yenye rasilimali nyingi ndani yake, kwani ipo mifano ya nchi nyingi za visiwa zimefanikiwa kimaendeleo kwa kutumia bahari tu.

Mhe. Naibu Spika, katika juhudi za kufikia lengo la kujitosheleza kwa chakula, Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi inaendeleza kilimo cha mpunga wa umwagiliaji maji kupitia mabonde yake mbali mbali yaliyopo Unguja na Pemba. Kamati inaipongeza wizara kwa kazi hiyo ngumu kwani wakulima wetu wameshajihika sana na kilimo cha umwagiliaji maji kwa kutambua kwamba wakulima wanaolima kilimo cha umwagiliaji maji huwa wanatumia nguvu kidogo na uzalishaji huwa mkubwa.

Vilevile, huweza kulima mara mbili au zaidi kwa mwaka. Katika kutathmini na kusimamia kilimo cha umwagiliaji maji. Kamati ilifanikiwa kutembelea mabonde kadhaa kujionea shughuli za kilimo zilizofanyika katika mabonde hayo yakiwemo Bonde la Cheju, Uzini na Kibondemzungu kwa upande wa Unguja na mabonde ya Mangwena, Makombeni na Ukele kwa upande wa Pemba.

Mhe. Naibu Spika, kiujumla mabonde hayo yanakabiliwa na changamoto zinazofana, zikiwemo kugawika kwa wakulima ambapo katika mabonde ya umwagiliaji maji, kuna wakulima wanalima kilimo shadidi wakati wengine bado wamebakia katika ukulima wa kutegemea mvua, pamoja na kuelezwa faida kubwa iliyopo na umefika muda wakulima wetu kulima kilimo cha kibiashara na kuachana na kilimo cha kujikimu. Changamoto nyengine, wakulima wanaendesha shughuli zao kwa kutumia zana za asili ambazo hutumia nguvu nyingi na kuchukua muda mrefu, jambo ambalo linakwamisha shughuli nyengine za kimaendeleo.

Mhe. Naibu Spika, kamati yetu pia ilifika katika kitalu cha Chanjaani Mwanatojo kinachopatikana Mkoa wa Kaskazini Pemba ambapo hadi kamati inafika eneo hilo, kitalu hicho kilikuwa na jumla ya miche 28,575 ya mikarafuu ambayo imezalishwa kwa nguvukazi ya watendaji wanane. Kiwango cha ustawi wa miche hiyo ni asilimia 53 baada ya kutoka kitaluni

ambayo kiuhalisia huwa inapanda au kushuka kulingana na huduma zitakazotolewa na mkulima mwenyewe. Kiukweli shughuli za uzalishaji miche katika kitalu hicho huwa zinakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa huduma za vyoo jambo ambalo hurudisha nyuma ufanisi wa wafanyakazi hao. Aidha, Sera ya Serikali ya utoaji bure miche ya mikarafuu inatumiwa vibaya na baadhi ya wanajamii, kwani huchukuwa miche vitaluni na kuitelekeza mashambani au majumbani bila ya kuiendeleza miche hiyo.

Mhe. Naibu Spika, katika kufanikisha majukumu yetu ya kikanuni, kamati yetu ilifika Wakala wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo ulianzishwa chini ya Hati ya Kisheria Namba 2 ya mwaka 2011, kwa ajili ya kusimamia na kuimarisha shughuli za karakana za matrekta ziliopo Mbweni na Machomane Pemba, ambapo kwasasa Wakala huo una jumla ya matrekta 35.

Aidha, wakala imepokea Matrekta 10 mapya kutoka ubalozi wa Libya nchini Tanzania, lakini yameshindwa kufanya kazi mara tu baada ya kufika kutokana na kutolewa baadhi ya vifaa huko yalipohifadhiwa. Wakala imepanga kununua vifaa na kuyatengeneza matrekta hayo, ili yaweze kutoa huduma Unguja na Pemba, ambapo hadi kamati inapokea ripoti ya utekelezaji wa malengo ya bajeti ya Wakala huo, Matrekta matatu yalikuwa yameshatengenezwa na yanafanya kazi mashambani.

Mhe. Naibu Spika, maoni na maagizo ya kamati kuhusu mambo yote niliyoyaeleza na ambayo sikuyaeleza hapa, yanaonekana wazi katika ripoti kamili ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya mwaka 2017/2018, ambayo Waheshimiwa Wajumbe tayari mmeshapatiwa. *(Makofi)*

HITIMISHO

Mhe. Naibu Spika, mwisho kabisa, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe, wa Baraza lako tukufu, kwa kunisikiliza kwa utulivu na umakini wa hali ya juu wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha muhtasari huu wa Ripoti ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo.

Sasa naomba nichukue fursa hii kwa mara nyengine nikuombeni nyinyi Waheshimiwa Wajumbe, wa Baraza hili muijadili, mutoe ushauri pamoja na mapendekezo yenu na hatimae muuunge mkono muhtasari huu pamoja na ripoti yake, ili tumuwezeshe waziri kwenda kutekeleza na kufanikisha yale kamati iliyoyaibua, kwa nia njema ya kuwaletea maendeleo wananchi wetu, na baadae nasi tupate fursa ya kuja kumuhoji waziri kwa kile atakachokitekeleza kupitia maagizo yaliyomo katika ripoti ambayo nyote Waheshimiwa Wajumbe mmepatiwa. Baada ya maelezo hayo Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Yussuf Hassan Iddi (Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo) nakushukuru sana. Waheshimiwa Wajumbe, nimepata maombi ya michango ya wajumbe kumi, natarajia sana kwamba mtatumia muda wetu vizuri kwa dakika zetu kumi mtakazozitumia.

Kwahivyo, Waheshimiwa Wajumbe naanza na Mhe. Ali Suleiman Ali Shihata, baada ya hapo atafuata Mhe. Suleiman Makame Ali na ajitayarishe Mhe. Bahati Khamis Kombo. Mhe. Ali Suleiman karibu.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa mbele ya Baraza lako tukufu, kuweza kuchangia Ripoti ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii muhimu ya kwanza. Pili niwapongeze Waheshimiwa Mawaziri wote watatu na Manaibu Mawaziri waliokuwepo, Makatibu Wakuu na Manaibu Katibu Wakuu, Wakurugenzi, Makamishna na wafanyakazi wote wa hizi tatu, hasa tukizingatia kwamba Wizara ya Fedha ni uti wa mgongo, Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko ni uhai wa biashara zetu na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi ni muhimu kwa maisha ya wananchi wetu hasa tunaotegemea kwamba lazima ule ili uishi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, naipongeza kamati kwa kazi nzuri waliyoifanya, kuanzia mwenyekiti wake Makamo Mwenyekiti na wajumbe wote, lakini pamoja na watendaji wote walioshiriki katika kufuatilia mambo mbali mbali, kwasababu tumeona mambo mazuri waliyoyafanya hapa hadi kufika Dubai na kwengineko. Kwahivyo, tunaamini kwamba tunategemea mambo mazuri yamo katika ripoti hii japo kwa ufinyu.

Mhe. Mwenyekiti, nitaanza na Wizara ya Fedha na Mipango katika ukurasa wa tatu. Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri na watendaji wake wote kwa kusimamia vyema shughuli mbali mbali za mapato katika nchi yetu. Tunategemea kwamba bila ya mapato hatuna maendeleo na bila ya kuyahifadhi mapato pia tutakuwa tumefeli. Kwahivyo, nimpongeze sana Mhe. Waziri na watendaji wake wote kwa kazi nzuri wanazoendelea nazo siku hadi siku na ufanisi wa maisha katika serikali yetu tunauona kwa hivyo, nimtakie heri na watendaji wake wote. Lakini hapo hapo katika taasisi zinazojitegemea 2.3

1. Bodi ya Mapato Zanzibar (*ZRB*);
2. Benki ya Watu wa Zanzibar (*PBZ*);
3. Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi (*ZIPA*);
4. Mfuko wa Barabara (*ZFR*);

5. Shirika la Bima (*ZIC*);
6. Bodi ya Rufaa za Kodi (*Tax Appeal Board*);
7. Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*ZSSF*);
8. Mahakama ya Rufaa na;
9. Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali.

Mhe. Naibu Spika, taasisi hizi ni muhimu sana katika Wizara ya Fedha na Mipango, na hizi ndo msukumo wa kupatikana mapato na mambo mengineyo ili tuendelee vizuri, mimi nitatoa ushauri mfupi kwa baadhi ya maeneo.

Kwanza Bodi ya Mapato (*ZRB*) chombo hiki ni muhimu sana kwa nchi yetu na chombo hiki ndo kinachokusanya mapato kutoka sekta mbalimbali ambazo zinahusiana kutokana na sheria, lakini kuna masikitiko kidogo Mhe. Naibu Spika hapa lazima tuyaseme. Wafanyakazi wenye magari wengi magari ya abiria, magari ya mizigo wana malalamiko wanasemea kwamba kodi kubwa sana wanayotoleshwa kwa mwaka.

Kwa mfano, walipokuwa *TRA* wanakusanya kodi ile, walikuwa kwa mwaka wanalipa la mbili, lakini sasa hivi kuna magari yanalipa laki tano, laki saba na kuendelea. Kwahivyo, labda sijui pana nini Mhe. Waziri akija atueleze ili wananchi wasikie kuna tatizo hili na hili ili kwa manufaa ya pande zote mbili. Kwakweli, vijana wetu wengi wanajiajiri katika sekta ya magari na tunategemea wao kama wataweka msimamo mzuri basi watasaidia sana katika maendeleo ya kupata faida katika nchi yetu. *(Makofi)*

Lakini tuseme tu kwamba kama utaratibu utakuwa umewekwa vizuri zaidi mfanyabiashara ataongeza bidii ya kujaza mafuta katika gari yake kuendelea katika kufanya kazi, ili pato liongezeke, tunajua tu kwamaba mafuta ni muhimu na mafuta ni pia njia moja ambayo tunapata fedha kutokana na utaratibu

uliowekwa wa kisheria. Kwahivyo, nimuombe sana Mhe. Waziri ili aje atupatie maelezo kidogo tupate wananchi wetu malalamiko waliokuwa nayo ili wayaweke vizuri..

Mhe. Naibu Spika, Ya pili namba tatu nitasoma Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi hii *ZIPA* naiacha. Mfuko wa Barabara *(ZFR)*, mfuko huu ni muhimu sana na mfuko huu umetupa maendeleo mazuri sana katika barabara zetu. Kwakweli, naipongeza sana serikali na mfuko huu kwa bidii yao ambayo tunaiona mimi katika Jimbo langu na tukiacha jimbo langu na majimbo mengineyo tumefaidika kuona kuna barabara yetu ya Mwanakwerekwe mpaka Fuoni, kuna barabara ya Kwarara Jimbo Kijito Upele. *(Makofi)*

Vilevile, naipongeza serikali kwa dhati kabisa na mfuko huu pia barabara ya Cheju ambayo imejengwa kwa kiwango kikubwa sana na wenzetu hawa wa UUB ningeomba sana namuomba sana Mhe. Waziri. Tatizo letu kwa UUB ni ukosefu wa nyenzo, lakini kama wanapata nyenzo ni wajenzi wazuri kuliko hata hao wengine ambao tunatafuta nje wanachukua fedha zetu nyingi kuliko mfuko huu. Nashauri, naomba sana tuwaenzi wenzetu hawa na tuwapatie vifaa vya kutosha ili UUB wafanye kazi zao vizuri kunusuru fedha zetu za serikali. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, Shirika la Bima la Zanzibar tunalipongeza sana na kazi zao tunaziona sasa hivi wameweka kipindi kizuri wakati wa mawio kwanza anatokea yule Chande sijui nani yule msanii mmoja anatoa tangazo kuhusu Shirika la Bima la Zanzibar sijui nini upate faida kwa sababu kuna moto na mambo mengineyo. Kwahivyo, ushauri wao na vipindi vyao hivi ni uchochezi wa kuleta maendeleo katika Shirika la Bima kulitumia, niwaombe wananchi Shirka la Bima la Zanzibar ni shirika linalopendwa na lina faida sana tuone na sisi kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tuwaelimishe wananchi wetu watumie

shirika hili kwa mambo mbalimbali maana siyo magari tu na mambo mengine ya usalama wao.

Lakini jengine Mhe. Naibu Spika, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*ZSSF*), tushukuru sana kwamba wanaendelea vizuri wenzetu hawa na wanafanya kazi nzuri na wamo katika malengo ambayo yanafikia wakati. Lakini Mhe.Naibu Spika, kuna malalamiko kwa baadhi ya wafanyakazi, kuna wafanyakazi wamelalamika kwenye Kamati yangu ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii sehemu ya mahoteli kuna wafanyakazi wanakatwa fedha hazifiki katika mfuko. Namuhakikishia Mhe Waziri tatizo hili lipo na sisi katika taarifa tumeliweka, lakini hii ndio wizara yake nalisemea hapa hapa, tumekwenda Makangale na kwingineko Pemba tumekuta kadhia hiyo ipo wanakatwa fedha haziingizwi katika mfuko hawapati risiti na hawana chochote wanachoelewa wao wanajua kukatwa tu lakini fedha zao hazijulikani ziko salama kiasi gani. Kwahivyo, hapo nampa njia tu Mhe. Waziri aelewe.

Mhe. Naibu Spika, jengine nitakalozungumza maana muda unakwenda ukurasa wa saba mpaka wa nane Benki Kuu ya Tanzania *BOT* tawi la Zanzibar. Niipongeze serikali kwa dhati kabisa, naipongeza kwa kukusanya mapato mazuri lakini nitakuwa na rai tu kwasababu hapa katika figa yao ukurasa wa nane gawio linalotokana na benki kuu tumeambiwa tu kwamba 2014/2015 SMZ ilipata gawio la bilioni 5.8, mwaka 2015/2016 gawio la jumla lilikuwa bilioni 13.5 ni ongezeko kubwa tunasema tu kwamba tutongeze bidii na tutumie benki kuu ili ipate fedha tuongezewe.

Lakini ushauri namuomba sana Mhe. Waziri Benki Kuu (*BoT*) hivi karibuni iligawa gawio kwa serikali kama bilioni 300 na zaidi, tulishuhudia lakini gawio letu bado limebakia asilimia 4.5. Je, Mhe. Waziri hapa haoni kwamba wakati umefika *rate* yetu

imepanda sana au imeshuka sijui ongezeko limeongezeka bado hakuna mpango wowote wa kufikiria kwamba ongezeko la 4.5 likabadilika, tukenda angalau 6.5 au 7 hili nashauri Mhe. Waziri utaalam anao yeye na watendaji wake tutakuja kupata changamoto.

Mhe. Naibu Spika, lakini ukurasa wa kumi na tano fidia kwa wahanga wa karafuu Shirika la *ZSTC*, mimi siungi mkono suala hili kwa watoto chini ya umri wa miaka kumi na nane kupandishwa mikarafuu, ni suala baya na linaathiri sana watoto wetu mtoto ana umri wake wa kujitegemea, kuanzia miaka kumi na nane chini atakuwa bado kwa wazazi wake lakini keshakuwa mtu mzima. Kwahivyo, hawa watoto hawa lazima wazuiwe kwa mkakati wowote kwasababu katika wengi wanaoathirika wanakuwa wao.

Mhe. Naibu Spika, naomba sana hili tukaliangalia, ili kuondoa hitilafu hizi zinazotokea, lakini katika changamoto inasema udhibiti mdogo wa watoto chini ya umri wa miaka kumi na nane, halafu ukosefu wa elimu juu ya utaratibu wa kufutwa hadhi mwananchi kupatiwa kufuta jasho. Nafikiri Mhe. Naibu Spika, hii hata haitaki mtoto unamlea wewe mzazi au unae wewe anatoka asubuhi anakwenda zake na kapu lake kuchuma karafuu au pakacha lake unamruhusu, linalotokea lake mwenyewe, kwa hivyo mimi ningeshauri sana hili liangaliwe.

Mhe. Naibu Spika, tukija *ZSTC* ukurasa wa kumi na nane Tawi za *ZSTC* Dar-es-salaam nakumbuka toka mimi mdogo *ZSTC* iko Dar-es-salaam tawi, lakini wakati huo tawi hili lilikuwa linashughulika na bidhaa mbalimbali zinazotoka Unguja mfano mafuta ya nazi, Tanzania Bara ilikuwa mafuta ya nazi hakuna au kidogo, tulikuwa na viwanda tele hapa kwa marehemu Sheikh Abass Hussein na kwengineko. Lakini leo tunaambiwa tawi lile bado lipo linafanya kazi gani? Mhe. Naibu Spika, tunamuomba

Mhe. Waziri akija hapa atwambie na tumeona katika ripoti kuna uchakavu wa tawi, linataka linyanyuliwe lifanyiwe gharama mbalimbali faida gani inapatikana katika tawi hili. Kwahiyo, Mhe. Naibu Spika, naomba sana tubadilike kitu kinachotia hasara tusikiendeleze tukaongeza hasara. Kutengeneza ni hasara haina faida na sisi tuliache tuendelee na mengine.

Mhe. Naibu Spika, ukurasa wa ishirini na mbili kwa ufupi muda unakwenda, kiwanda cha ushoni cha Idara maalum za SMZ mimi kiwanda hiki nakiunga mkono sana wanashona nguo nzuri, kike kwa kiume kanzu na mambo mengineyo. Kwahivyo, naomba sana kiwanda hiki kikapatiwa vifaa mbalimbali na umuhimu wake tunauona hivyo nasema tu kwamba tuendelee nao kwa ajili ya maendeleo ya vijana wetu waliopata ajira mle na sisi kupata faida ya kupeleka nguo zetu za watoto na watu wazima.

Mhe. Naibu Spika, ukurasa wa ishirini na tano muundo wa Wizara ya Kilimo huku sina haja nako kuna maidara sina haja nayo lakini nitasoma maeneo ninayotaka kuyachangia. Mhe. tunashukuru au tunaipongeza idara kwa asilimia kubwa kwamba uhakika wa chakula unaonesha kidogo imani wananchi wamevuna mazao mengi, lakini mavuno hayo tunashukuru tumenunua michele yao mizuri na mambo mengine hata kwenye maonesho tuliyaona mengi mazuri. Kwahivyo, tunampongeza Mhe. Waziri na kwa juhudi yake mabondeni haondoki na kwenye mashamba, hivyo tunasema kwamba kitendo anachokifanya Mhe. Waziri wetu wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi na wengine waige ntawasemea kwa wenye mawizara yao hapa namzungumzia Mhe. Waziri wa kilimo anafanya kazi nzuri na anafuatilia usiku na mchana panapotokea hali na kila penye hali.

Mhe. Naibu Spika, lakini jengine nizungumzie suala la mwani, pamoja na matatizo yaliyokuwepo zao la mwani ni mkombozi kwa wanyonge wengi katika nchi yetu. Na hivi sasa hivi niseme tu

kwamba wananchi wetu wanaoishi katika vijiji vyetu vya Kiwengwa, Uroa, Bwejuu, Jambiani na kwengineko ari yao imeshuka sana kwasababu bado zao la mwani halina bei katika soko la ulimwengu au hatujui kuna njia gani. Namuomba Mhe. Waziri, bado atafute masoko watafute wataalamu hasa tukizingatia kwamba mwani mwingi sasa hivi unaharibika na katika kuharibika huko wale wananchi wetu wanazidi kuvunjika moyo.

Kwahivyo, nimuombe sana Mhe. Waziri lakini jengine kilimo bora ni matrekta bado kilimo kinahitaji nguvu za kutumia nyenzo za kisasa, bila matrekta hakuna kilimo jembe la mkono limepitwa na wakati. Mhe. Naibu Spika, nimuombe Mhe. Waziri na hili liangaliwe, ili wananchi wetu wapate matrekta ya kutosha pamoja tumeambiwa kuna matrekta yameshaagizwa na yatafika wakati wowote lakini bado hilo tulitilie mkazo ili liendelee vizuri.

Mhe. Naibu Spika, hapo hapo Kampuni ya Uvuvi Zanzibar *ZAFICO* ...

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe imebakia dakika moja.

Mhe. Ali Suleima Ali: Ah! Haya Mhe. Naibu Spika. *ZAFICO* ni muhimu sana Mhe. Naibu Spika na kampuni hii kama itawekwa katika nchi yetu faida kubwa itapatikana kwa vijana wetu, ajira itaongezeka na fedha pia zitapatikana tunaamini serikali yetu ina mambo mengi ya kufanya ili wananchi wetu wapate huduma hizo.

Mhe. Naibu Spika, namalizia kwa ufupi kabisa kwasababu muda umekwenda. Msitu wa Kiwengwa nyumbani. Mhe. Naibu Spika, kwa imani yako naomba uniruhusu dakika mbili tu sijapata maswali ya nyongeza toka juzi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, msitu wa Kiwengwa mimi ndiko nilikozaliwa bahati nzuri, msitu huu kwa nje utauona mzuri lakini namuomba Mhe. Waziri pamoja na askari aliokuwa nao aongeze kumi na nne hawatoshi, msitu umekwisha watu wanaingia usiku wanakata kuni wanapeleka Nungwi, Pwani Mchangani sikosei ndio hali ilivyo Potoa wapi kwa siri na wanatumia baiskeli. Kwahivyo, namuomba Mhe. Waziri hili likaangaliwa ili kunusuru msitu ule. Msitu kwa nje mzuri lakini ukienda katikati umekwisha kwa hiyo Mheshimiwa kwakuwa muda hakuna na bahati nzuri muda mdogo tuna mambo mengi.

Mhe. Naibu Spika, nasema kwamba ripoti hii naipokea nampongeza Mwenyekiti na wenzake wote lakini niseme kwa ufupi tu kwamba mimi naikubali kwa asilima mia moja na wenzangu naomba wachangie ili tuwape nguvu wizara zetu hizi wafanye kazi zao vizuri. Ahsante Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Ali Suleiman Ali. Mchangiaji wetu wa pili atakuwa Mhe. Suleiman Makame Ali baada ya hapo ajitayarishe Mhe. Bahati Khamis Kombo na muda ukibakia nitataja wengine.

Mhe.Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi hii na kuweza kuchangia ripoti hii iliyo mbele yetu.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nipeleke pongezi zangu kwa Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango hususan kwenye ukusanyaji wa mapato. Mhe. Naibu Spika, kwenye zile sifa tatu ambazo anatakiwa awe nazo mwanadamu Mhe. Waziri wa Fedha anazo sifa hizo ya kwanza uaminifu, ya pili utekelezaji lakini ya tatu hana hiyana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, suala hili la kusema kwamba hana hiyana yaani ni mkweli, amefika asilimia sitini na tatu kwenye ukusanyaji wa mapato kuanzia mwezi wa Julai hadi Disemba nimpongeze sana sana na nimuombee azidi kufanya kazi, namshauri hivyo na *inshaallah* Mwenyezi Mungu atampa nguvu zaidi nasi tupo bega kwa bega nae pamoja na wafanyakazi wa wizara yake. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo niende ukurasa wa kumi na tatu kwenye utekelezaji wa bajeti Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko, nayo wizara hii naipongeza sana hususan Katibu Mkuu pamoja na Mhe. Waziri kwenye ukusanyaji wa mapato na katika ukusanyaji wa mapato alisema kwamba walikadiriwa kukusanya kiwango cha pesa hizo hapo shilingi milioni 236 laki 217069 lakini wamefikia wamefikia asilimia mia mbili na sitini na tatu ni asilimia nzuri ambayo inaonesha moyo. Lakini vingine huenda ikawa zaidi kwa sababu wanachokadiriwa kukusanya ikawa ni kidogo kutokana na kiwango walichokikusanya.

Mhe. Naibu Spika, mimi nina imani fedha zipo ila usimamizi, kwa hiyo niwaombe Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko na wizara nyengine waendelee kukusanya mapato, ili kufikia asilimia hizo zinazokusidiwa.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo nielekee kwenye ukurasa wa kumi na tano kwenye fidia ya wahanga wa mikarafuu, kwenye suala hili la fidia nimesikitika kidogo kwasababu hatukuona ile idadi ya zile pesa ambazo alisema Mhe. Mwenyekiti wa Kamati kwamba inatarajiwa kutoa pesa hizo lakini cha kushangaza kwenye masuala haya ya fidia na kwenye masuala yale ya mapato ambayo pesa zilizotakiwa kukusanywa, pesa zilizotarajiwa kukusanywa walizosema kwamba wamekodisha mikarafuu shilingi bilioni mbili na iliyopatikana ni bilioni moja. Hapa kusema kweli ni mtihani kwasababu pesa ambazo mikarafuu

zimetakiwa kukodishwa na imekodishwa karafuu kwenye mikarafuu hazimo tena zishachumwa pesa hazipo.

Mhe. Naibu Spika, ni mtihani na ni jambo la kusikitisha sana, sasa Mhe. Naibu Spika mimi niwaombe sana serikali kwamba wale ambao wamekodishwa mikarafuu hii na karafuu wamezichuma warejeshe pesa hizi haraka hizi ni pesa za taifa si pesa zao za kutioa mifukoni. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, hawa watu ilikuwa wachunguzwe kabla ya kukopeshwa. Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa mfano au hadithi ndogo siku moja kulikuwa na mwalimu akisomesha darasani, akaandika hesabu akawambia wanafunzi baba yako anakopa shilingi elfu mbili elfu moja kakopa benki elfu moja kakopa kwa jirani baba yako anatakiwa alipe shilingi ngapi? Mwanafunzi mmoja akajibu baba yangu halipi, mwalimu akamuuliza kwa nini ukasema hivyo hujui hesabu wewe, akamwambia mimi najua kwasababu baba yangu akikopeshwa halipi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, hili ndio hilo kwamba kuna watu wanajulikana hawalipi halafu wakenda wakakopeshwa mikarafuu. Kumbe ni bora wangepewa wale wale waliokuwa wakiendelea kuitunza na kuienzi ile mikarafuu pesa zingerudi kulikoni kupewa watu waliokuwa hawana muelekeo hawana azma ya kulipa pesa hizi. Naiomba sana serikali kuwachukulia hatua watu wote hawa ambao wamekodi mikarafuu, karafuu wameshazichuma pesa hawakurejesha serikalini.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo niende moja kwa moja kwenye suala la madagaa, juzi Mhe. Hamza Hassan Juma amesema hapa alikuwa anazungumza Mhe. Makame kwamba kamati haikuwatembelea wavuvi imewatembelea waanikaji wa dagaa, hii ni Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi lakini wavuvi wamesahaulika, hakuna kazi ngumu kama uvuvi, uvuvi wa

madagaa unafanyika usiku hadi usiku wavuvi hawalali na kipato chenyewe hakipo. Sasa juzi Mhe. Hamza Hassan Juma alisema hapa kwamba dagaa sasa hivi imekuwa hadi balaa kule wateja wale wa Congo wanafika mpaka kukata tamaa kwamba hawaji tena hapa kuja kuchukua lile dagaa ukiangalia kipato chenyewe hakipo.

Kutokana na hali hiyo, Mhe. Naibu Spika, namuomba sana Mhe. Waziri wa Biashara, Mhe.Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na Mhe.Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kuhakikisha kwamba dagaa linatoka vilevile kama ilivyokuwa mwanzo kwasababu hakuna faida ya hivyo na serikali kila siku zinapiga kelele watu kujiajiri wenyewe na watu wanajiajiri, leo mvuvi wa dagaa anakwenda baharini kuvua dagaa akirudi ana shilingi elfu moja ana watoto ishirini ndani ya nyumba wanamtegemea.

Mhe. Naibu Spika, naiomba sana serikali kuliangalia hili kuka pamoja na Serikali ya Jamhuri ya Muungano, kuhakikisha kwamba wale wanaokuja kuchukua dagaa hapa, basi wapewe nafuu, ili kuhakikisha kwamba wale wavuvi wale kufanya kazi ile bila ya vikwazo vyovyote, kwasababu Mkongo ikiwa kama hakuja kununua dagaa hapa hiyo biashara haipo.

Leo ukitizama Zanzibar nithubutu kama kusema asilimia 40 ni wavuvi vijana wamejipeleka katika bahari kutafuta vijio, lakini leo dagaa halitoki halina tena bei hicho wanachopata kwanza hakipo kwanza hakipo vilevile itakuwa wateja hawaji itakuwaje watakufa na njaa Mhe. Naibu Spika, kwahivyo naomba sana suala hili la wavuvi liangaliwe. Mhe. Naibu Spika, pia naiomba kamati kwamba mara nyengine itakavyokwenda kamati wawafikie wavuvi wasiwafikie waanikaji wa madagaa, wawafikie wavuvi kama ni wavuvi wa pweza, samaki wote wawafikie, ili kusikiliza changamoto zao wavuvi wamesahauliwa katika jimbo langu mimi

asilimia 60 ni wavuvi Wesha, Ndagoni, Michungwani, Pale na kwa Mhe. Makame Kojani pia, lakini sasa wavuvi wamesahauliwa kabisa. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo niende kwenye suala la mashamba ya mikarafuu, Mhe. Mwenyekiti alisema kwamba kuna pesa ambazo kwamba wanataka kupewa wale vifuta jasho ambao wanashughulikia yale mashamba. Mhe. Naibu Spika, naomba kusema kwamba kidogo Mhe. Rais hakuambiwa ukweli baadhi ya mashamba mengine ukifanya tathmini kusema la ukweli hakuna mpka hii leo baadhi ya wengine hawajalipwa ile pesa. Kwahivyo, naiomba serikali kufanya kila iwezekanavyo wale waliokuwa wanashughulikia mashamba yale kwanza warejeshewe yale mashamba kwa taratibu nzuri, kwasababu serikali ilikuwa lengo lake ni kuyatambua na tayari washayatambua, bila ya wao waliokuwa wakishughulikia mashamba yale ingelikuwa yana mkekewa kama utakuwa hujui mkekewa na nyambo nyambo au kifa uongo, ingelikuwa basi yale si mashamba ingekuwa ni mwitu, lakini wao walikuwa wakiyaenzi na kuyatunza.

Kutokana na hali hiyo, naiomba serikali na kwa imani yangu Mhe. Rais tuliyenaye msikivu, muadilifu, kwasababu lengo ilikuwa ni kuyatambua naomba sana kwamba mashamba yale werejeshewe, ili waendelee kuyaenzi na kuyatunza. Ahsante sana Mhe. Spika, naunga mkono asilimia mia ripoti hii. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Bahati Khamis Kombo, atafuata Mhe. Ali Khamis Bakari.

Mhe. Bahati Khamis Kombo, ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunpa nafasi ya kuweza kuchangia Ripoti ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo. Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa nitangulize kwa kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wetu wote watatu, Makatibu pamoja na watendaji wao wote kwa kazi

ambazo wanafanya kwa mashirikiano ya pamoja. Lakini pia pongezi za pekee ziende kwa kamati yetu ambayo imefanya kazi kubwa na leo hii wameweza kutuletea changamoto mbalimbali ambao zimo katika wizara hizi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, naomba niende moja kwa moja katika ukurasa wa saba kwenye changamoto namba nne, changamoto hii ya kuweko kwa mashirikiano yasiyoridhisha baina ya Tume ya Mipango Zanzibar na Tume ya Mipango ya Tanzania Bara, hususan katika uwasilishaji wa mapendekeo ya maandiko ya miradi ya maendeleo ya wahisani, changamoto hii tunaiona ni ndogo lakini changamoto hii ni kubwa sio ndogo kama tunavyoiona. Kwahivyo, kwa mchango wangu naiomba tu serikali kwamba wakae pamoja Tume ya Mipango ya Zanzibar na Tume ya Mipango ya Tanzania Bara, ili kuweza kuiondosha changamoto hiyo.

Mhe. Naibu Spika, niende moja kwa moja katika ukurasa wa tisa Benki ya Watu wa Zanzibar lakini katika Tawi la Mkoani, ipo changamoto ambayo changamoto hii kama sisi wanawake na sisi hatuioni kama ni jambo jema kwamba katika kituo kile cha Benki pale Zanzibar kutokuwepo kwa mfanyakazi mwanamke, tunaomba sana suala hili lizingatiwe kama walivyoiona changamoto hii wenzetu wa Kamati na wakatoa maoni yao basi tunaomba maoni haya yathaminiwe, ili aweze kupatikana mfanyakazi mwanamke katika benki hii. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, niende moja kwa moja katika ukurasa wa kumi benki ya *CRDB* mimi nataka nimpongeze sana meneja wa *CRDB* katika tawi lilioko Chake Chake Pemba, meneja yule anawashajihisha wakulima, wafanyabiashara mbalimbali, ili kuweza kulitumia tawi lile liliopo Chake Chake. Lakini tumeona kuwa wajasiriamali wengi hususan Wilaya ya Mkoani bado hawajakuwa na ile taaluma ya kuona kuwa walitumie tawi lile la

CRDB, ili waweze kujikwamua kiuchumi,pamoja na wajasiriamali hawa waweze kukuza kile kipato chao na waweze kuajiri wajasiriamali wengine ili watu wajikwamue kiuchumi, tusitegemee watu kupata kazi katika serikali, serikali inaajiri lakini si kweli kama itaweza kuajiri wananchi wote. Kwahivyo, nawaomba wananchi wote wa Wilaya ya Mkoani tushirikiane kwa pamoja ili tuone kwamba wanaitumia benki hii ya *CRDB*, ili waweze kujikwamua kiuchumi.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo niende moja kwa moja katika utekelezaji wa bajeti, na mimi nichukue fursa hii ya kuwapongeza sana Waheshimiwa Mawaziri wetu jinsi walivyoweza kukusanya mapato haya na mpaka hii leo kuona kwamba tayari wameshafikia asilimia 263.

Nikitoka hapo Mhe. Naibu Spika, niende moja kwa moja katika ukurasa wa 15 kamati hapa imetoa maagizo yake, kamati inashauri Wizara kuchukua hatua kali za kisheria dhidi ya wafanya biashara wote wanaobainika wanauza bidhaa zilizopitwa na wakati. Mhe. Naibu Spika, hili ni jambo jema naipongeza kamati hii kwasababu hivi karibuni tumewaona watoto kwamba wamekwenda kununua biskuti lakini ukizikata ndani yake zinatoka mafunzo, kwakweli kama sikuwepo watu wazima wakawanyang'anya biskuti ile, basi watoto wale wangeweza kuathirika kwa kiasi fulani.

Mhe. Naibu Spika, niende moja kwa moja katika changamoto ya udhibiti mdogo wa watoto chini ya miaka kumi na nane kujihusisha na uchumaji wa zao la karafuu, suala hili kwa kweli ni suala gumu na sipingani na amri iliyotolewa kwamba watoto chini ya miaka kumi na nane ndio waweze kuchuma karafuu. Lakini Mhe. Naibu Spika, kuna watu ambao wako katika visiwa watu hawa mara nyingi inakuwa hata ile elimu wanakuwa wao hawanayo, na hata ukimuelimisha basi hawezi kuelimika yeye ni

pwani na pani na yeye na ukisikia wakati wa karafuu wanahama katika kisiwa kile wanakuja Mabopwe kwa ajili ya uchumaji wa karafuu, na wakifika pale wanakuja na watoto wao.

Mhe. Naibu Spika, watoto hawa mzee anajitahidi kuwadhibiti lakini yeye mzee akipanda mkarafuu mtoto yule tayari yeye ameshakwenda kupanda mkarafuu mwengine, kwa hivvyo naiomba Seirkali tuangalie jinsi gani ya kuweza kuwadhibiti vijana hawa, lakinivile vile tuangalie kuanzia umri wa miaka kumi na tano mpaka kufikia umri wa miaka kumi na nane ili waweze kuruhusiwa kuchuma hizi karafuu kwa sababu tunawajua watoto wetu wa chini kabisa walivyo na wale kiasi gani walivyo. Kwahivyo, suala hili Mhe. Mwenyekiti sipingani lakini naiomba sana serikali iangalie sana juu ya tatizo hili kwasababu watoto wetu tunawaona kwamba wanakwenda skuli, lakini badala yake huko skuli wanakokwenda wanatoroka wanakwenda katika uchumaji wa karafuu.

Mwaka huu uliopita watoto wetu wengi walipigwa na vikosi vyetu vya ulinzi kuona kwamba watoto hawa tunataka kuwapeleka skuli waende wakasome, lakini pia ilishindikana na asilimia kubwa ni ndani ya Jimbo langu la Chambani tulipata athari kubwa na watoto ndio maana katika Shehiya yetu ya Chambani kuonekana kwamba hawakupasi vizuri.

Mhe. Naibu Spika, ningeomba sana utakapofika uchumaji wa karafuu pasi ni vyema hizi skuli ikafungwa kama zilivyokuwa zikifungwa zamani, ili hawa wazee wakawa karibu na watoto wao kwasababu mtoto utakapokuwa nae karibu hata kama umekwenda kuchuma karafuu yeye yuko chini lakini utaona kwamba huyu mtoto yupo, lakini bila ya hivyo Mhe. Naibu Spika, ni lazima hapa bado tutaendelea kuwa na tatizo kuhusiana na watoto hawa ambao hawajafiki umri wa miaka 18. Naiomba serikali iliangalie

tena kwa kina suala hili ili tuweze kupata ufumbuzi na malezi bora ya watoto wetu.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea mbele niende moja kwa moja katika ukurasa wa 22 maoni na maagizo ya kamati, kamati hapa ilitembelea katika kituo cha ushoni cha Idara Maalum ya SMZ lakini pia ikakuta changamoto ambayo imetolewa maagizo na kamati kwamba inataka Wizara kufanya juhudi zaidi ili kuhakikisha jeshi la Polisi linalipa deni la shilingi milioni kumi na moja kwa kiwanda hicho. Na mimi naunga mkono kuona kwamba fedha hizo zimerejeshwa kwa muda mfupi sana kwasababu tunapokopa lazima tunawekeana kiwango muda fulani fedha zile ziweze kufika, lakini mpaka leo fedha hizi bado zinadaiwa. Mhe. Naibu Spika, naomba sana Mhe. Waziri hili achukue juhudi za makusudi kuona kwamba fedha hizi zimerudi katika kiwanda hichi.

Mhe. Naibu Spika, nikimalizia ukodishaji wa mashamba kwa kweli ukodishaji huu hasa kule Pemba baadhi ya wananchi wengine kwa kweli walifanyiwa mambo yaliyokuwa sio mazuri, lakini nadhani ilipokwenda ilionana na wahusika tu wa Wizara lakini haikushuka chini kwa wananchi. Mhe. Naibu Spika, niiombe kamati itakapokwenda tena Pemba ionane na wakulima wa karafuu, kuna baadhi ya mikarafuu kama waziri hatambui basi namwambia rasmi kama Mhe. Waziri mikarafuu mingine bado imefichwa hajapewa na mikarafuu hii ambayo imefichwa ni wafanyakazi wake wa Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi wanaitumia kwa wanavyojua wao wenyewe (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri ningeomba tena sana uangalie kwa kina kuona kwamba hii mikarafuu imekuja serikalini na wamepewa wale ambao wana haki ya kupewa, kuna mikarafuu ambayo wananchi ni mikarafuu ya urithi wa wazazi wao. Lakini kilichofanyika katika ukodishaji ule wa mikarafuu

inaachwa shamba ya eka inachukuliwa shamba ya mtu ambaye karithi kwa wazazi wake anakodishwa mtu, mtu akilalamika anarejeshewa lakini hii ya eka haitajwi tena imeshaachwa, wafanyakazi wake wa kilimo wanaitumia wao wenyewe kwa wanavyojua wao, tuna changamoto kubwa sana Pemba juu ya ukodishwaji wa mikarafuu. Kuna mikarafuu ambayo imekodishwa Shilingi milioni moja na laki tisa, lakini yule anayeshughulikia ile mikarafuu kapewa shilingi laki tano na hizo laki tano sio kwamba ameshapewa mkononi lakini kaandikiwa tu kupewa laki tano.

Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri aangalie tena jinsi yule mtu ambae anahudumia ile mikarafuu kwa ufanisi mzuri ili aangaliwe na kile kima cha kupewa cha kukidhi, kwasababu kama tunavyojua zao la karafuu linazaa mwaka mmoja pengine mwaka wa pili halizai, lakini mwananchi yule analihudimia mwaka mpaka mwaka kuona kwamba mikarafuu ile iko katika hali nzuri ndio maana tukaweza kupata fedha hizi leo, kama ingelikuwa haikuhudumikiwa mikarafuu ile basi serikali isingeliweza kutimiza fedha hizo ambazo zimepatikana mwaka huu uliopita. Mimi naomba kile kima cha shilingi laki tano tunawaonea wananchi suala hili liangaliwe tena kuona kwamba mwananchi na yeye kafaidika na kile kipato ambacho kimepatikana katika mikrafuu ile.

Mhe. Mwenyekiti baada ya kusema hayo ahsante sana nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii na naunga mkono kamati.

Mhe. Naibu Spika: ahsante sana Mhe. Bahati mchangiaji wetu anayefuata ni Mhe. Ali Khamis Bakari na muda kama utatosha atachangia Mhe. Hassan Hamis Khafidh (Diaspora).

Mhe. Ali Khamis Bakari: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nami kwa kunipa nafasi kuweza kuchangia ripoti hii kwa siku ya leo

iliyopo kwenye meza yetu ya Kamati ya Biashara, fedha, kilimo ya Baraza la Wawakilishi, kwanza niipongeze Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kazi kubwa inayoifanya juu ya kuboresha katika Wizara zake zote, lakini vile vile kwa kuweza kuwajali wananchi wetu waliomo ndani ya Serikali hii.

Mhe. Naibu Spika, vilevile niipongeze kamati kwa kazi kubwa waliyoifanya, lakini niipongeze wizara kwa kutoa ushirikiano, ili kuweza kukiandaa kitabu hichi na ripoti hii ikawa leo tunaijadili.

Mhe. Naibu Spika, nianze kwa ukaguzi wa vipimo ukurasa namba 20 Kitengo cha Vipimo cha Mizani kinafanyakazi kwa mujibu wa sheria namba nne vipimo vya mwaka 1983 ikiwa ni moja uhakiki wa vipimo vyote vinavyohusiana na biashara hapa Zanzibar ikiwemo mizani za vipimo, bidhaa kutoka kwa wauzaji kwenda kwa wanunuzi. Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba sheria hii ipo kwa mujibu wa Sheria ya mwaka 1983, lakini tumeona kwamba kuna baadhi ya sehemu karibuni zote za Unguja na Pemba wananchi wote wanafanya biashara na ni jambo zuri, ili kuweza kupata kipato na kuweza kusaidia familia, lakini tumeona kwamba biashara hizi baadhi yao wanaofanya kusema kweli si waaminifu na tukiangalia siku zote kwamba mfanyabiashara mungu wake basi huwa ni pesa anaweza kula kiapo au akafanya mambo anayoyajua yeye pale Mwenyezi Mungu huwa anamuweka pembeni yeye anajali zaidi pesa.

Mhe. Naibu Spika, kwa mfano katika sehemu zetu za vijijini, namuomba Mhe. Waziri anisikilize kwa makini, ili aweze kutambua baadhi ya changamoto ambazo zipo, kwenye vijiji vyetu sasa hivi kuna wafanyabiashara ambao wanauza biashara kwa mfano mambo ya duka mizani zao ambazo zinafanya biashara zile zimefungwa vibwebwe zimefungwa kamba, mtu pengine hana ile mizani hana jiwe la kilo ambalo ile kilo haitimii, pengine ana kijiwe pembeni.

Vilevile, ukiangalia nataka hata kwenye sheli za mafuta kule Pemba sitaki kusema ni sheli gani, lakini kuna watu wanakwambia hasa ukitaka upate mafuta mengi yale ya taa ukienda kununua, basi watu wanayaangalia sheli fulani inatimiza mafuta yake, lakini sheli fulani anakwambia hee mafuta haya na hilo hilo kwenye maduka kuna vipimo vile wanavyopimia watu vya amani bado vyengine havitimizi, hivyo mizani bado kwenye upimaji wao wa yale mawe au ratili zinakuwa hazitimii.

Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri aandae mpango wa kupita katika vijiji kama ni mwezi au mwaka kuhakikisha kwamba wafanyabiashara hawa wanawatembelea na wanaangalia mizani uzima wao pia katika mawe ambayo wanayatumia katika upimaji wa vyakula au kuwafanyia huduma wananchi, tumeona hii ni kadhia kubwa lakini wafanyabiashara wapo tu hawajali kubwa wao wanajali maslahi yao na wanawapunguzia vipimo wale ambao wanakwenda kununua.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo niende kwa Shirika la Taifa la Biashara (*ZSTC)* niungane na Mhe. Bahati Khamis Kombo kwamba shirika hili lipo kwa mujibu wa sheria na tumeona kwamba linafanya kazi kubwa kuweza kutoa huduma. Kwakweli, serikali yetu imejitahidi katika kuhakikisha kwamba wakulima hawa wanaboreshwa na wanapewa misaada na mikopo kuweza kuliokoa zao hili na mambo mengine. Hivyo, naipongeze kamati imesema kwamba kamati inaipongeza Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kupitia (*ZSTC)* kwa kuwafariji wananchi ambao walipata ajali mbalimbali kutokana na harakati za kuliokoa zao la karafuu, miongoni mwa
faraja hizo ni kuwapatia vifutia jasho ambavyo vinasaidia kwa kiasi kikubwa matibabu ya wahanga hao.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli, lakini katika changamoto kumeandikwa hapa kwamba udhibiti mdogo wa watoto chini ya miaka 18 kujihusisha na uchumaji wa zao la karafuu na kupata athari mbalimbali.

Mhe. Naibu Spika, changamoto hii napingana nayo. Sote hapa ni *mas-ula* kinapofika kipindi cha uchumaji wa karafuu tunahamasishana, serikali inawatangazia wananchi, redio zinapiga kelele mpaka maonesho ya michezo ya kuigiza akiwemo Mwinyimpeku, Kachara wanatoa mifano ya kuchuma karafuu, ili tunahamasishwa twende tukaliokowe zao la karafuu na wanaoliokoa zao hili ni vijana kuanzia umri wa miaka 18 kushuka chini, mtu mzima hawezi tena. Zao la karafuu tunaona kwamba uzaliwaji wake wa karafuu zinakuwa ni kileleni, vyengine vitawi vya ncha uweze kuvivuta ili kupata karafuu zile.

Mhe. Naibu Spika, niseme kwamba ni kweli kuna watoto wanaojihusisha na mambo haya, lakini wanakwenda kupata riziki, leo tukisema kwamba watoto hawa wasiende kidogo tutakuwa hatuwatendei haki. Kutokana na hali hiyo, naiomba wizara iandae utaratibu kama ambavyo kwa upande wa serikali kumewekwa masheha na baadhi ya watu, ili kuhakikisha kwamba pale panapotokezea tatizo wafanye pengine ndani ya wiki sheha aseme katika shehia yake ni watu wangapi labda wameathirika kutokana na uchumaji wa karafuu, ili iweze kujulikana kama kuna watoto au kuna watu waliopata kuathirika na suala hili, lakini isiseme kwamba watoto hawa wasiende kuchuma karafuu.

Mhe. Naibu Spika, katika vijiji vyetu ukisema umri wa miaka 18, hawa ni watu wazima wameshazaa watoto hawa, kwa hivyo ukisema kwamba wasiende kuchuma karafuu je, mtu keshakuwa mtu mzima anataka watoto wake wapate pesa na wapate riziki wavae, wewe unasema kuanzia miaka 18. Ni vyema watu hawa

wakaachiwa, wakaenda kuchuma karafuu, lakini kuwe na utaratibu mzuri wa kuweza kuwalinda pale. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, watu wote wanaokwenda pale sio kama tunawapeleka kwasababu ya kuwa waende wakaanguke, lile ni suala jengine, ni bahati mbaya tu imemtokezea mtu Mwenyezi Mungu kaandika katika kuliokoa zao la karafuu ameanguka, lakini hategemei kwamba nikifika pale mimi nakwenda kupata hii athari. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, vilevile ukosefu wa elimu juu taratibu za kufuatwa hadi wananchi kupatiwa kifutia jasho fidia, baada ya kuanguka katika mikarafuu nalo ni tatizo kwani baadhi ya waathirika hubakia wakisononeka tu bila ya kupata msaada wowote.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli wamo watu ambao baada ya kwishaanguka hawana elimu na hawajui wapi pakukimbilia kuweza kupata hiki kifutia jasho. Hili nakubaliana nalo, lakini vile vile kuandaliwe utaratibu kama huu ambao nimeuzungumza mwanzo. Sheha pale yupo katika shehia yake watu anawajua, fulani na fulani wamepata athari, kwa hivyo akaripoti yeye jamani mimi katika shehia yangu watu watatu wameathrika kwa suala hili, taarifa hii ipelekwe kunakohusika kama ni wizara au kama ni hawa *ZSTC*. Kwasababu tumeona ikifika kipindi hiki *ZSTC* yenyewe inaweka ma-*gate* karibuni barabara nzima, kila utakapokwenda pana *gate*.

Sasa kwa nini wanashindwa kutoa elimu juu ya hawa watu walioanguka. Je, wale ambao wanafanya magendo kwa nini wakaweka ma-*gate*. Tumeona kwamba kuna ma-*gate* ambayo yamewekwa kwa ajili ya kudhibiti. Lakini kwa nini wanashindwa kuwapa elimu wale ambao wameathirika. Naomba uandaliwe utaratibu kama ni wa shehia au wa wilaya, ili kuweza

kutambulikana watu hawa na wao waweze kupata elimu kwamba mtu aliyepata kuanguka katika suala hili basi aweze kupata kifutia jasho.

Mhe. Naibu Spika, niende katika ukurasa wa 6 Nyumba ya Treni. Kwanza nimpongeze Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi Mhe. Ayoub Mohamed Mahmoud kwa kazi kubwa anayoifanya, tumeshuhudia pamoja na kero nyingi ambazo zilikuwepo pale juu ya uwekaji mzuri wa lile jengo, bado hali inaendelea vizuri. Mimi jana nimepita nikaona kwamba mambo yanakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, niwapongeze zaidi kamati kwa kuibua changamoto nyingi ambazo wamezitaja katika kitabu hiki. Vilevile niungane na Mhe. Suleiman Makame kwa wale wavuvi ambao wanafanya uvuvi wao katika Bahari Kuu. Tumeona kwamba hapa wametajwa zaidi wale waanikaji dagaa, lakini hawa wavuvi wameachwa na wavuvi ndio ambao wanaokwenda kuuza roho.

Kwahivyo, ni lazima na hawa waangaliwe na watengewe fungu au kama kuna elimu ya kupewa, basi kuwepo na utaratibu maalum ambao kama ni wiki au mwezi kuweza kuitwa na kuweza kupewa taratibu maalum juu ya masuala mazima ya ushughulikiaji wa dagaa. Hali halisi tunaiona, watu wanapokwenda katika uvuvi wakirudi biashara zao wanakuwa kidogo watu wanaokuja kununua dagaa lile linakuwa haliko katika hali ambayo ni nzuri, biashara inakuwa ndogo kuliko kipato.

Mhe. Naibu Spika, niunge mkono hoja hii na nikushukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Mjumbe, sasa nimpe nafasi Mhe. Hassan Khamis Hafidh, natarajia utamaliza muda huu.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kuchangia dakika tano zilizobakia. Mhe. Naibu Spika, kwakweli sina mengi lakini nataka kuipongeza serikali kwa juhudi kubwa wanayoifanya katika kuwaletea maendeleo wananchi wa Zanzibar, wakwezi na wakulima na wanamapinduzi wa nchi hii. *(Makofi)*

Pili, nataka kuchukua fursa hii ya kumpongeza Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa kufanya kazi nzuri yeye pamoja na watendaji wake katika kukusanya fedha, ambapo fedha hizo tunazitumia katika kuwaletea maendeleo wananchi wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, baada ya kumpongeza Waziri wa Fedha na Mipango, niwapongeze na watendaji wa zile taasisi ambazo zinakusanya mapato, kaka yangu Mcha wa *TRA*, kaka yangu Amour Mohamed Bakar wa *ZRB*, kwakweli wanafanya kazi nzuri za kukusanya mapato katika kuwaletea maendeleo wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuchukua fursa hii *just* kumkumbusha tu Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango katika bajeti kuna kitu tunaita *income and expenditure*, mapato na matumizi. Sasa ningemuomba Mhe. Waziri anafanya vizuri sana katika kukusanya mapato, lakini ningemuomba nako afanye vizuri katika kutumia, Zanzibar au nchi nyengine zote za dunia kuna kitu kinaitwa miradi. Sasa kunako hii miradi katika hasa nchi za Kiafrika, nchi zinazoendelea ndipo watu wengi kwa lugha ya leo wanapopiga yaani wanapopata pesa. Kutokana na hali hiyo, naomba Mhe. Naibu Spika, iwekwe kamati maalumu ya kufanya

uratibu wa kuhakikisha kile ambacho kinatumiwa au mradi wowote unaokuja katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ufanyiwe *analysis* ya kutosha, ili ile *value for money* ipatikane.

Mhe. Naibu Spika, serikali ina lengo zuri pamoja na azma nzuri, lakini bado naamini kuna baadhi ya watu wachache watakuwa hawana lengo zuri dhizi ya maendeleo ya nchi yetu, hao ndio kikwazo cha maendeleo ya nchi yetu. Kwahiyo, namuomba sana katika miradi Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango ambaye anahusika na matumizi miradi mingi Zanzibar na nchi nyengine kwa jumla kuwa ile *value for money* haipatikani. Nitatoa mfano.

Mhe. Naibu Spika, juzi Mhe. Waziri wa Elimu wa Bara, Mhe. Joice Ndalichako alitembelea mradi mmoja katika mkoa mmoja ambao ulitumia karibu shilingi milioni mia mbili, anauliza hizo shilingi milioni mia mbili ndio zimetumika kwa hapa? Mbao hizi mbovu? Ile *value for money* akasema ilikuwa haipo akaunda tume hapo hapo, akasema naleta tume ya kuchunguza mapato haya. Mhe. Naibu Spika, naomba Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, anafanya kazi nzuri, aendelee kuhakikisha matumizi hasa katika miradi ya serikali lazima awe na Kamati au Tume Maalum kabla ya mradi haujaanza kufanya kazi Zanzibar uwe umefanyiwa kazi vizuri, ili kuhakikisha mradi ule *value for money* inapatikana.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo nakwenda katika Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi. Naye nimpongeze mzee wangu, mzoefu anafanya kazi nzuri sana, leo si jana. Lakini nimkumbushe tu ahadi yake aliloliambia Baraza hili tukufu la Tisa kwamba atajitahidi kadiri ya uwezo wake kabla hajatoka katika Baraza hili ataweza kuwaletea Wazanzibari mchele japo asilimia 50. Namuomba hiyo kazi aendelee kuifanya kwasababu muda aliouweka tayari unakaribia na sijui kama tayari ameweza kuupata mchele angalau asilimia 50. *(Makofi)*

Pia nimpongeze Mhe. Waziri wa Kilimo kwamba, kwa kuanzisha Mhe. Rais nimpongeze kampuni ya *ZAFICO* ya kuweza kuvua kupitia Bahari Kuu. Hiyo ni hongera, kazi nzuri kwa sababu Zanzibar tumezungukwa na bahari lakini bado bahari wavuvi wetu wanapokwenda baharini kule jamaa zangu hawana uhakika wa kupata, wanakwenda kwa kubahatisha, wanakwenda kwa Mungu nisaidie, wanakwenda kwa *Yallahtif, Yallahtif*. Naomba sana Mhe. Naibu Spika, hii kampuni sasa ianze kufanya kazi, ili Wazanzibari wavuvi waweze kufaidika wakwezi na wakulima waweze kufaidika na bahari yao aliyowaletea Mwenyezi Mungu iliyozungukza nchi nzima. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kulitolewa *statistic* nimeisahau kidogo, ukiangalia mapato yanayopatikana kutoka Bahari Kuu yanatosha kuendesha Zanzibar, ambapo mapato au hawa samaki wengi wanavuliwa na wageni Wajapani na nchi nyengine. Namuomba sana Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi ahakikishe Bahari Kuu sasa amekuja na meli kupitia Shirika lake la *ZAFICO* za uvuvi wa kile ili nchi yetu sasa iweze kuvua kupitia Bahari Kuu. Nampongeza sana kwa kuanzisha shirika hili. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nimkumbushe Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi juzi au jana nilikuwa nachangia kuhusu embe nikasema na leo naomba nirudie, embe shomari ni embe bora kuliko embe zote duniani. Mhe. Waziri alipopanda juu ya jukwaa akasema si kweli. Sasa leo nataka nimpe *prove* kumwambia kwamba embe shomari ni embe zote duniani ambazo embe hizi zinapatikana shamba ya Mchangani hasa pale mwisho wa njia nyumbani.

Mhe. Naibu Spika, hivyo nataka kusema wazi mwaka 2009 wakati niko *diaspora* nilizichukua embe shomari nikazipeleka katika Umoja wa Wakulima wa Uingereza, *Fruit and Vegetable Association* wakazipima embe hizi wakazikuta ni embe bora

zinaongoza, kosa lake zina wadudu haziwezi kuuzika nje. Lakini pia mwezi mmoja uliopita alikuja *Lulu Supermarket* ambayo *supermarket* hii ndiyo inayouza *fruit and vegetable* katika nchi zote za UAE, walizichukua embe shomari wakenda wakazipima, wakakuta ndio embe bora lakini bado embe hizi zina wadudu.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri juzi alipochangia akasema hazijui, kumbe alichanganisha baina ya embe shomari na embe hemeri. Embe hemeri kwa Kiswahili kule kwetu Mchangani tunaziita embe punda ndizo zinazotumika kwa embe za mchuzi. Embe shomari bado ni embe bora zinazojulikana duniani na akasema embe bora ni embe siagi. Nataka nimwambie leo embe bora duniani iliyopasi inaitwa *jury mango* na inapatikana Pakistan, hii ilipitwa na embe shomari katika mashindano ya mwaka 2009 pale Uingereza, *jury mango*.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri alisema kwamba embe shomari ni embe wanazotumia watoto wadogo kuzinyonya kwa sababu zimejaa mizizi. Ningemuomba awaombe radhi watu wa Mchangani wanaofanya jitihada nzuri, wanalima embe nzuri ambazo zinaongoza dunia ambazo ni embe shomari. Ningemuomba ahakikishe embe shomari hazina wadudu ili ziweze kuuzika nje jamaa zangu wa Mchangani waweze kufaidika na embe zao wanazouza kule Mchangani lakini bado embe hizi zimejaa wadudu haziwezi kuuzika nje. Namuomba sana ajitahidi awatoe wadudu hao kwa utaalamu ili embe hizi ziweze kuuzika nje.

Mhe. Naibu Spika, mwisho namalizia nakuja Wizara ya Biashara na Viwanda na Masoko, niwapongeze sana wanafanya kazi nzuri. Lakini nataka niwakumbushe Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko mfanyabiashara nilisema katika Baraza hili tukufu hana dini, dini yake ni faida kitabu chake ni ghilba. Kwahivyo, kama mfanyabiashara hana dini, dini yake ni faida kitabu chake ni

ghilba nataka nimwambie tumekuwa tume-*experience in this country that*, wafanyabiashara wengi wanaongeza bei kwasababu *there is no monitoring system* ya bei haupo mfumo maalumu kwa utaratibu wa kuangalia bei. Wafanyabiashara wanaongeza bei na wengi wao tunawajua *same time* wanataka kuhakikisha kwamba tunakenda chini.

Mhe. Naibu Spika, namuomba sana Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko ahakikishe bei hizi zinakuwa *monitored* kinajulikana kitu hichi ile *contry of origin* kimetoka wapi, kimekuja hapa kiasi gani, ili wananchi wetu wapate kufaidika wasikomolewe. Wafanyabiashara wa Zanzibar wengi wao wanawakomoa wananchi wa Zanzibar kwasababu hawajui bidhaa hii inatoka wapi, wanaongeza bei kiholela. Namuomba sana Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, juzi tumepitisha Sheria ya Bei hapa tunaomba ifanye kazi.

Tulishuhudia sote wakati wa Mwezi wa Ramadhani, *Alhamdulillahi* serikali ilifanya kazi nzuri sana ya kuwaondoshea kodi tende, mafuta, sukari, mchele, vitu vyote vinavyouzwa Ramadhani lakini *Wallahi*, mimi mwenyewe nilikwenda katika maduka kabla ya Ramadhani tende ilikuwa inauzwa 64,000 ilipoingia Ramadhani tende ikawa 92,000, sasa najiuliza imepunguzwa bei au imeongezeka bei. Tena basi serikali imeondosha kodi, hapo ndipo ninapoweka *verification that* mfanyabiashara hana dini, dini yake ghilba kitabu chake faida.

Mhe. Naibu Spika, nasema tena tuhakikishe tunawa *monitor* wafanyabiashara, ili wasiwaongezee bei wananchi wetu wanawaongezea bei. Kwa kumalizia nilisema siku moja pale Darajani kunapowale wauza mbatata waliwekeana *date* wakasema leo tuuzeni mbatata kilo shilingi elfu mbili, wote wakakubaliana wakauza bei hiyo kwa siku mbili. Baada ya siku ya pili mmoja akasema mimi siuzi, alichokifanya akawa anauza shilingi 1500/

ikawa mteja akenda kununua zile mbatata anamuuzia bei ile, wakamuona mbona anauza nyingi huyu, wakajua wakamtuma mtu kwenda kununua zile mbatata kumbe anauza shilingi 1500/= wakampiga.

Hii nini tunajifunga, tunajifunza kwamba mfanyabiashara anaamka asubuhi analiangalia soko halafu anaongeza bei, hakuna mfumo maalum. Mfanyabiashara narudia tena hana dini naomba sana serikali iwa *monitor* wafanyabiashara, ili wasikomoe wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, baada ya haya machache mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya watu wa Welezo kwa niaba ya wanamapinduzi wa nchi hii wakwezi na wakulima, nakushukuru sana na mimi naunga mkono hoja hii mia juu ya mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, niwashukuru sana kwa utulivu wenu pamoja na michango mbalimbali ambayo imetolewa lakini, Waheshimiwa Wajumbe nina wachangiaji kama 14 hapa ambao wote wanatakiwa wachangie leo pamoja na kama na Mhe. Waziri na yeye ana hoja ambazo atataja kuzitolea ufafanuzi basi tutatumia muda huwo huo wa jioni tuliona. Kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe, wale ambao wameleta majina yao waje mapema ili waweze kupata nafasi ya kuchangia mapema zaidi.

Jengine, naomba niwakumbushe Wajumbe Wawakilishi Wanawake (UWAWAZA) kuwa ile miadi ipo kwa hivyo baada ya kutoka hapa tukutane Mkahawani kwa ajili ya kufanya shughuli yetu.

Baada ya hayo machache, Waheshimiwa nawashukuru ..

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kuhusu utaratibu kidogo Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Spika: Kuhusu utaratibu hamna tumeshamaliza.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ungetutajia wachangiaji wa jioni ili tupate kujijua.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa nimesema wapo 14 na wewe kama umeleta na wewe utakuwemo ndani yao.(Makofi)

Kwahiyo, Waheshimiwa Wajumbe nasikitisha kikao hadi jioni saa 11:00.

(Saa 6:00 jioni Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

HOJA ZA KAMATI

Ripoti ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Mwaka 2017/2018

Mhe. Mwenyekiti: Sasa naomba nimwite Mhe. Masoud Abrahman Masoud atafutatiwa na Mhe. Mussa Foum Mussa.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipatia nafasi hii kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu...

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe samahani mheshimiwa nilikuwa naomba niwambie wachangiaji wetu ni wengi walibakia na muda utakuwa hautotosha kwa hiyo, ili kila mmoja apate nafasi ikiwezekana naomba waheshimiwa sana tuchaangie kwa dakika kumi ili tupate na wachangiaji wengine nao wapate nafasi.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipatia nafasi ya kwanza jioni hii kwanza nimkushukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia kukutana hapa kwenye kikao hiki.

Mhe. Mwenyekiti, nende moja kwa moja...

UTARATIBU

Mhe. Mwenyekiti: Naam Mhe. Jaku kuhusu utaratibu

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Nimesimama kanuni ya 63, 72 kiwango cha vikao, mheshimiwa idadi yetu haitoshi tunachangia mawaziri hawapo wahusika hao tunawachangia nani mswada huu, wahusika wenye shughuli hii hawamo humu ndani itakuwa tunatwanga maji kinuni na kanuni zimetupa kwa mujibu wa katiba labda nisome, wahusika mfano Waziri wa Kilimo yuko wapi, Waziri wa Biashara yuko wapi, Waziri wa Fedha yuko wapi tunamchangia nani. *(Makofi)*

Tumekuja kuwakilisha wajumbe ikawa hawa viongozi wetu wanaonesha mfano huu sisi tufanye nini, idadi ya nusu ya wajumbe hawajatimia naomba mheshimiwa muongozo wa kiti chako uwahirishe kikao wajumbe watafutwe *otherwise* tunatwanga maji kwenye kinu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku nimekufahamu na nimekuelewa na umesema mawaziri hawapo lakini mawaziri wapo kama serikali...

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Hoja ya pili mheshimiwa wajumbe hawajatimia nusu.
Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku nimekuachia umemaliza kusema na mimi niachie basi kwa hiyo mawaziri wapo na manaibu waziri wapo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Wahusika wa hii shughuli Mhe. Mwenyekiti, wahusika wa shughuli mawaziri wawili tu hawa ahaa.

Mhe. Mwenyekiti: Wahusika wa shughuli Mhe. Jaku ni serikali kwa hiyo ipo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Wawili tu waziri wawili Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum na Waziri wa Wanawake na Watoto hakuna waziri mwengine humu ndani.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku na mwenyekiti aliyetoa hoja yupo hoja ya mwenyekiti na mwenyekiti yupo mheshimiwa naomba tuendelee na waheshimiwa wanaingia.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kuendeleza kikao chetu hiki.

Mhe. Mwenyekiti, mimi moja kwa moja niwapongeze mawaziri wote watatu Waziri wa Fedha, Waziri wa Kilimo na Waziri wa Biashara pamoja na watendaji wao wote kwa kazi nzuri ambayo wameifanya na kutuwasilishia ripoti hii jioni hii.

Mhe. Mwenyekiti, mimi moja kwa moja niende kwenye ukurasa wa arubaini Wakala wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwanza nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kulipa umuhimu suala zima la kilimo na ndio maana katika taarifa yao humu tunaona kuna matrekta kumi mapya ambayo yameagizwa na matrekta thelathini na tano yako katika matengenezo na sasa hivi inaonekana yako mabondeni yanafanya kazi.

Mhe. Mwenyekiti, suala la matrekta ndani ya Zanzibar kila kipindi cha msimu wa kilimo inakuwa ni tatizo lakini niombe sana wahusika na suala la matrekta, kwanza suala hili linaonekana haya matrekta mapya sijui yamepelekwa kwenye mabonde gani maana yake mabonde yetu ya Wilaya ya Magharibi sijayaona sasa Mhe. Waziri atakapokuja labda pamoja anatakiwa atujibu mwezi wa tisa lakini kwa sababu sasa hivi kilimo kinaendelea ni vizuri wakulima watu wakajua hayua matrekta mapya kumi yanafanya kazi kwenye mabonde gani. Lakini Mhe. Mwenyekiti, haya mabonde ambayo yapo hayo matrekta ya zamani mimi bahati nzuri ni mkulima na nafatilia sana suala hili la kilimo.

Mhe. Mwenyekiti, trekta moja anapewa dereva mmoja na wanapangiwa kwa siku alime heka pengine ishirini na tano kwa kweli inakuwa ni usumbufu mkubwa sana, trekta unalijua ni la nguvu kwa nguvu dereva kufanya kazi toka asubuhi mpaka jioni si kazi rahisi, hatima yake tunachokivuna inakuwa dereva siku ya pili anaanza kazi saa sita za mchana ikifika saa kumi na mbili anapumzika na lile lengo ambalo limepangiwa alime heka ishirini hakuweza kulima.

Kwa hiyo, niombe sana kwasababu wenyewe wahusika wananisikia basi waandae utaratibu angalau trekta moja liwe na madereva mawili ili wapate kupokezana na mmoja apate angalau kumpumzika. Lakini pia mheshimiwa hao madereva watakuwa wanapewa *overtime* kwa bahati mbaya sana *overtime* hizi

hawapewi, sasa niombe sana madereva hawa waandaliwe utaratibu angalau na wao wa kupata *overtime* ili apate nguvu ya kufanya kazi siku ya pili katika shughuli yetu.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo niende suala *page* namba thelathini na sita kilimo cha umwagiliaji maji nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wza Baraza la Mapinduzi kwa uikipa nguvu sana kitengo hiki cha umwagiliaji maji.

Mhe. Mwenyekiti, mimi mwenyewe nitakuwa shuhuda baadhi ya mabonde sasa hivi yanafanya kazi za kutengeneza misingi ya umwagiliaji maji ili zile hekta ambazo Mhe. Waziri alizisema kwa itakapofika pengine bajeti ijao kutakuwa na hekta karibu elfu nane za umwagiliaji Zanzibar inawezekana hilo likawa lipo.

Lakini nataka niseme Mhe. Mwenyekiti, kwenye suala la umwagiliaji maji kuna suala zima la kilimo hiki cha shadidi ambacho Mhe. Waziri anakipigia makelele kweli kweli niwapongeze sana kwasababu Serikali inapotoa taaluma ya kilimo hiki cha umwagiliaji maji kabla wakulima kupata taaluma hii walifikiria uzalishaji utakuwa mdogo, lakini bahati nzuri kwenye robo moja wana uwezo wa kuvuna mpaka polo kumi na sita na wakulima wetu wamevuna na kwa bahati nzuri wamechukuliwa kupelekwa Tanzania Bara kuwa wakulima wa mfano kwa hapa Zanzibar, kwa hiyo uwezo wa kulima mpunga wa shadidi na kuvuna kwa kipato kikubwa kwenye roba moja upo.

Lakini niombe tu kwenye ukulima huu kidogo kuna changamoto, kwa sababu sasa hivi suala la kilimo huwezi ukalipeleka trekta kwenye mabonde ya umwagiliaji maji kwa hiyo, inabidi tutumie jembe la mkono au kwa kutumia majembe wanayolima kwa ng'ombe kwa kweli bei imekuwa kubwa na ukiangalia kwenye kilimo hichi kunahitajika mbolea, kunahitakija maji ni ya kununua na kwenye robo moja unahitajika ulipe shilingi thelathini elfu

niipongeze serikali inatusaidia kufidia kwenye suala zima la mbolea.

Lakini kwenye suala zima la umeme niombe serikali kwa heshima na taadhima kwa sababu kilimo hiki kinahimizwa angalau nao watufidie japo nusu ya gharama ili wakulima wetu wapate uwezo mzuri wa kulima hiki kilimo cha umwagiliaji maji.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye hili la kilimo cha shadidi Mhe. Waziri ana deni juzi aliulizwa swali Mhe. Naibu Waziri lakini akashindwa kulijibu, tulikwenda kwenye uzinduzi wa uvunaji wa mpunga kwenye eneo la Bumbwisudi na Mhe. Waziri aliwaahidi wana kikundi kuwa mpunga wao utakwenda kununuliwa na watu wa umwagiliaji maji kwa ajili ya mbegu, lakini kwa bahati mbaya sana mpaka leo mpunga ule haujaenda kununuliwa na juzi tu tulifanya ziara na Mhe. Machano, Mwachealale kwenye hicho kikundi basi tukaulizwa lakini tukasema tutamkumbushia Mhe. Waziri kwa sababu hii ni ahadi aliiweka na yeye hana tabia ya kusema uongo naamini ununuzi wa mpunga huu utakuja kufanikiwa.

Lakini kwenye hili hili la umwagiliaji maji kuna suala zima la *powertilar,* ma-*powertilar* Mhe. Naibu alipokuja kulizungumza hapa uzoefu unaonesha *powertilar* nyingi zinazoletwa kwa TASAF na wanaonunua watu binafsi zinakufa haraka. Mhe. Mwenyekiti, na Mhe. Waziri mimi niliwahi kuwa mkulima kiongozi na niwahi kupelekwa KTC Moshi kupata mafunzo ya kilimo cha umwagiliaji maji. Kule wenzetu hawatumii *powertilar* wanatumia matrekta ya akaunti ambayo yanaingia mpaka kwenye maji yanafanyakazi kwa kutumia *rotavator.* Kwa hiyo niiombe sana serikali kwa kipindi kijacho wajiandae ili kununuliwe haya matrekta, hivi vi-*powertilar* kila siku tunanunua lakini vinakufa haraka.

Mhe. Mwenyekiti, suala la mbegu niwapongeze serikali mbegu tayari wameshaleta lakini bado mbegu inaonekana ni kidogo kwa hiyo tuwaombe wizara waandae utaratibu mzuri kwa sababu bado wakulima wanahitaji mbegu katika maeneo yetu waweze kupatikana mbegu hiyo wamepelekewe huko mabondeni.

Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze sana Mhe. Makamu wa Pili pamoja na Rais wa Zanzibar, Wizara ya Kilimo iliandaa tamasha la Kilimo Kizimbani bahati nzuri Mhe. Rais alikuja kufungua, Mhe. Balozi alikuja kufunga nakumbuka Mkurugenzi wa Manispaa pamoja na watu wa wizara waliomba soko la jumapili, kila jumapili kuwe kunafanyika lile tamasha la kilimo kwenye eneo lile la Kizimbani. Lakini kwa bahati mbaya niliwahi kukutana siku moja na Mkurugenzi akanambia kidogo kunaonekana ndani ya wizara kuna uzito, pale likiwepo soko lile wananchi wanapata bahati nzuri kwenda kutafuta mbegu lakini pia wanapata kujifunza kupita kwa wenzetu ambao tayari wameshapata taaluma za kilimo za aina mbali mbali. Kwa hiyo niombe soko lile ambalo lilikuwa lifanye kwa ombi liloombwa kwa Makamu wa Pili wa Rais wizara iandae utartibu wowote lakini hiki kitu kipate kifanyike.

Mhe. Mwenyekiti, nilizungumzie kidogo namba ishirini na sita suala la ukodishaji wa mikarafuu nitazungumzia kwa Pemba nia yangu nizungumzie kwenye eneo langu la Kizimbani. Mhe. Mwenyekiti, taarifa tumeisikia kama Pemba kumekodishwa mikarafuu lakini asilimia kubwa ya fedha ambazo zimekodishwa hazijapatikana. Mhe. Mwenyekiti, la kusikitisha matangazo ya kwenye TV na redio walipokuwa wanatangaza walikuwa wanasema mtu yeyote atakayebarikiwa kukodishwa shamba lazima alipe robo, baada ya wiki mbili aweze kulipa pesa zilizobakia. Kwa bahati mbaya sana Mhe. Mwenyekiti, leo tunapata kauli kuwa watu wale hawajalipa fedha mpaka leo na karafuu zote wameshavuna sina uhakika Mhe. Mwenyekiti, kuwa

lile tamko au tangazo lilikuwa linatoka kwenye vyombo vya habari ambalo serikali ndio ililolitoa kuwa unakiwa ulipe robo ya fedha siku ya kubarikiwa baada ya wiki mbili umalize. Sasa mimi naomba sana kwa heshima na taadhima kawaida ya michangio hii tunataka tupewe jawabu mwezi wa tisa lakini kwenye hili naomba mwezi wa tisa tuje tuambiwe pesa zote zimeshalipwa tusije tukaletewa hadithi tena ya kuwa fedha hizi mpaka leo hazijapatikana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nilisema nilizungumza kidogo kwa Unguja lakini nia yangu ni kulizungumza suala la Kizimbani na ukodishaji wa mikarafuu.

Mhe. Mwenyekiti, shamba la kizimbani limezungukwa na Shehia ya Kizimbani, Dole, Mbuzini, Bububu, Miwani na maeneo ya Bumbwisudi, sisi ndio walinzi wa mashamba yale lakini Mhe. Mwenyekiti, karafuu zinapozaa au miti mengine kama midoriani, mifenesi na vitu vyengine vinapozaa sisi inakuwa sio wenyewe wanakuja wenyewe ambao wanakuja kukodishwa, tunaambiwa kunapigwa mnada lakini mnada huoni unamkuta mtu na majamvi anakuja kupiga kambi katika maeneo yetu, hatukatai kuwa zimekodishwa lakini sisi ndio walinzi tupewe kipa umbele. Siku yoyote ile kupigwe mnada wa wazi isiwe mnada wa siri kwa sababu inawezekana ikawa mikarafuu imezaa sana unakuja kukutwa imekodishwa milioni mbili kumbe karafuu zile zilikuwa zikodishwe zaidi ya milioni saba. Kwa hiyo niombe sana kwenye suala la ukodishaji hasa eneo la Kizimbani naomba sana wananchi wa Shehia ya Kizimbani waweze kushirikishwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye Wizara ya Biashara wenzangu wamelizungumza sana lakini mimi nataka niseme serikali inabeba mzigo mkubwa wa kodi kipindi cha mwezi wa ramadhani wananchi wetu angalau bidhaa zipatikane kwa bei nafuu, lakini kwa bahati mbaya sana wafanyabiashara wa Zanzibar

hawapangiwi bei wanajipangia wao bei kulingana na meli. Meli wakigundua ina wiki mbili mbele itakuwa haijafika Zanzibar basi kama kuna polo za mchele mtu anapandisha bei, sukari anapandisha bei ilimradi kwa ule muda ambao meli itakuwa haijafika yeye mfanyabiashara anajipangia kupata faida.

Sasa niombe kwa mwezi huu wa ramadhani huwa tunasamehewa sana kodi wao wafanyabiashara hasa hii wizara ya kumlinda mlaji tuangalie utaratibu wa kuhakikisha hizi bei ndani ya maduka kama wanavyokuja Idara ya Chakula hawa, wanakuwa wanakuja chakula gani kimesha *expire* basi waje na madukani waangalie tende inauzwa bei gani kwa mwezi ule wa ramadhani ili angalau ile kodi isiwe wanapunguziwa wafanyabiashara sasa hawapunguziwi walaji, walaji kodi inaendelea kuwa ile ile kwa hiyo niombe sana kwenye hilo.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, niende moja kwa moja kwa Waziri wa Fedha na yeye kuna lake kwa watu wa Benki ya Watu wa Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi siku ambayo utatia nia ya kwenda kupasisha gari yako basi ujuwe siku nzima hufanyi kitu chochote unakwenda kwenye suala zima la kupasisha ukienda benki pale unakwenda unakaa zaidi ya masaa manne kutafuta kulipa shilingi elfu tatu. Nimuombe Mhe. Waziri aandae utaratibu wowote kule karakana kule Chumbuni kule kuwe angalau na eneo la kulipia unatoka kupasisha unalipia unamaliza shughuli zote palepale ili wananchi wetu wasipate tabu sana.

Mhe. Mwenyekiti, hilo nilitaka niseme lishasemwa mara nyingi lakini naomba na mimi nilitile mkazo...

Mhe. Mwenyekiti: Malizia mheshimiwa malizia.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Mwisho niunge mkono hotuba hii ya wizara hizi tatu kwa asilimia mia moja.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Masoud sasa naomba nimwite Mhe. Mussa Foum Mussa atafuatiwa na Mhe. Hidaya Ali Makame na Mhe. Miraji ajiadae.

Mhe. Mussa Foum Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipa ruhusa kuwa ni mchangiaji wa pili katika jioni hii.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi vile vile niipongeze kwanza Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi kwa ripoti yake nzuri yenye kueleweka. Mhe. Mwenyekiti, pia vile vile niwapongeze mawaziri watatu Waziri wa Kilimo, Waziri wa Biashara na Waziri wa Fedha pamoja na watendaji wake wote kwa kazi nzuri wanayoifanya katika mawizara yao.

Mhe. Mwenyekiti, mimi vile vile napenda nianzie kuchangia katika ukurasa wa ishirini na nane ingawaje wenzangu wameshazungumzia sana juu ya suala la ukodishwaji wa mashamba ya eka Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, hapa tumeelezwa utekelezaji wa zoezi la ukodishaji, matokeo ya ukodishaji na ukusanyaji wa mapato mambo yote hayo yameelezwa katika sehemu hii lakini mimi nataka kutoa maelezo zaidi hapa palizungumzia kwamba kamati zimefanikiwa kukodisha jumla ya mashamba ya eka 1452 sasa na asilimia 95 ya makadirio hayo.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza sina budi niipongeze hiyo kamati ya ukodishaji wa mashamba kwamba kwa mwaka huu wamekodisha mashamba mengi ni vyema tukawapongeza kwa jitihada yao kubwa waliyoifanya hii.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, nataka niseme kwamba hakuna jambo zuri lisilo kasoro. Kwa mawazo yangu mimi katika huu ukodishwaji wa mashamba kulitokea kasoro ndani yake, nataka nielezee kidogo namna kasoro zilivyojitokeza.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza matangazo yalivyokuwa yanatoka kwa mfano leo tunakwenda kukodisha mashamba Mkoani, tangazo lilikuwa linasema kwamba yeyote atakayebarikiwa basi atoe asilimia 25 pale pale na asilimia 75 iliyobakia baada ya siku 14 na atakaposhindwa kutoa hiyo pesa, basi pesa yake ile asilimia 25 itakuwa imekwenda na maji. Lakini hapa leo tunaambiwa kwamba katika watu waliokodishwa hayo mashamba pesa mpaka hii leo zimepatikana kidogo nyengine bado hazijapatikana. Sasa mimi hapa nimepata mshangao kwa nini mpaka hii leo kuna watu wanadaiwa pesa hii hawajalipa ina maana hawakuheshimu matangazo yaliyotolewa pale kabla.

Mhe. Mwenyekiti, mimi namuomba Mhe. Waziri atakaposimama na yeye kutoa hayo maelezo basi hapa atupe maelezo ya kina, kwa sababu mwanzo wa mashamba ya eka yalivyowekewa utaratibu mwanzo akodishwe yule mtu anayelishughulikia. Lakini kwa matangazo yalivyotoka na umasikini wetu tulionao Pemba mtu akajiona hana pesa ya kulipa wakati ule. Kwa hivyo, shamba ikabidi alikose, lakini matokeo yake bora apewe yule yule kuliko kukodishwa mtu mwengine aliyekuwa mpaka leo pesa haijapatikana.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niseme kwamba serikali ifanye jitihada kubwa kwa sababu watu wa zamani walisema hukuvua maji kame uje uvue maji yameshajaa, si rahisi. Leo pesa hazikupatikana wakati wa kuvuna karafuu na msimu umeshapita sijui kama hiyo pesa itapatikana. Sasa hapa pana ugumu mkubwa sana wa kuipata hiyo pesa.

Mhe. Mwenyekiti, halafu wanaoshughulikia mashamba wanapata dhiki. Kwa mfano, kuna watu wanashughulikia mashamba zaidi ya miaka 20 wameyakuta mashamba, wamevunja mapori, wamepanda mikarafuu upya wameyaomba mpaka hivi sasa hawajayapata ingawaje wameambiwa yatakapotolewa mtapewa lakini muyashughulikie. Leo mtu ameshapanda mikarafuu shamba analishughulikiwa, shamba wenyewe linaweza likafika pengine miaka mitatu halijazaa lakini lazima ulishughulikie kwa kulilima. Leo unaambiwa linakodishwa na serikali unaambiwa upewe ama asilimia 40 au 30 au 20 au 10, kweli ile gharama yako italipa? Hailipi kwa hivyo wale wanaoyashughulikia mashamba tunawavunja moyo kwa sababu kile wanachotumia kwa asilimia hii hakilipi.

Kwa hivyo, napenda niseme kwamba Mhe. Waziri tunaiomba serikali watu wa zamani wanasema iliyopita si ndwele tugange ijayo, kwamba hili limeshapita ingawaje mnadai mtajua nyinyi huko. Lakini kwa mara nyengine utakapotokea msimu wa karafuu basi wale wanaoshughulikia mashamba wapewe kipaumbele japo na wao kwa kukopeshwa, kwa sababu tumeshaiona athari hii.

Mhe. Mwenyekiti, halafu ubaya wa mambo uliokuwa ukitendeka mtu huyo huyo anatoka Chake-Chake leo mnada Mkoani, mtu huyo huyo mnada Kichunjuu, mtu huyo huyo mashamba yote anapewa mtu mmoja, hapakufanyika vizuri. Mhe. Mwenyekiti, kwa mara nyengine tunaomba utakapotokea huo msimu na karafuu zitakapozaa basi kwanza wapewe kipaumbele wale wanaoyashughulikia wakodishwe wale mwanzo hata kwa kukopeshwa kwa sababu hawa ndio wamekula dhiki, hawa wameyakuta mashamba hayana kitu, mikarafuu yote imekufa wamepanda wao. Leo matokeo yake imetokea neema hawa wananyimwa, Mwenyezi Mungu hatotuacha na jambo moja ndio hili tumewapa watu wameshachuma karafuu, wameshakimbia na pesa hatujapata, wale walioyashughulikia hawakupata kitu. Sasa

Mwenyezi Mungu hayuko radhi. Mhe. Mwenyekiti, hilo ndio ombi langu kwamba msimu mwengine utakapofika watu wanaoshughulikia mashamba wapewe kipaumbele.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile niseme kwamba kuna watu haya mashamba wanayo kwa muda mkubwa, na hapa tunaambiwa kwamba wote wale waliopewa nyaraka baada ya Mhe. Rais wa Kwanza Mzee Abeid Amani Karume na Mzee Jumbe wote waliokuja nyuma yake nyaraka hizo hazifai. Sawa sawa na iwe hivyo lakini watu wanayaomba haya mashamba ili wakabidhiwe kwa sababu Mzee Karume ametoa mashamba ili kusaidia wanyonge, bado mpaka hii leo wanyonge wapo. Kuna sababu gani mtu analo shamba amelikuta halina kitu, amepanda mikarafuu, shamba lina mikarafuu leo matokeo yake inafika wakati wakukodisha yeye hapati kitu, kwa nini? Hebu turudisheni ile ile kwamba mtu kama huyu basi hili shamba apewe kwa waraka ili aendelee kutumia muda unakuwa mkubwa.

Kwa mfano, ninae mzee wangu hapa analo shamba tokea mwaka 1995 na amepeleka maombi yake kwamba apewe hilo shamba 1996, mpaka hii leo shamba hilo ameambiwa kwamba shamba hili tunakukabidhi uendelee kulitunza mpaka hapo muda utakapofika kutolewa na wewe utakuja kutazamwa kama utapewa au hutopewa. Sasa muda unakuwa mkubwa manung'uniko yanakuwa mengi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kumaliza hapo niende katika suala la Shirika la Biashara (*ZSTC*)…

Mhe. Mwenyekiti: Una dakika mbili mheshimiwa.

Mhe. Mussa Foum Mussa: Haya nitamalizia Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, hapa nakwenda katika changamoto. Mhe. Mwenyekiti, kuna changamoto ya mwanzo inasema udhibiti mdogo wa watoto chini ya miaka 18 kujishughulisha na uchumaji wa zao wa karafuu kwa kupata athari mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, sote tunaelewa kwamba Zanzibar zao letu kubwa sisi hapa tunategemea karafuu hususan Pemba. Ukiangalia vijana wenye umri chini ya miaka 2 mpaka miaka 18 hapo kati kati unaweza ukawakuta watu kuanzia miaka 10 mpaka miaka 17 wameshaoa na wana watoto. Sasa ukisema kwamba watu hawa wadhibitiwe, hapa utakuwa unasema nini na sisi sote tunategemea zao la karafuu, karafuu ikiingia mdogo, mkubwa anategemea kupata chochote. Nadhani serikali ikiwa kuna ule mpango wa bima kwamba watoto wadogo hawakuwekewa bima, basi kuanzia hiyo miaka ya chini mpaka miaka 18 hapa serikali ijikite likitokea suala lolote ibebe serikali kwa sababu hili jambo ni jambo kubwa, haiwezekani kwamba watu wenye umri huu wazuiliwe au wasiende kuchuma au itakapotokea athari yoyote wao wasishughulikiwe, hili jambo ni kubwa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo naunga mkono hoja.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mussa Foum Mussa kwa mchango wako, sasa naomba nimwite Mhe. Hidaya Ali Makame, atafuatiwa na Mhe. Miraji Khamis Mussa na Mhe. Jaku Hashim Ayoub ajiandae.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipatia na mimi nafasi yakuweza kuchangia machache juu ya ripoti hii ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza na mimi nichukue fursa hii kuwapongeza sana Wajumbe wa Kamati hii kwa kazi ngumu ambayo wanaifanya katika wizara hizi tatu, lakini pia kwa

kushirikiana na mawaziri husika wa wizara hizi. Niwapongeze sana pamoja na Makatibu wao na Manaibu Mawaziri pia.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nianze kuchangia kwenye ripoti hii, mimi moja kwa moja naelekea ukurasa wa 25 Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi.

Mhe. Mwenyekiti, kamati imetembelea maeneo mengi tuipongeze sana kwa kazi kubwa waliyoifanya, lakini kwa uchambuzi wa kina ulionekana kwenye ripoti hii kuhusu masuala ya utekelezaji wa bajeti, na kutembelea katika maeneo mbali mbali. Mhe. Mwenyekiti, mimi hapa kwenye Wizara ya Kilimo ningezungumzia sana suala la Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Chuo cha Kilimo Kizimbani.

Mhe. Mwenyekiti, nikianza kwenye suala la utafiti ambalo linahusiana na Chuo cha Kilimo Kizimbani nina masikitiko makubwa sana. Kamati hapa wameeleza kwenye changamoto, lakini ukiachia hizi changamoto ambazo zimeelezwa na kamati hapa hazipungui nane. Kuna changamoto nyingi sana ambazo zimeikabili Taasisi ya Utafiti Kizimbani pamoja na Chuo cha Kilimo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitazungumzia miti ambayo ilipandwa pale chuoni kwa ajili ya utafiti. Kuna miti mingi sana ambayo imepandwa tangu wengine hata hatuna nia mayai yetu hayajaundwa ile miti ipo na mpaka sasa hivi bado inazaa. Lakini kwa kweli miti ile imeshakuwa sasa hivi tena inakufa, kila baada ya siku huoni ni jitihada gani ambayo wizara au taasisi itachukua juhudi ya kuizalisha tena upya miti ile na ikaendelea kuwepo.

Mhe. Mwenyekiti, nasikitishwa sana na shamba lililopo Mndo ambalo shamba hili ni la utafiti wa Chuo cha Kilimo Kizimbani, shamba hili lina miti ambayo tuseme ndani ya Zanzibar yetu ndio

inapatikana pale tu. Kuna miti pale ya *mangosteen*, kuna shokishoki bundala, kuna shokishoki za kawaida, kuna miratabu, kuna mi-*apple* ya Kiswahili, kuna muhogo, kuna michungwa, kuna miti tofauti. Lakini kwa hii miti ambayo nimeitaja mwanzo ambayo ni mishoki shoki bundala na *mangosteen* ni miti ambayo ya zamani na ya siku nyingi sana inafikia hali ya kwamba sasa hivi miti ile ule uwezo wake wa kuzaa umeshapungua kasi. Miti hii inahitaji sana kuendelezwa ndani ya shamba lile kwa sababu ni miti ambayo hadhi yake ni kubwa, na ni miti ambayo hao wageni wenyewe watalii wakifika hapa wakiambiwa kwamba ndani ya Zanzibar hii miti hii inapatikana basi wao wenyewe wanashangaa. Lakini tunaona hata kwenye masoko yetu haya ya Kiswahili, miti hii ya matunda tunda lake moja ukilikuta huko sokoni bei yake kutokana lilivyo huwezi kuamini kwamba bei yake ni kubwa na hadhi yake pia ni kubwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu unaambiwa mti mmoja wa *mangosteen* unaweza kuukodisha si chini ya milioni mpaka tatu. Je, hatuoni thamani ya mti huu? Ijapokuwa miti hii imeoteshwa kwenye shamba la utafiti, lakini limo ndani ya Wizara ya Kilimo, je wizara hainufaiki, haipati faida, na je hizi faida ambazo zinakodishwa ndani ya miti hii zinakwenda wapi? Kama ni Chuo cha Kilimo Kizimbani kina changamoto nyingi sana, kuna umuhimu mkubwa sana wa maeneo haya au miti hii kuimarishwa.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani ninapozungumza shoki shoki bundala humu wachache sana wanaozijua, naweza kusema hao mawaziri pia kuna baadhi hata hawajawahi kuzisikia. Hizi shoki shoki zipo na zinapatikana ndani ya Shehia ya Kizimbani na miti yake haizidi mitano iliyokuwemo ndani ya shamba lile.

Mhe. Mwenyekiti, ningeiomba sana wizara kupitia Taasisi ya Utafiti Kizimbani, hii taasisi niseme kwamba labda inaendea mwishoni, kwa sababu pale chuoni tunaona kwamba kila siku

wanafunzi wanaingia lakini je tujiulize wanakwenda kusoma nini wanafunzi wale? Kilimo si aghlabu kusomeshwa ubaoni, kilimo unagusiwa tu kidogo ubaoni ni sawa sawa na mambo ya upishi. Upishi utasoma kidogo ubaoni lakini baadae vingi unaenda kuvifanya jikoni kwa sababu ndiko kunakostahiki na upishi. Kwa hiyo, na hiki kilimo unapomaliza kusoma ubaoni kwa dakika chache, dakika nyingi unaenda kuzitumia kwenye *practical* ambayo ni ya kulima na kufanyia utafiti hii miti. Sasa kila siku tukiwa tunapokea wanafunzi pale tunaenda kuwaweka pale halafu huo utafiti wenyewe wanaokwenda kuusomea hiyo miti inakufa. Leo hii tunaona pale kuna hiyo mipili pili manga lile shamba la mipilipili manga ambalo nalo ni la utafiti linakwisha kwa sababu ile miti inakauka, ile mijenga ua ambayo ilijengewa iliwekwa pale kwa ajili ya kukuza ile mipilipili manga nayo imeshakuwa mipevu inakufa.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia tunaangalia kwamba hii hii shamba ya mipilipili manga, pili pilimanga tunaijua bei yake sasa hivi ni bei ambayo ipo juu kupindukia kwa haya mazao ya *spices*, lakini hatujasikia hata siku moja hapa ndani ya wizara tukaambiwa kwamba leo kuna uboreshaji au ndani maredio tukasikia kwamba kuna uboreshaji wa shamba la mipilipili manga au kuna uboreshaji wa shamba la midalasini na mengineyo ndani ya Chuo cha Kilimo Kizimbani.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli kuna haja tukakaa tukalitizama maeneo ya utafiti ndani ya Chuo cha Kilimo Kizimbani.

Mhe. Mwenyekiti, pia nitaizungumzia *vanilla*, *vanilla* nayo ni sehemu kubwa sana ambayo tunastahiki kupata pongezi ndani ya nchi yetu kwa sababu tunajitahidi kuimarisha. Pia ukiangalia katika shamba lile lile la utafiti Mhe. Mwenyekiti, vanilla zimeshakauka. Kwanza jua ni kali na jua kali sasa hivi linasababishwa na kukatwa na hiyo miti na mengine inakufa

wenyewe kutokana na kwamba haina uimarishwaji, haina ushughulikiwaji, ushughulikiwaji wake ni mdogo.

Mhe. Mwenyekiti, ni vitu ambavyo ukipita kama ni mzaliwa ambaye unatokana na ile Kizimbani sasa hivi ukienda pale machozi yatakutoka kwa sababu ile Kizimbani ile hadhi haipo sasa hivi. Kizimbani ilikuwa wewe ukifika Bububu basi harufu ya Kizimbani tayari umeshaipata kwa mazao na matunda ambayo yanapatikana pale, chuo hukioni lakini unakiona kutokana na zile harufu na hadhi ya Kizimbani iliyokuwepo.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi hakuna mcheza jemu wa utafiti, hiyo michungwa iliyokuwepo ipo robo *percent* ambayo nayo kila siku inakodishwa lakini hata hizo bei hatujui zinakodishwaje. Nitalizungumzia shamba la mikungu manga ambalo pia lipo kwenye eneo la Chuo cha Kizimbani.

Mhe. Mwenyekiti, Chuo cha Kilimo Kizimbani kina maeneo ya mashamba ambayo ya utafiti lakini pia yakikodishwa chuo kinajiendeleza, lakini kila siku ukiuliza pale amekodi nani unaambiwa kuna babu gani sijui analipaje hata sijui maana yake hata sifahamu anakodishwa vipi. Hizi jawabu zinavunja moyo kwa sababu tunafahamu kwamba kungumanga moja inauzwa mia tano au elfu moja mia tano, nambie mkungu manga mmoja unazaa si chini ya mazao elfu tatu wakati shamba lile lina ukubwa wa heka mbili kwa tatu. Je, niulize hapa hapaingii faida ndani ya chuo kile ambacho tunaambiwa baadae bajeti zake hazifahamiki, zinaweza kusaidia zile zile nyenzo ambazo zinazunguka ile taasisi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli kuna haja ya kukaa wizara ikaliangalia tena eneo la Chuo cha Kilimo Kizimbani kwa masuala yote yanayohusika na mafunzo ambayo yanaileta hadhi nchi yetu na kuipa umaarufu zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, Chuo cha Kilimo Kizimbani kina hadhi kubwa ndani ya nchi hii, kwa sababu ndio chuo cha mkulima na mkwezi, kila mmoja analima hata uwe tajiri wa aina gani lakini bila ya kilimo hujakuwa tajiri. Mhe. Mwenyekiti, ningeiomba sana wizara ikaliangalia suala hili lakini pia ikakiangalia Chuo cha Kilimo Kizimbani, kuna mashine nyingi pale hazifanyi kazi mbovu, yaani hata sijui zikoje. Kuna ile mashine ambayo imetaka kufungwa pale sijui mwaka wa ngapi huu inashindikana ya usagaji wa matunda.

Mhe. Mwenyekiti, ni hali ambayo inasikitisha, kinachorejesha nyuma zaidi pale kuna wazaliwa ndani ya kijiji kile ambao wazaliwa hawa ikiwa kunatakiwa kufanywe mambo ya kusafisha wanatafutwa wale wanashughulikia miti, wanashughulikia mashamba, wanashughulikia kila kitu kinachohusika na pale, siku za ajira wale wanasahauliwa wanakwenda kutafutwa watu wasiojulikana wanakwenda pale kupelekwa kwamba ni waajiriwa wakafanye kazi. Watafanya kazi waliokuwa hawaijui wakati wale wenye uchungu na uzalendo wa pale hawaonekani? Hili ningependa sana kulizungumza lakini pia na mawaziri walisikie na walijue umuhimu wake na wauone.

Mhe. Mwenyekiti, nimeona tayari umeshaniwashia taa nafikiri kwa ajili ya muda, lakini nimalizie kwa kusema kwamba bila kilimo nchi yetu itayumba naweza kusema hivyo. Mhe. Mwenyekiti, kilimo ndio uti wa mgongo wa masikini na tajiri. Niseme kwamba naiunga mkono Ripoti hii ya Kamati lakini pia niwaombe sana mawaziri kwa haya ambayo tunayachangia ule muda utakapofika wa kuja kujibu basi watoe majibu kwa wananchi ambayo yatawapa mwanga na mwelekeo. *(Makofi)*

Nimalizie kwa kusema naunga mkono ripoti hii kwa asilimia mia moja na niwashukuru sana Wajumbe wa Kamati. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Nakushukuru sana Mhe. Mjumbe kwa mchango wako sasa naomba nimwite Mhe. Miraji Khamis Mussa atafuatiwa na Mhe. Jaku Hashim Ayoub na Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi ajiandae.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi jioni ya leo na mimi kuwa mchangiaji kwenye Ripoti hii ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo. Mhe. Mwenyekiti, naomba na mimi niungane kumpongeza Mhe. Mwenyekiti wa Kamati pamoja na kamati yake kwa ripoti yao nzuri, imeyaibua mengi na sisi hatutakuwa na mengi ya kusema kwa sababu mengi waliyoyaona yameweza kuisaidia serikali katika kutafuta mwelekeo wa kuwatumikia wananchi.

Pia niwapongeze mawaziri wote watatu Waziri wa Fedha na Mipango; Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko na Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi na Manaibu Waziri pamoja na Makatibu Wakuu wote na wasaidizi wao.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba hivi sasa kwa haraka haraka mana dakika kumi ni chache niende kwenye eneo la *ZIPA*. Kwenye eneo hili Mheshimiwa ukisoma changamoto kuna changamoto ambayo inajaribu kutoa mwelekeo ambao sio mzuri wa kukosa mashirikiano na taasisi nyengine. Maana kama changamoto zake pale wanazilalamikia taasisi za serikali kukosa ule umoja wa kufanya kazi ili mambo ya uwekezaj yaende vizuri. Sasa wazo langu kamati imefanya vizuri lakini moja ya pendekezo basi serikali kwa kuona umuhimu wa kutatua tatizo hili iandae *stop center* moja ambayo itawashirikisha wadau wote wale ambao watahusika katika uwekezaji wetu. Kwa mfano utalii, *immigration*, Ardhi, Wizara ya Fedha, lakini na Wizara ya Kazi kwa sababu kuna masuala ya vibali.

Sasa *stop center* ile inaweza ikatusaidia kuondoa ile minong'ono ya pamoja mana hawa wote tukiwaweka kwa pamoja ile kazi inayohitajika pale basi wataifanya kwa wepesi zaidi. Sasa ushauri wangu lile wazo limekuwa likizungumzwa mara kwa mara basi serikali iandae utaratibu mzuri kwa kutuwekea *stop center*, ambayo itawashirikisha wale wadau wote ambao pengine akija kuwekeza itakuwa ni sehemu ya upatikanaji kwa urahisi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niende Tume ya Mipango. Katika eneo la changamoto na wao pia changamoto yao wameelezea kuwa bado mfumo wa uongozi katika njia ya ugatuzi haujafahamika kwa baadhi ya viongozi wanaoshughulikia yale maeneo yaliyogatuliwa. Sasa kidogo inatupa mashaka kwa sababu unafika pahala tunapoingia katika mfumo mpya lazima serikali itakuwa imefanya *study*, lakini lazima serikali iwape elimu wale maafisa ambao wizara na taasisi zao zimegatuliwa. Lakini leo toka ugatuzi upite karibu tuna miezi kadhaa kamati inapita kuna changamoto ya aina hii, sasa tunapata mashaka sana na mapendekezo ya kamati pia yakawa yako *silence*.

Sasa nilikuwa napendekeza Mhe. Mwenyekiti wa Kamati kuwa moja ya jambo ambalo muhimu kwa zile taasisi zote zilizogatuliwa basi maafisa hawa wawekwe pamoja, wapewe ile elimu ya ugatuzi ili tatizo hili liondoke na wananchi waweze kupata huduma kama tulivyowatarajia.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niende *BoT*, nachangaia haraka haraka. Kwenye sehemu hii ya *BoT* Mhe. Mwenyekiti wa Kamati tunamshukuru kwa yale ambayo wametuainishia, lakini kwa ujumla moja ya kazi za BoT nilikuwa naisoma ile (b) kufuatilia mwenendo wa uchumi wa Zanzibar. Kuna kadhia moja kubwa ndani ya utaratibu wa kuu-*control* huo uchumi tunaousema, wako wenzetu wanaishi nje wanatuma pesa kiholela nchini kupitia

bureau de change, kupitia mawakala tofauti. Sasa fedha ya kigeni inapoingia na ikatumika kwa wingi maana uchumi wako uko hatarini, vyenginevyo iwe tunakielewa kinachoingia lakini tuweze ku-*balance* maana yake kwa kiwango hiki. Sasa *BoT* hawa wanazisimamia *bureau de change*, benki zote lakini kuwe kuna utaratibu mzuri wa uingizaji wa fedha kwa wale wenzetu waliokuweko nje. Fedha inaingia kiholela sana ya kigeni na tunakosa kuitambua na ni hatari kwa uchumi wetu. Fedha ikiingia sana tukairuhusu kutumika sana wakati fulani huu uchumi jitihada za viongozi zinaweza zikenda vizuri katika kukuza uchumi, lakini ukiingiza pesa ya kigeni ndani ya nchi yako bila ya kiwango unachokitambua ni hatari.

Sasa nawaomba wenzetu kunako eneo hili nalo walione, moja katika changamoto ambayo tunaweza tukaizungumza kila wakati basi na hii iwe miongoni mwao.

Naomba niende Benki ya Watu wa Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, kwenye eneo hili tulijikita sana katika matatizo yale ya moja kwa moja ambayo tumezungumzia majengo na changamoto zao. Lakini changamoto katika eneo la huduma hatukuliweka na ndio changamoto muhimu. Kwa sababu benki tumeiweka isogee isiweko tu pale, sasa changamoto kubwa mabadiliko ya mfumo bado sisi tuko katika umoja na hili naendelea kulisema. Umoja ule unaturahisishia kupata huduma katika maeneo tuliyonayo, lakini sasa hivi lazima tutoke pale twende kwenye *visa*, lazima tutoke pale twende kwenye *master card*, lazima tutoke pale kwenda katika *internet banking*. Lakini pia katika nchi yetu waanzishe mfumo Benki yetu hii ya *PBZ* angalau ya malipo kupitia kadi zile *transaction* ndio huduma yenyewe. Sasa leo kuna mabenki mengi mpaka afanye malipo mtu atoke Kiwengwa huko, lakini kuna malipo rafiki ambayo ule mfumo wakaweza kuuendeleza basi tunaweza tukapata mapato na tukakuza uchumi wetu zaidi.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, katika eneo la huduma kwa uharaka naomba nichangie hivyo kwa sababu dakika ni chache na taa karibu itawashwa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niondoke katika eneo hilo niende katika mamlaka ya ununuzi na uondoshaji wa mali za umma. Katika changamoto yake moja namba 2 na naomba nisiisome kwa sababu vitabu sote tunavyo, lakini changamoto hii Mhe. Mwenyekiti, haikutolewa mapendekezo yake. Sasa mapendekezo yake tuiombe mamlaka inayohusika tunashauri itekeleze wajibu kwa mujibu wa matakwa ya sheria tuliyoitunga. Maana tumeiweka vizuri lakini nasema mapendekezo yale sitaki kuyasoma kwa sababu sote tunavyo vitabu, lakini tuone yale mapendekezo katika maeneo ya kamati basi na hilo liwepo ili zile kazi ziende, tusiiache *free* kwa sababu kazi yetu ni kushauri. Kwa hivyo, moja ya ushauri wetu Mhe. Mwenyekiti, naona nalo lingekaa katika utaratibu huo.

Mhe. Mwenyekiti, kuna eneo la Shirika la Bima Tawi la Pemba. Moja ya changamoto yake kuchelewa kupata ufumbuzi kutokana na Wizara ya Fedha na Mipango juu ya kandarasi wa ujenzi wa jengo la Bima Pemba. Sasa katika utaratibu huu Wizara ya Fedha ndio inayosimamia tawi la bima. Sasa changamoto hii tukikutana nayo lazima mwenyekiti wa taasisi hizi au wizara hii tusaidie kukutana nayo ili hizi changamoto ziende basi huu ujenzi ufanyike. Sasa leo kamati inakwenda tunakuja kuziripotia na hawa wote wamo ndani ya taasisi moja wakati fulani tunapata mashaka kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niende sasa kwenye eneo la Wakala wa Matrekta, naona nihame Wizara ya Fedha sasa hivi niende kwenye wakala wa matrekta na mwenyekiti namalizia maana sina michango ya ziada sana. Kwenye eneo hili kuna kipengele wakala imepokea matrekta kumi mapya kutoka Ubalozi wa Libya, lakini

yameshindwa kufanya kazi mara tu baada ya kufika kutokana na vifaa kutolewa yalikohifadhiwa.

Sasa katika mapendekezo ya kamati mana hapa nayo pia hiyo sentensi iko *free* kidogo, hatujui kama sisi tulikabidhiwa vifaa vimeshatolewa na kama vimetolewa maana yake basi maudhui ya hapa hayasomeki hivyo. Lakini kama tulikabidhiwa matrekta na vifaa vyake vimo tumekuja kuvitoa sisi maeneo tuliyoyahifadhi sisi. Sasa hatuwezi kuacha *free* lazima tufike pahala Mhe. Mwenyekiti, tutoe mapendekezo na maoni yetu kama hawa wote waliohusika na kadhia hii maana tuliwakabidhi watu, basi wachukuliwe hatua zinazostahiki kwa mujibu wa sheria. Sasa haya mapendekezo ya kamati na kadhia hii yote iliyotokea basi unakuta maeneo haya yote yako *free*.

Sasa nasema nilipokuwa naipitia sijabaini kama labda kukabidhiwa kwa matrekta haya tulikabidhiwa yakiwa pungufu vifaa hivi, lakini sentensi inakuja tulikabidhiwa yakiwa kamili maana matrekta mazima. Sasa kama kuna eneo tulihifadhi lakini na wenzetu wakafika pahala wakavitoa vifaa hivi, basi lazima hatua za kisheria tuchukue na maoni ili tupate utekelezaji yabaki. Kwa hivyo, moja ya maoni yangu kuwa hao wote ambao wamehusika na utoaji wa vifaa hivi basi kamati Mhe. Mwenyekiti wa Kamati tuagize serikali wachukuliwe hatua kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimalizie katika eneo la kitalu cha Chanjaani. Kuna eneo limeandikwa hapa katika changamoto, Sera ya Serikali ya Utoaji Bure Miche ya Mikarafuu iliwekwa kwa nia njema kabisa, lakini inatumiwa vibaya kwa baadhi ya wale ambao tunawasaidia miche bure. Kunako eneo hili Mhe. Mwenyekiti, lazima sasa kwa sababu serikali inachukua hatua ya uzalishaji wa miche lakini tunaowapa yale malengo tunayoyakusudia hayafikiwi, sasa lazima ule utaratibu na sisi tuubadilishe. Sasa

tuwe tuna utaratibu na mikakati mipya ya kuwapa miche hii wakulima, wale ambao wanakwenda kuitelekeza basi hatua nazo ziende tusiwape tu tukawaachia wakawa *free*, tuwape bure ikisha wakaitelekeze bila ya kufanya *follow up* yoyote, hiyo itakuwa ngumu tutaharibu nguvu na ile dhamira ya serikali.

Kwa hivyo, bora tufike pahala wale wote watakaoharibu kwa makusudi na katika ile dhamira ya kawaida ya kuwapa bure ibaki, lakini utaratibu sasa tuuandae mzuri tutakapowapa wakaharibu basi hatua nao tuwachukulie, hatuwezi kuwapa bure ikisha wakenda wakaharibu, yenyewe katika sura nyengine mikarafuu hii tunakuwa tunaipanda sisi wanakwenda kuikata, sasa pengine hao tunaowapa ndio hao ambao wanataka hiyo mikarafuu isibaki ndani ya nchi yetu. Kwa hivyo, katika maoni yangu kunako eneo hilo lazima wizara iandae utaratibu mzuri ambao unaweza ukatusaidia kuibakisha dhamira nzuri ya serikali kama hapo awali.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Miraji Khamis kwa mchango wako, sasa naomba nimwite Mhe. Jaku Hashim Ayoub, atafuatiwa na Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi na Mhe. Hamza Hassan Juma ajiandae.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nami nikushukuru; tunachangia ripoti za wizara tatu ikiwa ni Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi. Lakini kwa bahati nzuri ninayemuona ni Waziri wa Fedha na Waziri wa Kilimo, Waziri wa Biashara simuoni wala kaimu wake simuoni sijui hayo majibu atakuja kutoa nani, lakini najua serikali ipo vile vile.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze na mchango wangu kwa huzuni kubwa, katika ukurasa wa 5 Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi (*ZIPA*). Mhe. Miraji Khamis Mussa kazungumza serikali inayoongozwa na Dkt. Ali Mohamed Shein Rais makini kabisa anachukua jitihada kubwa sana. Nimezungumza na *hansard* zipo, haijafika hata wiki baadhi ya watendaji wanaendelea kumdanganya Rais wetu na ara nyingi hujaribu kufuatilia sikurupuki tu, kitengo hiki ni muhimu *ZIPA* hata katika Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi kimo.

Mhe. Mwenyekiti, Waziri wa Fedha naomba anisikilize kwa makini sana hapa, tangu Machi mwaka jana hakuna kibali kilichotoka cha mwekezaji kama sikosei au kama nakosea Mwenyezi Mungu anisamehe. Tokea Machi mwaka jana kuna vibali si chini ya saba kutoka *ZIPA* serikali hapa tuwe makini. Mchangiaji aliyepita Mhe. Miraji Khamis amezungumza tokea Machi, tokea kuundwa hiki kitengo *DCU* sijui kina mwaka gani, Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira siku moja keshasaini kibali cha mfanyabiashara Pemba keshakipeleka Kamisheni ya Ardhi kimekaa miezi mitatu au minne. Sitaki kumtaja kamisheni kama katibu mtendaji au nani hajakitoa, kesha saini waziri katibu mtendaji kimewekwa kwenye droo. Moja tuseme moja, mbili tuseme mbili, kavu tuseme kavu, mbichi tuseme mbichi, kweli tunataka kuwainua wawekezaji sisi?

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira nilimshukuru sana nikamwendea mwisho akawa mkali, yeye ilikuwa tayari aende mwenyewe. Sasa kweli tunamsaidia Mhe. Rais au tunamrudisha nyuma Mhe. Rais? Kamisheni ya Ardhi na Mazingira pana mashaka tena makubwa, kitengo kile serikali wakiangalie. Kuna vibali karibu saba kwa wawekezaji leo watu wanakosa ajira mwekezaji huyo tokea Machi, wafuatilie *ZIPA* kama haya maneno anayosema Mhe. Jaku Hashim ni ya kweli au uongo, mwekezaji anakimbia hawezi kuja kuwekeza uzalendo

unakuwa mwingi. Tokea kuundwa Machi, Aprili, Mei, Juni, Julai, Agosti, Septemba, Oktoba, Novemba karibu mwaka huu, kweli ndio hilo tatizo ninalosema huwa tunasema kwa mdomo vitendo havionekani.

Kitengo cha *ZIPA* kilifanya kazi kubwa kilipokuwa kiko peke yake katika ilani humu, kilipokuwa peke yake kilifanya kazi kubwa sijui miradi mingapi. Ukienda pale mradi haulali na ndio maana kilichomsaidia mkurugenzi kukaa zaidi ya miaka 30 au 25 sasa hivi kama sikosei au 15 kutokana na utendaji wake na timu yake.

Lakini leo *DCU* hii imekuwa tatizo kweli kweli Kamisheni wa Ardhi kuna matatizo Mhe. Mwenyekiti, lakini mwenyewe hayupo Mheshimiwa wa Ardhi hapa. Huku tunatafuta wawekezaji na wawekezaji wanasokotwa ilipokuwa mradi ule wanao wenyewe Mamlaka ya *ZIPA* kazi ilikuwa hailali.

Lakini leo mwaka mzima vibali karibu saba wawekezaji watawekeza wapi au tuna serikali tatu hapa Zanzibar, anachoamua huyu sicho anachamua huyu ndicho hatuwezi kwenda. *ZIPA* wamefanya kazi kubwa. Lakini changamoto ndio hizi kazizungumza Mhe. Miraji Khamis Mussa ingawa serikali imeanzisha kitengo cha kushughulikia vibali vya ujenzi kwa ajili ya usimamizi wa vibali vya ujezi nchini baada ya maombi ya wawekezaji wanachukuwa muda mrefu *ZIPA* wanalia tuwasiadieni serikali ndio imo ndani, hatuwezi kwenda hiyo miradi ndugu zetu watoto wetu wangepata kazi uchumi wa serikali ungekuwa lakini hakuna kitu.

Mhe. Mwenyekiti, nije kunako Sekta ya Biashara kidogo nigusie naomba ni-*declay interest* kidogo maana baada ya kutoka hapa pengine huko nje nitarudia kazi yangu hii ya biashara na kuna msemo unaosema "Usidharau dafu kwa embe ya msimu". Dafu

kwenye mnazi siku zote unaweza ukaipata lakini embe mwaka mpaka mwaka ndio izae. (*Makofi*)

Mhe. Mwanasheria Mkuu hapa kidogo tufafanulie kuna watu wanataka kuleta meli hapa ziko *ZMA* ripoti zao meli zinatoka nje zinakuja kusajiliwa hapa zinafanya safari kutoka Zanzibar Pemba, Mtwara, Mafia. Leo *ZMA* wanashindwa kutoa kibali wanasema tumezuiwa kutoa meli. Ninachojua mie meli zinazopepea bendera ya Tanzania nje ya nchi leo huyu muwekezaji keshafanya safari nafikiri leo au kesho anaenda zake Comoro kuekeza namjua anapanga safari kwenda Comoro kweli biashara tunataka ikuwe.

Meli inakuja hapa hapa isajiliwa hapa hapa kama *speed boat* inafanya ya mzunguko humu humu ndani leo mtu anaondoka anakwenda zake Comoro kuekeza tunakwenda wapi? Ile meli nilivyofahamu mimi kutokana na elimu yangu ndogo angalau ingekuwa inakwenda safari za nje Japan, Dubai, Iran ingekuwa mtihani haionekani, lakini katika bandari hii hii. Sijui tunakwenda au tunarudi mtihani wawekaji watakimbia kwa mtihani kama huu. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, nije kidogo kunako Wizara ya Kilimo. Mhe. Mwenyekiti, nimkumbushe tu Mhe. Waziri wa Kilimo tarehe 9/6/2016.....

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim Ayoub una dakika tatu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Heee! Mheshimiwa siwezi kushindana na kitu chako lakini niliweka *stop watch* mimi. Nimjulishe Mhe. Waziri wa Kilimo tarehe 9/6/2016 alisema maneno mazito katika chombo hichi naomba kuyanukuu:

Mhe. Spika, cha kwanza kuweza kujua tani gani tulizinazo tatizo la kwanza huku *focus* kwamba mwaka huu tunataka tuhakikishe

jambo fulani tumemaliza na tumefikia lengo fulani hatuko hivyo na ndio maana tukisoma bajeti utakuta hapa umepeleka shilingi kumi hapa ishirini hapa thalathini huoni *impact* tunataka tuone *impact.*

(1) Alisema Rais hatuna sababu kwa nini tuendelee kuagiza tani na thamani elfu za mchele hakuna sababu ya tani elfu nane mia tano kwa ajili ya *irrigation* kwa utalaamu waliotoa Dokta, hapa kwamba tunaweza tukatoa tani kumi na nne. Mimi mwenyewe Bagamoyo chini ya Magereza tulizalisha tani sana *point* tano mpunga kwenye hekta moja kwa mvumo huo mmoja. Hivyo, mawili tutapata tani tano tunapate tani saba tu zitatutosha.

Mhe. Spika, hivyo tukizungumza sekta ya mpunga tu pekee katika kipindi cha miezi sita Waheshimiwa nitawachukuwa mkatembee mkaone hali ilivyo mimi nilimwambia Mhe. Rais Mohammed Shein kama nilivyowahi kumwambia Rais Nyerere. Nilimwambia miezi sita Rais Nyerere kama sijailisha Magereza najiuzulu. Namwambia Rais Ali Mohammedd Shein ikifika miaka mitatu kama hatujazuia kuagiza mchele hapa bora tu nikuachie tu wizara yako aibu. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, hichi ni chombo miaka mitatu haijafika, kipindi kilichopita tulisokotana na Mhe. Juma Duni humu kuhusu *ICU* Wajumbe waliokuwepo kipindi hicho watakumbuka alitaka kujizulu humu ndani. Kiongozi anatakiwa awe kioo bado siku chache tu vyenginevyo Mhe. Waziri itabidi uje utueleze au uliombe Baraza hili, haya maneno tunayozungumza mengine tuweke akiba tusimalize yote kuzungumza chombo kizito ulichokiahidi hichi. Vyenginevyo itabidi uwajibike Mhe. Waziri. Haya maneno mazito yanaingia kwenye *hansard.* (*Makofi*)

Lakini kuna tatizo la mikarafuu nataka maelezo mashamba ya karafuu yamekodishwa kwa njia gani kule Pemba kwa mnada au

huyu yuko hivi au yuko hivi na atwambie Mhe. Waziri katika kitabu chake humu kuna mapato hayakupatikana waliokodishwa hawaonekani au imekuwa bee, wau, bee, ree imekuwa bure. (*Makofi*)

Mashamba haya ya mikarafuu waliokodishwa hawaonekani wako wapi serikali inatafuta mapato huku wanaondoka au ndio hiyo"bee" "wau" "ree" bure au ndio yamekodishwa kwa njia gani hata pesa ziondoke. Wakati huku mchanga umebanwa huko Pemba karafuu pesa hazionekani bilioni ngapi hazionekani. Pesa zimekwenda wapi? Au zimekwisha maana unamkodisha mtu humjui umpate wapi amekwenda wapi? anarudu lini? Serikali inataka kukusanya mapato. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Sasa naomba nimwite Mhe. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi atafuatiwa na Mhe. Hamza Hassan Juma na Mhe. Hamad Abdalla Rashid ajiandae.

Mhe. Dkt Makame Ali Ussi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii na mimi niwe mmoja kati ya wachangiaji wa mada hii tulinayo hivi sasa. Mada hii inayohusu wizara tatu.

1. Wizara ya Fedha na Mipango
2. Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko
3. Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi

Kwa kweli nampongeza alieunda kamati hii kwa sababu wizara zote hizi zinahusika na shughuli za uzalishaji kuuza na kununua pamoja na mambo mengine yanayohusiana na fedha.
Mhe. Mwenyekiti, nikianza uchangiaji wangu kwanza niingie kwenye ukurasa huu wa 4 ambapo hapa Wizara ya Fedha imeainisha mapato yaliyopatikana kwa kipindi cha Julai, Disemba

2017-2018. Ukiziangalia hizi takwimu utaona kwamba kuna ile sehemu ya bajeti iliyopangwa halafu kuna makadirio na kuna uhalisia wa kukusanya. Sasa ukiangalia ile nafasi baina ya *budget amount of money* na makadirio yaliyofanywa na uhalisia kidogo kuna tafauti kubwa sana.

Huwa najiuliza Wizara ya Fedha ndio iliyoleta utaratibu wa kufanya *Program Base Budget* ambayo hii kwa njia moja au nyengine inawezesha kupata bajeti ambayo haikingani sana na uhalisia. Sasa hapa kidogo napata utata kwamba kuna bajeti kubwa sana lakini mapato siku zote yanakuwa nusu wa bajeti yenyewe. Hapa kidogo tuje tupate maelezo.

Halafu tena kuna sehemu mbali mbali tumekusanya mapato lakini tukiangalia tena kuna gawio la *BOT* limekuwa *budgeted.* Lakini hakuna makadiro wala hakuna kilichopatikana kwa nini. Halafu pia kuna mashirika na mashirika nayo yamekuwa *budgeted* lakini kwenye hakuna makadirio wala hakuna kilichopatikana hakuna uhalisia. Sasa na hapa pia tupate maelezo.

Lakini pia tukienda chini kabisa huku kuna *(MVRI)* hakuna bajeti wala hakuna makadirio lakini kuna uhalisia imekujaje? Hivyo hivyo, kwenye *GBS* nayo hivyo hivyo kuna uhalisia lakini hakuna *budgeted* kuna budgeted lakini hakuna makadirio. Sasa ni kwa nini zimeingizwa hapa wakati ambapo hazitoi mchango wake kwenye makadirio wala mapato. Tukipata maelezo hapa kidogo tutaweza kujua ni kwa nini tutoe mapendekezo ya kufanya.

Tukitoka hapo sasa naenda kwenye Mamlaka ya Vitega Uchumi, *ZIPA*. Niipongeze sana *ZIPA* wanajitahidi sana lakini wamezitaja changamoto zao nne:-

1. Kuna watendaji wakuu wenye kauli tafauti ambayo inasababisha urasimu wa kutoa maamuzi ya kuwezesha mradi uliokusudiwa ufanyike.

2. Kuna ile *Development Control Unit* nayo haifanyi kazi ipasavyo hivyo vibali vinachelewa.

3. Uchakavu wa majengo ya maeneno huru wa Amani,

4. Ucheleweshaji wa utoaji wa vibali kwa wawekezaji unazorotesha na kuwavunja moyo.

Tunavyojua ni kwamba muwekezaji yoyote anakuja nchini anatumia fedha, fedha zake zile ingawa anazitumia lakini anataka ziwe salama aweke mradi ili uweze kupatikana ukimeleweshea unaanza kumvunja moyo na naweza akaahirisha kufanya *investment* ya aina yoyote.

Sasa mimi nashauri hapa hawa watendaji wakuu wanaohusika wote pamoja na hizi *control unit* na kadhalika. Nafikiri wangefanyiwa semina wakaelezwa umuhimu wa kuharakisha uwezeshaji wa kupatikana vibali kwa haraka. Najua lazima zifatwe taratibu kwa sababu wawekezaji wengine wanaweza kuwa na matatizo lazima kidogo urasimu uwepo lakini urasimu ukizidi mambo yanakuwa mabaya sana.

Nikitoka hapo naingia kwenye Wizara ya Biashara kwa sababu muda ni mfupi sitasema sana kwa maana nitapoteza muda wangu mwingi wakati mambo mengi yameleezwa vizuri sana humu. Tukiingia kwenye Wizara ya Biashara tunasema kwamba biashara yoyote ya kununua na kuuza inategemeana sana na uhalisia wa soko yaani *market forces*. Sasa kama *market forces* za dunia zinasababisha bei ziwe za juu, bei hapa nchini zitakuwa za juu,

lakini mara nyingi sana bei zinazopatikana nje zinakuwa si za juu kama zinazouzwa hapa.

Kwa hiyo, mimi nadhani kuna haja ya kuwa na chombo cha kudhibiti najua kipo lakini kiimarishwe. Chombo cha kudhibiti wafanyabiashara wanaoleta vitu kutoka nje ili wasiwaumize sana wananchi. Kuna mafuta nayo hatuyajui, yale mafuta ni *super* ama ni *ordinary* au nini mafuta mara yamekuja ya njano, mara yamekuja mekundu mara yamekuja kijani hatujui. Haya magari najua mashine, mashine zozote zile zinakuja na *recommendation* ama utumie *super* au utumie *ordinary* . Ukilazimisha kutumia mafuta yaliyopakwa rangi kama haya, tunayotumia sisi hapa ambayo pengine kiwango chake pengine ni *super* au ni nanihii unaweza ukayaingiza kwenye mashine ambayo haistahiki na mafuta yale, matokeo yake ni hasara za kuharibikiwa mara kwa mara umasikini unarudi pale pale. Kwa hivyo, pia naomba wizara husika iangalie suala hili la uletaji wa mafuta kama kuna mafuta ya aina tatu basi yaletwe mafuta ya aina tatu yatumike kwa mujibu wa mahitaji ya gari mtu aliyoleta.

Kwa upande wa Wizara ya Biashara,Viwanda na Masoko, nadhani mimi niishie hapo isipokua naiomba sana Wizara ya Biashara,Viwanda na Masoko kwa sababu sisi tunaishi kwenye nchi ambayo tunategemeana na wenzetu wa nchi za nje. Matokeo ya matatizo maafa mbali mbali yanatokea mahala popote, itakapokuja kutokezea upungufu wa uzalishaji basi sisi hapa tuwe na akiba yetu hakuna ghala linaloweza kumaliza kama hakuna vitu vinavyoweza kuletwa hapa hakuna ghala linaloweza kumaliza hata miezi sita sidhani kama lipo ghala hilo.

Mimi nashauri Wizara ya Biashara,Viwanda na Masoko, Wizara ya Fedha na Mipango, na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuzi, zishirikiane lijengwe ghala kubwa liweze kuwekwa vyakala au bidhaa ambazo zinaweza kutuchukua angalau miezi

sita pindi huko duniani yakitokea maafa ikawa vitu vile havipatakani.

Nakwenda zangu sasa Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi. Nitakwenda moja kwa moja kwenye hizi Taasisi za ukodishaji wenzengu wamelalamika sana kwamba watu wametangaziwa wajitayarishe kwa mambo fulani fulani na wakienda kama wamekubali lakini matokeo yake wamekwenda kinyume kwamba hawakumaliza madeni. Mimi nasema nadhani iko haja ya kuziita zile kamati maana zimeunda wizara tatu nadhani, basi zile wizara tatu zikutane zikae zifanye mikakati ya kuzidai hizo fedha na kuandaa mikakati ambayo itawezesha matokeo kama haya yasitokee tena kama walivyosema wenzangu. Sitaki kuchangia tena zaidi sana muda mfupi, nakwenda kwenye misitu.

Misitu ni jambo la muhimu sana, ni kitu muhimu sana misitu ndiyo inayoleta mvua nchini, bila ya misitu ni jangwa inasemekana hata huko Arabuni zamani kabisa kulikuwa na misitu mikubwa sana lakini ikakatwa katwa ikasafirishwa Ulaya sasa hivi majangwa kule hakukaliki ni jangwa tu, huwezi kupanda kitu kikaota mpaka ukiwekee mazingira maalumu ndio kiote.

Kwa hivyo, nasema kwamba misitu yetu lazima tuilinde msitu wa Kiwengwa uliobaki huu tunastahiki kuulinda sana inasemekana historia ya Zanzibar, msitu umetoka Jozani huko na mbele Kusini ukaingia Kiwengwa ukaenda zake mpaka Nungwi kote huko kulikuwa na Mikwe sijui miti gani ya asili na miti mengine mengine, sasa hivi kote kumekatwa kweupe kumebakia Kiwengwa kipande kidogo sana.

Kwa hivyo, mimi naiomba sana Wizara ya Kilimo ijitahidi sana kuutunza msitu huu uliobakia pamoja na Jozani angalu tusije tukakosa mvua kabisa kabisa. Sisemi kwamba na misitu mengine

isihudumiwe lakini misitu yote ihudumiwe tusije tukakubwa na majanga ya jangwa kama walivyokubwa wenzetu huko.

Sasa nakwenda kwenye maendeleo ya kilimo, miaka sasa hamsini au tuseme mingi zaidi ya hamsini hata elfu Zanzibar haijaweza kujitosheleza kwa chakula kwa muda wote huu. Ingawa jitihada mbali mbali zinafanywa lakini bado hatujaweza kujitosheleza kwa chakula, tunalima mihogo, tunalima ndizi, migomba hiyo, tunalima vyakula mbali mbali ikiwemo mipunga lakini bado hatujajitosheleza kwa chakula. Hili ni tatizo wakati tunaisifu sana nchi yetu ina rutuba, sasa nasema kilimo chochote hakiendi bila ya kuwa na elimu ya ugani *extension*, bila ya kuwa na utafiti *research* tena na mambo mengine ya *administration* na kadhalika, haya ni mambo ya kawaida ambayo yanawezesha mambo haya yafanyike.

Mhe. Mwenyekiti, sasa kwenye *extension* inabidi ni lazima tujuwe kwamba *extension* inatokezea kwenye maendeleo, yaani ni muhimu kwa maendeleo ya uzalishaji, bila ya *extension* hatuwezi kufanya kitu. Najua huko kuna mabwana shamba vijijini, kuna mabwana shamba kila pahala na wanafanyakazi zao vizuri zaidi, lakini bado matatizo ya uzalishaji yapo.

Kwa hivyo, nashauri sana Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi tufanyeni kila njia tufanye utaratibu ule ambao umefanywa na nchi za wenzetu, utaratibu wa kuwafikishia wakulima huko waliko taaluma zinazohitajika. Tunaweza kuwafikishia taaluma zinazohitajika kwa kuandaa programu maalum ambayo tunaweza tukafanya *demonstration* huko huko kwa wakulima mashamba ya maonesho. Najua yanafanywa lakini tuya-*modify* yawe mashamba ya maonesho mazuri sana.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nasifu Makunduchi. Makunduchi nafikiri kwa Unguja na Pemba ni ya kwanza inayozalisha ndizi kubwa na

nzuri. Tunawapongeza sana wanajitahidi kwa kulima. Lakini maeneo mengine ukienda ukinunua ndizi ya mtwike basi hiki kidole changu ni kikubwa, kwa kweli ule sio uzalishaji mzuri wakati kuna wataalamu wengi wapo na bado matatizo haya yanatokezea.

Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba tuanzishe hizo *demonstration plot* huko kwa wakulima ili waone sehemu inayowekewa mbolea inakuwaje, sehemu ambayo haina mbolea inakuwaje na sehemu iliyopaliliwa inakuwaje. Sasa mkulima anavutika kwa kuona yale ambayo yanafanyika pale. Pia tuanzishe...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, una dakika mbili.

Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi: Dakika zimekwisha, sawa nitajitahidi sasa nimalizie. Pia tuanzishe tunaita *farm service centre*, yaani maduka ambayo kwa kweli huko vijijini wakulima wanaweza kwenda kujinunulia mbolea kwa idadi wanayotaka. Kuna wengine hawataki *packet* moja ya mbolea, wanataka kilo moja, kwa nini tusiwawekee kilo moja ya mbolea wakanunua wakenda kufanyia hata bustani au kitu chengine. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, halafu tena nashauri ifanyike *research*. Sasa hivi matumizi ya mbolea yanafanywa tu, yaani tumia mbolea gunia moja la *ammonia*, tumia gania la pili la *potassium* na nusu gunia ya *phosphorus* na *potassium* nusu gunia. Hii sio *recommendation* nzuri, nadhani ufanyike utafiti. *Soil analysis* ijulikane, hapa panahitaji *ammonia* kiasi gani, hapa pahahitaji *phosphorus* kiasi gani, hapa panahitaji *potassium* kiasi, kwa njia hizo ndipo tunaweza tukazalisha mazao mengi. Bila ya kutumia taaluma za namna hiyo siku zote tutakuwa hatufanikishi, kwa sababu uki-*overdose* kwenye mbolea hupati mazao bora, uki-*under dose* hupati mazao bora, ni lazima utumie kiwango ambacho kinatakiwa kwa mujibu wa mahitaji ya udongo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo na kwa sababu hii ni wizara adhimu tungeichangia sana, lakini muda umekwisha. Nakushukuru kwa kunipa nafasi na nawapongeza sana wizara hizi ambazo kamati hii imezifanyia kazi, kwa kweli kitabu kinaonesha wanafanyakazi nzuri kwa hivyo waendeleze bidii hiyo.

Kwa hivyo, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi. Sasa naomba nimwite Mhe. Hamza Hassan Juma, akifuatiwa na Mhe. Hamad Abdalla Rashid na Mhe. Ibrahima Makungu ajiandae. Waheshimiwa Wajumbe, ni dakika kumi tu.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia ripoti wizara tatu kwa dakika kumi, kila wizara dakika tatu. Mhe. Mwenyekiti, hunitendei haki lakini nitajitahidi kujibanabana ili niweze kutoa mchango wangu.

Kwanza nataka nianze na lililosemwa na wengi, kwa sababu suala hili isiwe hapa Barazani tunakuja tunaropokwa tu jambo ambalo linahusu uchumi wa nchi ni lazima tulifanyie kazi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, suala la waliokodishwa mashamba ya karafuu, karafuu waliovuna pesa zetu hawajaleta. Mimi nataka niseme hawa hawakukodishwa, hawa inaonesha kama waligaiwa, sasa mashamba haya yanakodishwa. Mimi ninashauri Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako kwamba Baraza liunde kamati maalum ya kwenda kuwachunguza hawa waliopewa haya mashamba na wakakodisha karafuu, wakaziuza na sijui kama wameziuza *ZSTC* waziri atakapokuja kutoa jawabu atatuambia, kwamba hizi karafuu walizokodishwa je waliziuza *ZSTC* na kwa nini wakawa hawakulipa serikalini. Sasa Mhe. Mwenyekiti, hilo

naanza la kwako uhakikishe kwamba unachukua hatua ili fedha hizi zirejeshwe mara moja. Vile vile ule ushauri ambao wameutoa waheshimiwa kwamba wale ambao wanayahudumia yale mashamba wale waliokuwepo karibu, mimi nadhani kwa mara nyengine wangepewa kipaumbele kadhia hii isingeweza kutokea.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nianze moja kwa moja katika ripoti hii ya kamati naunga mkono kama walivyosema wenzangu ripoti hii ya kamati, alianza hapa mwenyekiti kwa namna alivyoisifu Wizara ya Fedha na Mipango kwa kuweza kukusanya mapato vizuri. Mimi nimefurahi zaidi kwamba katika takwimu yale mapato ya ndani kwa kweli yameweza kukusanywa vizuri na hii, kwa sababu nimejaribu kuangalia kwenye asilimia pale,wamefika karibu asilimia 67 ambapo mapato ya sehemu nyengine yoyote hayakuweza kufikia hatua hiyo.

Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kuendelea kuwapa vipaumbele wafanyabiashara wazalendo, ili kuhakikisha kwamba wanachangia katika uchumi wa nchi kama ilivyoonesha katika jadweli hili.

Mhe. Mwenyekiti, nakuja katika Kitengo cha *ZIPA*. Mhe. Mwenyekiti, mimi naendelea kusema kwamba *ZIPA* tunaizungumzia kwamba iwe ni *one stop centre*, sasa hivi huu ni mwaka wa kumi. Kila siku tunaambiwa kunafanyika maboresho ya *one stop centre*. Waziri wa Fedha na Mipango wa awamu iliyopita Mhe. Omar Yussu Mzee, alipokuwa akifanya majumuisho ya bajeti kuu ya serikali, alijaribu kuwaita wale wajumbe wa ile Bodi ya *ZIPA* aliwaita juu pale, na akasema safari hii tumeunda *strong* timu, makatibu wakuu wao ndio wenye kauli za mwisho lakini leo kamati inarudi tena inaishauri *ZIPA* kwamba kuwe na *one stop centre*.

Kwa hivyo, mimi nadhani kitu ambacho nakiomba kwanza Mkurugenzi Mkuu mwenyewe wa *ZIPA* awe na mashirikiano na wakurugenzi wenzake. Hapa inaonesha Mhe. Mwenyekiti, kuna bifu, kila mmoja kwa kuwa kateuliwa na Rais anaonesha ubavu wake, matokeo yake miradi inakwama na mambo hayaendi. Kwa hivyo, mimi naomba kila mmoja awajibike kwa nafasi yake ili tuweze kufaidika na uchumi wa nchi.

Mhe. Mwenyekiti, kama wenzangu wanavyozungumza leo vibali unaambiwa mara ardhi, ukenda ardhi wanakuambia *ZIPA*, yaani kila mmoja hajulikani nani hasa anayehusika. Kwa hivyo, tunataka kwamba vibali vitoke ili uwekezaji uwepo wa kutosha.

Mhe. Mwenyekiti, katika ripoti yetu tutakuja kuelezea namna gani serikali kwa kupitia Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira ilivyopokea wito wa Baraza kuhusu kufuta yale maeneo ambayo hayajawekezwa kwa muda mrefu. Sasa mimi nashauri kwa sababu masuala ya uwekezaji yanahusu *ZIPA*, ardhi wao kazi yao kutoa *lease*. Kwa hivyo, naomba sana yale maeneo ambayo yaliyorudi serikalini yasiendelee kukaa matupu, wawekezaji bado wapo wanahitaji ardhi ya kuwekeza ili tuweze kupata ajira tuwaondowe vijana wetu mitaani waende wakajitafutie riziki.

Kwa hivyo, naomba sana hayo maeneo ambayo tayari serikali imeshayarejesha serikalini, basi wapewe wawekezaji ambao wako *serious* waweze kuwekeza. Bado natoa wito wale ambao mpaka leo bado maeneo hawajayaendeleza serikali iharakishe kuweza kuyarejesha serikalini.

Mhe. Mwenyekiti, nakuja katika ukurasa huu huu wa tano unaozungumzia *ZIPA*. Kwa kweli mimi nasikitika sana katika changamoto, maoni na maagizo ya kamati. Hapa katika hii *column* namba 4 wanasema, *ZIPA* ihakikishe inakamilisha *master plan* ya Micheweni ili wawekezaji waweze kuitumia. Leo *master*

plan maeneo ya uwekezaji yametangazwa tangu mwaka 1992/1995, tokea awamu ya tano mpaka leo hakuna *master plan*. Kama hakuna *master plan* utegemee mwekezaji atakayekuja, mwekezaji gani. Kwa hivyo, mimi naomba sana *ZIPA* wajitahidi na hili Mhe. Mwenyekiti, naomba ulisimamie ili tutakapokuja kwenye bajeti tuhakikishe kwamba ile programu ya *master plan* iweze kupatikana.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, nakuja hapo hapo *ZIPA*. Mimi naomba sana *ZIPA* wawe waadilifu na wawe wakweli, wasiwe kila siku wanatuambia maneno ambayo hayatekelezeki. Sisi huu muhimili wa Baraza la Wawakilishi, tuliomba eneo kwa muda mrefu. Tuliwahi kupewa eneo na Rais mstaafu Dkt. Salmin Amour Fumba kule, eneo letu walimpa mtu mwengine matokeo yake mpaka leo hawajatupa eneo letu, kila siku wanatupiga danadana kesho sijui keshokutwa sijui ipo kwenye kamati.

Mhe. Mwenyekiti, juzi Mhe. Simai alisema kwamba tunatakiwa sisi tuwe na Baraza la Wawakilishi la *modern* la kisasa lenye *equipment* zote kila kitu. Tunatakiwa tuwe na majengo yetu *hostel* zetu. Waheshimiwa Wajumbe wengine wanatoka Pemba wanakodi mitaani sio vizuri, tunatakiwa tuwe na *hostel* zetu, tuwe na *gym* yetu ya kufanyia mazoezi na vile vile kuwepo na *swimming pool*, ambapo waheshimiwa wanaopata matatizo ya viungo waweze kufanya mazoezi katika eneo lile. Sasa mpaka leo *ZIPA* wanatupiga danadana. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba sana suala hili tumeshalizungumza sana, hivyo nawaomba sana *ZIPA* wawe wakweli katika kauli zao wasiendelee kutubabaisha.

Mhe. Mwenyekiti, nakwenda haraka haraka nakuja katika jengo la Chawal pale Darajani. Mimi nawapongeza sana *ZSSF* kwa miradi ambayo wanaifanya, lakini nawaomba sasa hivi wawekeze katika miradi ambayo itakuwa inazungusha fedha kwa haraka. Leo

tunajenga jengo la Chawal *building* pale Darajani, jengo la treni. Lakini tatizo kamati imezungumza, tutakuwa tuna tatizo la *parking*, kwa sababu pale milango ya biashara imeongezeka, *parking* hatuna. Leo tuna ile Darajani *Corridor, why* tusiitumie ile kwa kujenga *parking ZSSF*. Naomba sana Mhe. Mwenyekiti, na watu tutawashauri vile vile na wenzetu watu wa mipango mji, lile eneo la Darajani tena *parking* pamekaa vizuri, lakini *parking* yenyewe ni ya kawaida tunataka *parking* za kisasa, *parking* ya ghorofa. Inaanza *flow* ya chini, ya kwanza, ya pili, ya tatu, ya nne mpaka ya sita, *ZSSF* pale wataweza kurejesha pesa zao kuliko miradi mingine ambayo wanaifanya, kwa hivyo naomba hili.

Mhe. Mwenyekiti, lakini hapa kuna changamoto imeelezwa kwamba mradi ule wa Darajani gharama zimeongezeka kutokana na masharti ya Mjini Mkongwe, suala hili naomba tena. Mhe. Mwenyekiti, mimi kamati yangu inasimamia taasisi ya Mamlaka ya Mji Mkongwe, tatizo linalojitokeza kuna baadhi ya taasisi wakishakuwa na miradi yao, wanaanza ku-*design* wanapanga kila kitu bila ya kuwashirikisha Mamlaka ya Mji Mkongwe, sasa kule kuna taratibu zake. Matokeo yake wakati wa kutekeleza ule mradi Mji Mkongwe wakija kuwapa zile taratibu, ndio pale inaonekana Mji Mkongwe wana usumbufu, lakini Mji Mkongwe wanalinda masharti ya Urithi wa Kimataifa, naomba lazima watendaji tuweze kushirikiana. Kwa hivyo, hii ndio changamoto iliyojitokeza, lakini naamini sasa hivi kamati yetu pia ilifuatilia nafikiri mambo yanakwenda vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, *ZSSF* wanatunyanyasa. Bodi yangu ya wakandarasi pamoja na Mamlaka ya Wakala wa Majengo wametubomolea jengo letu la idara pale Michenzani hawajatulipa hata shilingi moja. Leo wametuazima jengo Kilimani kila siku sokosoko wanataka kutuhamisha. Mimi katika ripoti yangu nimeandika Wakala wa Majengo asihame katika jengo la *ZSSF* mpaka watulipe fidia tuweze kujenga jengo letu, serikali imesema

huwezi kumuhamisha mtu bila ya kumlipa fidia. Sasa leo wanawahangaisha watu wetu Wakala wa Majengo, bado nawaambia ZSSF najua Mkurugenzi yupo, Wakala wa Majengo pale hahami mpaka muhakikishe kwamba anapata eneo la kuweza kufanya kazi, vyenginevyo murudishe jengo lake ambalo mlilolibomoa.

Mhe. Mwenyekiti, nakwenda haraka usije ukanipigia kengele. Kamati hapa imezungumzia suala la Tume ya Mipango. Mimi kwa kweli nawapongeza sana hii tume, naomba tuwape mashirikiano taasisi zote za serikali tunapokuwa na miradi yetu mikubwa Tume ya Mipango ile ndio *simtank* sasa hivi ya taifa. Kwa sababu tuna uzoefu huko nyuma miradi yote inayokuja, akija kiongozi huyu anafanya miradi hii akiondoka anakuja na mambo mengine, lakini hii Tume ya Mipango ndio inakuja sasa kusimamia mipango ya kitaifa.

Kwa hivyo, kitu ambacho nakiomba Mhe. Mwenyekiti, Tume ya Mipango kuna eneo ambalo limepangwa kuendelezwa Mangapwani. Mhe.Mwenyekiti, naomba sana pale kuna uwekezaji wa aina tofauti, uwekezaji wa Sekta ya Mafuta na Gesi, wawekezaji waliokuwepo pale ambao tayari wameshapata *lease*, wameshaanza kulalamika wanataka kuanza miradi yao tayari wamesimamishwa. Mimi kusimamishwa nimefurahi, kwa sababu haiwezekani eneo lile kila mmoja akaja na mradi wake ambao hauko katika mipango mkuu ya serikali. Kitu ambacho nakiomba Tume ya Mipango wawatafute wale wawekezaji wa pale, lakini vile vile wakae pamoja na wawekezaji waliokuwepo hapa Mtoni kwenye *storage tank* ya mafuta, kwa sababu wanaambiwa watahama watahamia Mangapwani, lakini wao mpaka sasa hivi unapowauliza hawajapewa hata *site* ya kujenga. Wawekezaji hawa kama mtakaa nao Tume ya Mipango, wana mipango mzuri na wana *idea* nzuri, mnaweza mkashirikiana wakatoa fedha wao

pengine nyengine wakatoa serikali kwa njia ya PPP tukaweza kupata miradi pale ambayo itaweza kusaidia.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mfano mimi kama ningeshauriwa kuhusu kununua meli ya mafuta. Mimi ningesema serikali ile pesa iliyotoa kwa ununuzi wa meli ya mafuta wangesubiri kwanza. Pesa ile ingetumika kwa kujenga miundombinu ya mafuta kule Mangapwani ili tuwe na *storage tank* ya kutosha. Leo tunanunua meli ya mafuta, meli ya mafuta ikishakamilika kujengwa haiwezi kuingia kwenye Bandari ya Mtoni kutokana na kina kidogo cha maji. Sasa mimi naomba sana serikali kwa kupitia Tume ya Mipango ielekeze nguvu zote eneo la Mangapwani, ili pale zijengwe *storage tank* za kutosha tuweze kupata mafuta ndani ya nchi, lakini vile vile mengine yaweze kupatikana.

Mhe. Mwenyekiti, hapa kumeelezwa changamoto. Tume ya Mipango ya Zanzibar hawapati mashirikiano na Tume ya Mipango ya Tanzania Bara. Mimi nawaombeni shughulikieni ya kwenu, mkitaka lazima mpate mashirikiano watakusumbuweni kwa muda mrefu. Kwa hivyo, shughulikieni ya kwenu tuna mipango mingi ambayo ya miradi ambayo Zanzibar tunaweza tukajitosheleza na hayo mengine jitahidini hivyo hivyo, lakini kwa kweli isiwarejeshe nyuma.

Nakuja suala la Benki Kuu. Mhe. Mwenyekiti, kamati hapa imeeleza *BOT* waje kutoa elimu kwa wananchi. Mimi nakushauri mwenyekiti, utakapoanza kamati panga ziara ya kwenda *BOT* Makao Makuu, sio *BOT* Zanzibar. Nenda *BOT* Makao Makuu mwambie *Governor* aje Baraza la Wawakilishi kutoa semina. Mimi naamini humu wajumbe wengi wa Baraza la Wawakilishi hawajui hasa majukumu ya *BOT*, sasa waje hapa wale *BOT* ukiangalia kwenye sheria yao inasema wao kazi yao ku-*facilitate* biashara na uwekezaji ili uweze kukua ndani ya nchi. Sasa tujiulize *BOT* anasaidia nini ukiacha gawio lile la 4.5 ambalo

tunalipata Zanzibar, wanawasaidia nini wawekezaji wa Zanzibar, hakuna *is nothing*. Leo Bara wanasaidia mpaka sio mikopo mpaka misaada, wamewahi kutoa mpaka bilioni moja moja kwa taasisi. Leo hapa Zanzibar hakuna hata *single cent* iliyotoka.

Kwa hivyo, naomba Mhe. Mwenyekiti, mtafute *Governor* wa *BOT* aje Baraza la Wawakilishi tumwambie maneno yake, ili tuhakikishe kwamba *BOT* inaweza kufanikishwa na wawekezaji kwa upande wa Zanzibar. Lakini sio *BOT* peke yake mpaka *TRA* naomba uwaite hapa, hicho kipindi cha nyuma ndio tulikuwa tunafanyakazi nao kwa pamoja.

Mhe. Mwenyekiti, najua unaniambia bado dakika zangu tano namaliza haraka. Nakuja *PBZ*. Mhe. Mwenyekiti, *PBZ* mimi naomba nichanganye na swahib wangu wa Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi. *PBZ* sasa hivi kama unataka siku hiyo watoto wasile nyumbani basi nenda kaweke pesa *PBZ*, kuanzia saa 2 mpaka saa 7. Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi kuna mambo ya kitaalamu, hebu tutafutieni mashine za *EFD*. Wenzetu Bara unaambiwa mashine ile ukiingiza tu tayari mpaka *TRA* wanajua kodi yao kiasi gani imepatikana na hizi mashine za *EFD*, naomba sana na kule kwa swahib wangu Mhe. Hamad Rashid kwenye mashimo ya mchanga tuwekewe kule ili kuhakikisha kwamba mapato ya serikali yanapatikana na ukwepaji usiweze kupatikana.

Lakini hili nataka kidogo kumpa changamoto Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi

Mhe. Mwenyekiti: Malizia Mhe. Mjumbe.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Haya. Nampa changamoto Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, kipindi cha nyuma aliwahi kuyakamata magari ya mchanga ambapo vijana wake

wale wali-*forge* risiti, sasa hivi huenda ukaja ukakamata tena kwa sababu watu wanakimbia foleni kwenda *PBZ* kulipa, matokeo yake kuna watu wamekuwa kama ma-*agent* wanakata risiti halafu wanauza kule wanatoa kamisheni ya shilingi 5,000/-. Sasa leo risiti zile kama ziko sawa ni sawa. Je, risiti zile zikija zikifojiwa itakuwa tatizo jengine, *the only solution* mimi nafikiri ipatikane *EFD* mashine pale utaweza kukusanya kodi yako.

Mhe. Mwenyekiti, nawaomba kamati wayachukuwe haya moja kwa moja mambo matatu tu. Naomba kamati ikirudi kwenye kamati waende wakaangalie maghala ya *ZSTC* yako mangapi Unguja na Pemba. Vile vile waangalie majengo ambayo yaliyotolewa, maana yake sijui kama yaliuzwa watu waligaiwa, majengo yaliyokuwa ya Wizara ya Viwanda yako mengi kuna viwanda vilivyokuwa vya usumba, wayafuatilie waangalie mikataba kwa sababu ninahisi kidogo kuna ubabaishaji kama hauko vizuri.

Lakini vile vile Mhe. Mwenyekiti waangalie suala la mashamba ya mipira shamba la mipira watu wanavuna, lakini sijui angalau Serikali kama inapata kitu chochote.

La mwisho kabisa Mfuko wa Jimbo, Mhe. Mwnyekiti, leo tunakaribia tunakwenda kwenye bajeti mfuko wa jimbo hatujapata, leo Wizara ya Fedha wanataka eti sisi badala ya kuwasimia wao Serikali wanataka kutusimamia sisi, wanasema aa hatukupeni pesa mpaka mrejeshe *return.* Sasa *CAG* ana kazi gani, sasa kazi ya *CAG* anataka kuifanya Waziri wa Fedha. Tupeni pesa za mfuko wa jimbo msizuie maendeleo katika maeneo yetu, leo Mheshimiwa Mwenyekiti, wabunge wameshapewa zaidi ya milioni hamsini wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tokea tulipopewa milioni ishirini mpaka leo taaban mpaka wengine tunaambiwa tushazila, tunakwambieni wananchi pesa hatujapata

na tukipata tutakuja mtaona shughuli za maendeleo Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

Mhe. Mwenyekiti: Nakushukuru Mhe. Hamza Hassan Juma kwa mchango wako sasa naomba nimuite Mhe. Hamad Abdalla Rashid na Mheshimiwa Ibrahim Makungu na Mhe. Rashid Makame Shamsi kwa leo atakuwa mchangiaji wetu wa mwisho nae ajiandae.

Mhe. Hamad Abdalla Rashid: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi ndogo ya kuchangia hotuba hii ya kamati ya Fedha biashara na Kilimo, kwanza kama wenzangu walivyotangulia kuwapongeza wenzetu na mimi niwapongeze Mawaziri wote watatu kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuendeleza nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze na *ZRB* kwanza niwapongeze kwa kazi kubwa wanayoifanya ya makusanyo ya mapato ambayo leo hii hata Waziri mwenyewe anatamba namna gani Serikali inapata mapato au mapato yalivyoongezeka, lakini nina ombi maalum kwa ndugu zetu wa *ZRB* pamoja na Waziri mwenyewe. Mhe. Mwenyekiti, ni jambo zuri kuweza kuongezeka katika ukusanyaji wa mapato lakini nawaombea ndugu zangu madereva naiomba *ZRB* pamoja na waziri wazingatie hili na nitatoa vigezo maalum wavielewe. *ZRB* hapo mwanzo ilikuwa *TRA* inakusanya mapato ya magari sasa hivi imekuja *ZRB* na ilikuwa ni 110,000/= Lakini ndugu zetu madereva sasa hivi wamepandishiwa ile kutoka 110,000/= mpaka laki sita kwa basi, laki tano kwa daladala za mbao.

Mhe. Mwanyekiti, ni pandisho kubwa ambalo ukizingatia na natoa mfano hasa bei ya mafuta inapandishwa kwa mwaka zaidi ya mara tatu au nne, lakini huu unafika mwaka wa kumi daladala haijapandishwa nauli sasa basi ukizingatia kule Pemba daladala

hizi zinafanyakazi nusu mwaka na zinafanya hivyo kwa sababu ni nyingi zikitoka kwa siku moja haziwezi kupata kipato cha kutosha pale. Sasa haidhuru Serikali tunataka mapato lakini tuangalie na wafanya biashara wetu kwa sababu wao ndio wanaotoa hayo mapato yenyewe tunawafanya vipi au tunawasaidia vipi katika yale malipo.

Mimi naomba kwa sababu wanafanyakazi nusu mwaka ni kwa nini *ZRB* na Wizara ya Fedha isiwatoze bima ya nusu mwaka na ile *ZRB* ya nusu mwaka, ukizingatia hata upakiaji wa abiria katika zile gari zao wenzetu kule bara hakuna tatizo kupakia abiria mpaka wakasimama, kwetu sisi basi zima unaruhusiwa kupakia watu ishirini na sita tu. Sasa bado mapato wanakuwa hawayapati na ndugu zetu hawa ikiwa tunang'ang'ania hapa bila ya kuwasaidia itafika hadi watashindwa kufanya biashara ile na wananchi kuna hatari ya kuja kukosa usafiri wa kwenda zao katika majukumu yao ya kazi.

Mhe. Mwenyekiti, naiomba sana ZRB izingatie na nashukuru wenzetu wale wamepeleka maombi wayazingatie na waweze kuwasaidia, kwa mfano magari ya *Private hire*, magari ya mizigo imekuwa ni chachafyo kubwa na mimi naomba kabisa kwa moyo mkunjufu tusikilize maombi ya wenzetu wale ili tuweze kuwasaidia angalau basi kuwateremshia kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo mimi nakuja kwenye suala la uchumaji wa karafuu wenzangu waliotangulia wamesema sana kuhusu watoto na namna gani wachume karafuu. Mimi naunga mkono Wizara na Serikali hasa kwa kukataza watoto wadogo kuchuma karafuu. Nina sababu maalum Tanzania ni nchi ambayo imejiunga katika Jumuiya za Kimataifa na kuna haki za mtoto, niwakumbushe wenzangu tusing'ang'anie vitangi tu na wale wanaoharibu watoto wadogo, lakini bado kuna haja ya kuzuia watoto wetu wasichezee ile miti kuchuma karafuu ni hatari.

Lakini kwenye jumuiya za kimataifa kuna haki ya mtoto uchumaji wa karafuu ni ajira jumiya za Kimataifa haziruhusu mtoto kuajiriwa, inakuwaje leo tunazunguka aidha tujitoe basi kwenye Jumuiya za Kitaifa turuhusu watoto wetu waachume mkarafuu, lakini tusiwe wakali kwa vitangi tukakubali kuruhusu watoto wetu wachume karafuu wakati nchi yetu imejiunga kwenye haki za mtoto, tutamkosesha mtoto kusoma akenda kuchuma karafuu, tutamkosesha haki yake nzuri ya afya. Kwa sababu sheria ya Z*STC* haimlipi mtoto chini ya miaka kumi na nane pale atakapopata ajali ya kuanguka mkarafuu, sheria hasa ya Zanzibar hairuhusu hivyo. Leo tukawaruhusu watoto wetu hawa kuchuma karafuu akipata athari kule matibabu huku hapati kwa sababu haki yake tumeiondoa kule, tumemtoa kwenye masomo tumempeleka kwenda kuchuma karafuu tunaomba skuli zifungwe, lakini hatuoni kama skuli zikifungwa tunakosesha mtoto wetu haki yake ya kimataifa, haki yake ya kimataifa ya kupata afya. Mimi naomba bado tuendelee na katazo hili kwa kumlinda mtoto wetu kumuweka na afya nzuri mtoto wetu, lakini kupata haki zake zote za kimataifa.

Mhe. Mwenyekiti, nije sasa kwenye michango mimi nakuomba tafadhali kuna lugha mbaya zinatumika hapa kiundani na mimi niseme uwazi hasa Mhe. Jaku kazidi sasa si vizuri kukebeheana humu ndani kwa asili ya mtu, yansoza yammaliza maana yake nini asimkebehi Mhe. Waziri si kitu kizuri nilichelewa pale kumpiga kanuni, kanuni kifungu cha 59 kinasema wazi ni marufuku Mjumbe yoyote kumfanyia kazi au kutoa maneno ya matusi kwenye Baraza bee,wau, ree kwenye kamusi la kiswahili ni tusi kubwa. Namuomba Mhe. Jaku sisi Wapemba tunajua kusema kihindi, tunajua kusema Kimakunduchi hili ni Baraza lenye heshima alinde heshima za wengine si vyema kumkebehi kwa asili yake, anamkebehi Mhe. Waziri na Rais mpemba naende basi akamwambie Rais basi yansoza yammaliza, atakuja

kumdhalilisha Rais mbele ya umma kazidi na mimi namuomba aje chini kidogo apunguze, Baraza la kutunga sheria lina heshima zake hatukuja kukebehiyana kwa asili hapana.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sitaki kuchukua dakika zako hizi tano zinanitosha naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia naomba tuendelee. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Hamada Abdalla Rashid, sasa naomba nimuite Mhe. Ibrahim Makungu atafuatiwa na Mhe. Rashid Makame Shamsi.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu jioni hii kufika hapa kwenye Baraza tukufu kuchangia tukiwa na afya njema, lakini Mwenyekiti, nikushukuru kunipa nafasi hii kuchangia ripoti hii ya Kamati ya Fedha, Biashara, Kilimo ya Baraza la Wawakilishi.

Lakini kwanza niwapongeze Mawaziri wote watatu kwa kazi zao nzuri sana na zinaonekana kwa hivyo niwapongeza sana, pia nimpongeze Mwenyekiti wa kamati kwa ripoti yao nzuri na Wajumbe wao wote walioleta ripoti hii.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze ukurasa huu wa kumi na tatu nianze kwanza kuipongeza Serikali kwa juhudi zake kubwa kukuza Idara ya Biashara na ukuzaji wa masoko mimi nipongeze sana kuanzia Rais kwa juhudi zake kubwa alieanzisha kuhakikisha masoko yanapatikana katika nchi yetu. Lakini pia nimpongeze sana mfanyabiashara maarufu AZAM Ndugu Said Bakharesa kwa juhidi zake kubwa sana kwa kujitahidi sana kuwekeza sehemu mbali mbali uwekezaji wake mkubwa Fumba wa nyumba za kisasa na kiwanda pia kuwekeza, nampongeza sana kwa kuwekeza fedha nyingi.

Lakini Mhe. Mwenyekiti mimi niseme kitu kimoja na Wizara iangalie sana hili suala la kuongeza masoko *AZAM MARINE* imeleta boti karibu boti nne au tano, lakini cha kusikitisha Mhe. Mwenyekiti, lile soko sasa hivi naweza kusema *AZAM* labda limeshamzidi na kazidiwa kwa wateja. Kwa sababu juzi nilikuwa Dar es Salaam mimi nilikuwa na mgonjwa wangu nataka kumleta Zanzibar ilikuwa Jumamosi. Mhe. Mwenyekiti, tiketi ya pale *economic class* unainunua kwa shilingi elfu sitini na kitu kibaya zaidi nataka niseme kwa *AZAM* mfanyabiashara mkubwa sana pale nje kuna watu wanakuuzia tiketi elfu sitini. Lakini wanakwambia jina litaandikwa la hilo hilo la abiria wako, sasa yule mtu wa nje anakuwa ndani anaandikisha jina la abiria wako anauza tiketi, sasa wale wanyonge hawawezi kununua tiketi kwa shilingi elfu sitini lakini kwa shida zao wananunua.

Kwa hivyo mimi naomba sana Mhe. Waziri liangaliwe hili soko la maboti hivi sasa limekuwa kubwa sana na limekuwa kama limemzidi mfanyabiashara kidogo, kwa hivyo tuangalie hawa wananchi wetu masikini tiketi za ulanguzi zipo lakini zinauzwa kwa ulanguzi Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo tuangalie sana.

Lakini nije haraka haraka katika ukurasa wa pili wa ripoti yetu ya Kamati hii, Shirika la Taifa la Biashara *ZSTC* wajumbe wengi wamesema wamesikitika sana kwa hii changamoto waliyotuletea hawa wajumbe wetu wa kamati kuhusu udhibiti mdogo wa watoto chini ya miaka kumi na nane kuchuma karafuu. Hili jambo la kusikitisha na mimi naomba sana Serikali kwa sababu mtoto kuanzia miaka minne na kuendelea ndio anapata kujifuna mambo mengi akili yake hii wataalam ndio wamesema. Kwa hivyo mtoto huyu kama takuwa hasomi anakwenda kuchuma karafuu atakuwa hata uelewa wake mdogo kwa sababu elimu ya msingi inaanza kwenye miaka minne kuendelea na kupata ile mila na utamaduni

wa kila kitu kuanzia miaka minne, kwa hivyo naiomba sana Serikali iangalie watoto kuchuma karafuu ni marufuku kabisa.

Lakini jambo jengine changamoto kubwa hawa wenzetu wanaochuma karafuu wanaanguka kwenye mikarafuu na hapa changamoto kubwa wamesema baada ya kuanguka katika mikarafuu inakuwa hakuna kinachoendelea kuwasaidia hasa kama kaumia, inatakiwa bima ya afya hana. Kwa hivyo mimi naomba sana Mheshimiwa bima ya afya ni muhimu kwa kila mtu, tuangalie sasa hivi kuwapa elimu watu kuwa na bima, bima ya afya watoe elimu kuelimisha watu. Kwa sababu ukiangalia bila ya afya kwa mwezi shilingi elfu kumi sasa kama mchuma karafuu kama hana bima bora asichume kwa sababu kama ukiwa na bina itakusaidia kutibwa na kuondosha mzigo kwa serikali. Kwa hivyo naomba sana elimu ya bima itolewe kwa watu wetu wajue kuipata bima vipi wengine mpaka leo hawajui wanataka kujiunga na mfuko wa bima lakini hawajui zile taratibu zake kwa hivyo naiomba Serikali itoe taaluma mbali mbali kwa ajili ya ufahamu wananchi wetu.

Mheshimiwa niende kwenye ukurasa huu wa tano kuhusu changamoto hapa mamlaka ya uwekezaji vitega uchumi ZIPA wenzetu wamezungumza sana sekta hii. Mimi niseme changamoto kubwa hapa wawekezaji wanachelewa kupewa vibali kuwekeza Mheshimiwa, hili jambo ni jema na wawekezaji wanakuja kujua Zanzibar ni nchi nzuri nchi njema yenye amani na watu wake ni wakarimu, sasa wanakuja kuwekeza kwa fedha nyingi sana. Sasa naomba tuwaangalie sana kama vigezo vyao vimetimia tuwape vibali haraka haraka kwa sababu changamoto inasema mtu anafuatilia vibali mara kadhaa anaishia njiani anakata tamaa anaondoka.

Kwa hivyo mimi naomba sana Mheshimiwa hili jambo ni jema sasa tukiangalia takwimu zetu kila mwaka tunapokea karibu

wageni laki nne na nusu wa kitalii wanakuja Zanzibar kutembea, na inafika wakati Zanzibar sasa hivi wakati wa *season* hata hoteli unakuwa hupati zinakuwa zimejaa kwa hivyo wageni wanaokuja kuwekeza watalii wetu hawa wawekezaji tuwape fursa bado maeneo yako wazi yawakezwe na tupate ajira sisi kama wananchi tupate kuajiriwa kwenye sekta hii.

Mhe. Mwenyekiti, niende haraka haraka pia katika maoni ya kamati pia wamesema katika eneo la Michenzani pale Kisonge limekaa mpala leo tupu na kamati imesema hapa halifanyiki uchumi wowote. Mimi nataka kusema tuangalie Serikali kama imeamua kujenga basi ilikuwa kuwaondosha wale lakini wajenge, kwa sababu ukitizama Mheshimiwa wananchi wanahangaika maduka hamna, ajira hawana. Mhe. Mwenyekiti, tuseme takwimu zinaonyesha kama mtu atapokuwa hana ajira atakuwa ana mawazo mengi ya maisha anaingia kwenye madawa ya kulevya mwisho wake, ukiangalia hata watoto kama hawaendi skuli hawapati huduma nzuri ya kifamilia wanaachiwa tu hali ngumu ya maisha wataingia kwenye madawa ya kulevya mwisho wake Mheshimiwa.

Kwa hivyo mimi naomba sana Serikali iangalie lile eneo lifanyiwe haraka haraka wananchi wapate kulitumia kwa mambo yao ya kibiashara, kwa sababu Zanzibar kadri tunavyojua uchumi wetu utalii, karafuu na biashara hakuna chengine. Sasa naomba sana hii sehemu itumiwe kama jambo la kujenga basi atafutwe muwekezaji ijengwe haraka wananchi kutumia ili waweze kujikimu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa Iringa juzi juzi ajira ilivyokuwa shida sasa hivi nimekwenda Iringa kwenye mradi mmoja wa *TASAF* wamepewa fedha vijana wale wakafilisika kwa sababu hawana taaluma nzuri. Lakini sasa vijana wale walivyosikitisha watoto wametoka Chuo Kikuu lakini wameunda mradi wa kuzoa

taka Mheshimiwa uone kama muhimu ajira ilivyokuwa tabu watu wa Chuo kikuu leo wanazoa taka wanapata ajira kwa familia zao wanapata malipo kwa ajili ya kuzoa taka. Kwa hiyo sasa hivi ajira imekuwa ni jambo kubwa sana kwenye nchi yetu kwa hivyo naomba sana Serikali iangalie wananchi wa Zanzibar tusifikie wakati Chuo kikuu leo wakaja kusoma wakaja kujua kuzoa taka ikwa ni ajira yao. Kwa hivyo naomba sana tuangalie haya maeneo yaliyokuwa wazi tuweze kuyafanyia kazi wananchi wetu wakayatumia.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niende kwenye ukurasa wa nne katika ukusanyaji wa mapato Julai, hadi Disemba mimi kwanza niwapongeze sana ndugu zetu wa *ZRB* na nimpongeze sana Waziri anafanya kazi nzuri na niseme watendaji wake wote wa *ZRB* sasa hivi wapo *up to date*, wanafanya kazi vizuri niwapongeze sana kwa juhudi zao kubwa. Mheshimiwa Waziri mimi nakuomba wafanyakazi wako wape zawadi ata *percent* kidogo wape motisha kwa kazi yao nzuri wanayofanya, kukusanya mapato na ku-*deal* na wafanya biashara kupata mapato.

Lakini pia niwapongeze wafanyakazi wa *TRA* kwa kukusanya mapato mazuri na kujfanya kazi nzuri sana, ukiangalia kwenye ripoti yetu asilimia sitini na tatu inakusanywa karibu ukiangalia haraka haraka mwezi zinakusanywa bilioni hamsini hapa si jambo la mashara, ni jambo zuri na la kupigiwa mfano katika visiwa vyetu vya Zanzibar mapato mazuri yanapatikana kwa wafanya biashara mbali mbali.

Lakini Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niseme kitu kimoja wafanyabiashara wetu wanategemea sana biashara kutoka hapa kwenda Zanzibar, Zanzibar kwenda Dar, Dar kwenda Zanzibar kupeleka mizigo kubadilishana huu ni muungano wa nchi huru mbili zimeungana ni muungano wa kidugu wa mapenzi makubwa

sana. Sasa mimi naomba sana Mheshimiwa tuangalie kwa sababu ukitizama changamoto kubwa sasa hivi ukichukua bidhaa hapa ukipeleka bara kuna hii kodi moja *levy duty*. Ukenda Bara *Levy duty* hawaitambui, hapa unalipa 0.5 parcent, lakini ukenda Bara hawaitambui.

Halafu kuna *duty* nyengine UEF hii ukenda bara unalipishwa 3.0 *percent* hapa unalipa sawa vizuri hii *duty* mbili lakini ukenda Bara wanakwambia *duty* hizi hatuzitambui, wao wanataka ulipe *duty custom process fee* ambayo unalipa tena na hizi *duty* mbili hawazitambui wanataka ulipe *duty* hizi mbili. Sasa unakuta wananchi wa Zaznzibar mzigo wao kutoa hapa kupeleka bara unawa-*cost* hata faida inakuwa shida kuipata, ukiangalia ukitoa mzigo kutoka Dubai au nchi nyengine yoyote *freight* kutoka kule kuja Zanzibar ni ghali kuliko kutoka kutoka freight wa kule kwenda Tanzania Bara ni rahisi freight ya kontena.

Kwa hivyo tuangalie mzigo ukija hapa ukiutoa hapa kupeleka tena Bara na hizo kodi zinavyokuwa wananchi wa Zanzibar watashindwa kufanya biashara na itakuwa hata hiyo ajira tunayosema itakuwa haipatikani, mwisho hii takwimu inaonyesha kuwa mtu akiwa na msongo wa mawazo akiwa hana ajira, familia ikiharibika ndio watu wanaingia kwenye madawa ya kulevya kwa kuwa hawana la kufanya hata watoto familia zinaharibika kwa sababu ya ajira.

Kwa hivyo naomba sana tuangalie muungano wetu wa kidugu wa mapenzi mazuri kabisa kwa hivyo tukae pande mbili kutatua na kuangalia faida ili wananchi kidogo waanze kuleta mizigo yao. Kwa sababu ukiangalia pale Dar es Salaam unaweza kuambiwa utoe pesa kwa mzigo wake lakini pesa serikalini haiendi watu wanachukua wao. Sasa mimi naomba tuangalie sehemu zote mbili hizi pesa tuwaachie pele pafungwe kamera pasichukuliwe fedha, ka sababu kutoka na mzigo Zanzibar upite tu pale Tanzania bara

hasa wafanya biashara wadogo kilio chao kikubwa kila ukenda uchaguzi mimi uchaguzi zangu mbili tumekwenda tumeona mapambano wapinzani wanakuja na agenda yao moja tu, hawasemi kwenye jimbo hakuna maji, hawasemi kwenye jimbo hakuna barabara hakuna skuli, wanasema muungano tu kila tukienda kwenye muungano, muungano huu ni mzuri ni faida sana kwa Zanzibar lakini turekebishe kidogo tu hii ajenda yao wapinzani tuondoshe kabisa kila mwaka kubomoa muungano wetu huu wa kidugu wa damu kabisa.

Kwa hivyo mimi naomba sana Mheshimiwa tuangalie na nina jambo moja nataka kusema ukiangalia ukitoa kama gari hapa ukipeleka Bara utaambiwa ulipe kodi na ulipe kodi na *deference* lakini *deference* yenyewe unalipa hapa, lakini ukenda kule pia *deference* wanakuwa hawaikubali, juzi juzi kuna mfanyabiashara mmoja kaambiwa alipe *defrence* kalipishwa kule pesa ile haibakii hapa inabakia kule.

Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia upande mwengine mimi nakwenda mikoa mingi natembea naona nakuta gari za Kenya, gari za Uganda, gari za Ruwanda sasa mimi nashangaa hizi gari za Ruwanda zinakuja zinaondoka kwa nini wanapewa vibali kwa dola hamsini tu wanaingia Tanzania Bara wanatembea wanarudi. Sisi leo ukiamua kuchukua gari yake uende nayo Bara unaambiwa ulipe ushuru. Sasa kama mtu anakwenda kutembea kwa wiki mbili wiki tatu kwa nini hapati fursa na huu ni muungano tena muri jamani. Sasa mimi naomba Mhe. Waziri hebu kaa kidogo uangalie zaidi kwa sababu Zanzibar wapo watu milioni moja laki tatu sio wengi na kule wako watu karibu milioni arubaini na tano. Sasa kama milango hii ikifungika na hichi ni kisiwa Mheshimiwa itakuwa shida kwa ajira kwa wananchi wetu hawa wanatuzunguka katika kisiwa cha Zanzibar, kwa hivyo mimi naomba sana tuangalie pande zote mbili.

Leo hapa Mheshimiwa Mwakilishi wa Welezo alisema wafanyabiashara wana tabia mbaya hivi lakini mimi nasema Mhe. Hassan kidogo kakosea kwa sababu niseme hawa wafanyabiashara wanachangia pato la taifa *thirty percent* wa ushuru wanalipa, kuna wafanya biashara baadhi lakini sio wafanyabiashara wote utasema wabaya. Kwa sababu kuna wengine wanatoa zaka humu, kuna wengine wanalipa kodi vizuri, sisi tunapata *thirty percent* kuchangia pato la taifa kwa ajili ya wafanyabiashara hawa. Sasa tukiwasema vibaya mimi siko pamoja nae kwa sababu wafanyabiashara hata humu kwenye Baraza wamo, Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil mfanyabiashara, Mhe. Jaku Hashim Ayoub mfanyabiashara, Mhe. Mohamedraza Hassanali mfanyabiashara, mimi pia ni mfanyabiashara. Kwa hivyo nasema tuwaheshimu na tundelee kuwa nao, tuwalee na tuwapende, hawa ni ma-*patner* zetu, hawa ni marafiki zetu na serikali kwa sababu wanatulipa kodi. Mimi naomba sana ndugu zetu wa ZRB tushirikiane nao vizuri hawa ndugu zetu wafanyabiashara ni sawa na uti wa mgongo au wanatusaidia kama kusukuma ni kama injini ya nchi yetu kwenda kwa ajili ya kodi. Tukae nao vizuri, tuwaheshimu na tuwapende ili wazidi kuipenda nchi yao na wafanyabiashara katika Zanzibar yetu kwa pamoja.

Mheshimiwa baada ya hapo mimi nakushukuru sana na naunga mkono ripoti hii, lakini sana nawapongeza Mawaziri wote hasa Waziri wa Fedha kwa kazi yake nzuri kabisa, hasa sisi Wabaraza la Wawakilishi hatujawahi hata siku moja kukosa mafao yetu kwa ajili yake. Kwa hivyo namshukuru sana, Mwenyezi Mungu amzidishie. Pia Mwenyezi Mungu amzidishie hekma na busara Rais wetu wa Zanzibar na Makamu wetu wa Pili kwa kutuongoza vizuri na nchi hii kuwa na amani na utulivu, mimi nashukuru sana, ahsante sana. Naunga mkono asilimia kwa mia.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana nakushukuru Mhe. Hussein Ibrahim Makungu kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite

Mhe. Rashid Makame Shamsi mchangiaji wetu wa mwisho kwa Waheshimiwa Wajumbe Wawakilishi na baadae nitawapa nafasi Mawaziri husika ili na wao watoe ufafanuzi. Lakini wakumbuke kwamba ripoti hizi zitapatiwa majibu katika mwezi wa 9, kwa hivyo kama wana chochote wanaweza wakazungumza.

Mhe. Rashid Makame Shamshi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipa nafasi hii ya kuweza alau na mimi kuchangia machache juu ya ripoti hii ya Kamati ya Fedha, Kilimo na Biashara.

Awali ya yote nichukue fursa hii kuwapongeza Mawaziri wote watatu ambao wanahusika na ripoti hii kwa utekelezaji wa majukumu mbali mbali katika Wizara zao. Nichukue fursa hii vile vile kuishukuru na kuipongeza sana Kamati inayohusika kwa kuweza kuwasilisha ripoti hii kwa uweledi mkubwa, ni ripoti ambayo imeweza kusheheni mambo mbali mbali ambayo wenzetu wameyabaini, changamoto mbali mbali na yale maoni na mapendekezo ambayo wameyatoa kwa serikali. Niwapongeze sana na nimpongeze sana Mwenyekiti wa Kamati Mwakilishi makini wa jimbo la Fuoni.

Mhe. Mwenyekiti, niwapongeze Wajumbe wote walionitangulia kwa michango mbali mbali yenye nia ya kujenga na kuishauri serikali juu ya utekelezaji wa majukumu ambayo yanaweza kuleta muafaka lakini vile vile tija na maslahi kwa wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niogelee katika mambo matatu, nianze ukurasa wa 16 juu ya ziara ya wenzetu wana kamati waliotembelea Dubai na wakaweza kuibua mambo mbali mbali na changamoto ambazo wameziainisha juu ya suala zima la mkataba uliopo kati ya Kamapuni ya Jabar, Kilimanjaro, pamoja na Shirika letu la ZBS Zanzibar. Wenzetu katika Changamoto napenda nizinukuu wamesema:

1. “Kutopitishwa kwa magari katika Kampuni hiyo kwa ajili ya kukaguliwa kunakofanywa na baadhi ya wafanyabiashara wajanja.”

Serikali imeweza kuingia mkataba na Kampuni hii kwa lengo la serikali kuweza kujiingizia kipato juu ya suala zima la uagizaji wa magari kutoka nje. Kazi hii inafanywa na wakala huyu kwa mkataba maalum. Inapotokezea kwamba kuna wafanyabiashara wajanja ambao wanakwepa magari yao kukaguliwa na Kampuni hii maana yake serikali inakosa mapato. Changamoto ya pili nayo inasema:

2. “Kuingia na kupokelewa kwa magari katika bandari ya Zanzibar yaliyokuwa yajakaguliwa licha ya kufahamika kuwa serikali imeingia mkataba na Kampuni".

Sasa hapa napo pana tatizo, kama kuna magari yanaingia na yanaeleweka kwamba hayakukaguliwa, wakati serikali ina mkataba na kampuni husika halafu yanaingia na yanaruhusiwa kutoka. Maana yake hapa kuna utendaji ambao una kasoro. Kama serikali imekubaliana na Kampuni basi sheria lazima zifuate mkondo wake. Hatuwezi sasa kuyapitisha magari ambayo hayajakaguliwa, huku tukielewa kwamba serikali ina makubaliana na Kampuni hiyo, maana yake hapo ni kuipunguzia serikali mapato.

Changamoto ya tatu wanasema:

3. "ZBS kushindwa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara ili kujionea wenyewe Kamapuni.”

Sasa hapa chombo chetu hichi lazima nacho kiwe makini kwa sababu tumeingia mkataba nacho kinalazimika kuweza kutekeleza

majukumu yake ambayo yamepangiwa, vyenginevyo maana yake ile asilimia 30 ambayo ipatikane kwa serikali maana inawezekana isipatikane. Kwa maana hiyo serikali itakuwa lile lengo la kufanya mkataba huu lisiweze kupatikana. Niiombe sana ZBS kuweza kutekeleza majukumu yake lakini na vile vyombo vyengine ambavyo vinaisaidia ZBS basi kuweza kuona vinatekeleza majukumu yake ili kuona hakuna mapato yanayovuja katika suala zima la mkataba huu.

Mhe. Mwenyekiti, nielekee sasa ukurasa wa 22, katika ukurasa huu kuna suala zima la kiwanda cha ushoni cha Idara Maalum za SMZ. Kiwanda hichi kinamilikiwa na Wizara ya Nchi, Afisi ya Rais Tawala za Mikoa, humu limezungumziwa suala zima katika Wizara ya Biashara. Hichi ni kiwanda, nimeshtushwa sana na changamoto ambazo zipo pamoja na juhudi za serikali kuweza kuanzishwa kiwanda kile, lakini tuwapongeze wenzetu Wachina kwa msaada waliotupa wa vifaa mbali mbali katika kukihuisha kiwanda kile. Lakini changamoto zilizotajwa na Kamati ambazo ni tatu na napenda nizunukuu kwa muhtasari:

1. Kuna ukosefu wa mitaji ya kutosha kwa kukiwezesha kiwanda hicho kujiendeleza kwani kiwanda hicho kilianzishwa mara tu baada ya kupatikana msaada wa mashine kutoka Jamhuri ya Watu wa China.

2. Uhaba wa mashine za kufanyia kazi.

3. Kuwepo kwa deni kubwa linalodai kiwanda hupunguza ufanisi wa shughuli wanazozifanya.

Kiwanda hichi miongoni mwa malengo yake ilikuwa ni kuzalisha au kushona nguo za askari wetu wa Vikosi vya SMZ, hilo lilikuwa ni lengo moja kubwa.

Lengo la pili ni kuweza kukifanya kiwanda hichi kiweze kujiendesha kibiashara. Sasa kama kunachangamoto ya ukosefu wa mtaji, lakini vile vile kuna changamoto ya uhaba wa mashine, kidogo inashangaza.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naelewa sana kiwanda hiki, Serikali ya China ilitoa msaada wa mashine zisizopungua 50, lakini ukweli usiofichika, mashine ambazo hasa zinatumika katika kiwanda hichi hazizidi 20. Sasa kusemwa hapa kuna uhaba wa mashine labda iwe ni mashine za aina nyengine. Kiwanda hichi kinafanya kazi chini ya kiwango, huo ndiyo ukweli.

Mhe. Mwenyekiti, hapa tumezungumza katika mijadala mbali mbali, vikosi vyetu vinatatizo la unifomu, vikosi kama vina tatizo la unifomu maana yake unifomu hizi iwe zinashonwa na kiwanda hichi. Inaonekana kuna ukosefu wa ubunifu, kiwanda hichi hakina kazi, kitafutiwe kazi hichi kiwanda kama ni kuwashonea vikosi, basi serikali iweze kununua vitambaa ili nguo za vikosi zishonwe na kiwanda hichi, hapo kiwanda kitakuwa na manufaa. Lakini kama hali inayoendelea ilivyo, kiwanda hichi kina ukosefu wa kazi kutoka katika sehemu yengine. Kwa sababu gani? Maana yake ndani ya kiwanda huna wataalamu wa uchumi, huna wataalamu wa biashara wa kuweza kutafuta masoko. Maana yake hizi changamoto tutazizungumza lakini hata wakipatiwa mtaji kama huna wataalamu wa kutafuta masoko au vile vile serikali ikaingiza vitambaa pale kwa kuwashonea vikosi maana yake hichi kiwanda kitakuwa hakina kazi ya kufanya na mashine ambazo zipo pale zinaweza kupelekea kufa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo niiombe sana serikali, najua serikali ina nia nzuri na Mhe. Waziri wa Vikosi amezungumzia juu ya azma njema. Vile vile Mhe. Waziri wa Fedha aliwahi kuzungumzia juu ya suala ya kuondosha tatizo la unifomu la maaskari na lengo ziweze kushonwa pale. Niiombe sana serikali

kukitumia kiwanda hichi kwa sababu tunapoelekea tunasema kwamba tunakwenda katika karne hii ambayo tunataka kwamba viwanda iwe ni sehemu moja kubwa sana ya kuzalisha kwa uchumi wetu Watanzania. Tanzania, tukitumie hichi kiwanda lakini kiandaliwe mazingira mazuri ya wataalamu, lakini vile ubunifu katika kutafuta masoko.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo naomba nimalizie katika ukurasa wa 31(4) (5) kuhusu Misitu ya Hifadhi wa Taifa wa Kiwengwa. Serikali kwa malengo mazuri sana imeweza kuweka misitu hii ya hifadhi, suala hili linaifanya serikali kuwa na uhakika wa rasilimali misitu. Kama tunavyoelewa misitu yetu mingi hivi sasa imekatwa ovyo, imechomwa ovyo, kiasi ya kwamba hata ile kuni ya kupikia hivi sasa kwa wananchi imekuwa tatizo. Lengo la serikali kuweka misitu ya hifadhi ni kuweza kulinda mali ya asili hii.

Mhe. Mwenyekiti, wenzetu wana Kamati wameibua changamoto mbali mbali hapa juu ya Msitu wa Hifadhi wa Kiwengwa, wamesema kwamba kuna hali ya uvamizi wa msitu huo na baadhi ya wananchi wanaotoka nje ya maeneo hayo kwa kufanya shughuli za ufugaji na ukulima na kuanzisha makaazi kinyume na utaratibu uliowekwa.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa naomba umalizie.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana, vile vile kuna upungufu mkubwa wa wafanyakazi walioajiriwa kuiendesha hifadhi hiyo. Katika ripoti ya mwaka jana juu utekelzaji, wenzetu walitwambia kwamba uongozi wa misitu uendelee kutoa mashirikiano ya karibu na wana kijiji na Wizara ikasema kwamba imewezeshwa uundwaji wa Kamati 57 za Uhifadhi wa Misitu ya Jamii kwa Unguja na Pemba. Mimi hapa nina wasiwasi kama Wizara imeunda Kamati ya 57 bila ya shaka moja kati ya Kamati

iwe ya Msitu wa Hifadhi Kiwengwa, sasa kama bado msitu huu unaendelea kuvamiwa basi hii ni hatari. Niiombe sana Wizara inayohusika na misitu kuweza kuona kama hizi kamati zimeundwa basi Kamati hizi ziwe zinafanya kazi na kama kuna uhaba wa wafanyakazi basi tuweze kuwaajiri wafanyakazi ili kuweza kulinda rasilimali hizi muhimu, vyenginevyo nchi yetu hii itageuka jangwa na madhara mbali mbali ya majangwa tunayaelewa.

Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi hiyo na mimi niseme tu kwamba naunga mkono ripoti hii kwa asilimia mia na niwaombe wenzetu wa Mawizara basi waweze kuitizama vizuri ripoti hii ambayo imepangika vyema na mwezi Septemba watuletee majibu ambayo yatakuwa na matumaini kwa wananchi wetu. Ahsante sana Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Nakushukuru sana Mhe. Rashid Makame Shamsi. Waheshimiwa Wajumbe nilikuwa nimeombwa nafasi na Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, lakini naomba niombe radhi kwa sababu nataka nimpe na Mwenyekiti, wa Kamati nafasi muda wetu mchache kwa hivyo nitampa moja kwa moja Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, aseme machache na baadaye atafuatiwa Mhe. Waziri wa Fedha na mwisho nitampa nafasi Mheshimiwa anayekaimu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko.

Mhe. Nadir Abdul-latif yussuf Al-Wardy: Mhe. Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa nimekuona kuhusu utaratibu lakini nakuomba ukae tumalizie.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mnatuonea hivyo.

MICHANGO YA MAANDISHI

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Yussuf Hassan yeye ni kamanda wa makamanda wa Jimbo la Fuoni. Naunga mkono hotuba yake ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa asilimia mia moja. Wewe ni tegemeo la Fuoni na CCM kwa ujumla.

Mhe. Juma Ali Khatib (Waziri Asiye na Wizara Maalumu (MBM): Mhe. Mwenyekiti, nashauri tuchukue hatua za haraka kuwakamata watu wote huko Pemba ambao wamekodishwa mashamba ya Karafuu na hadi hii leo hawajalipa serikalini. Ni vizuri wapelekwe kwenye vyombo vya sheria ili walipe fedha walizokodishiwa mashamba ya karafuu na mara nyengine watu hawa wasikodishwe tena. Ahsante.

Mhe. Mtumwa Suleiman Makame: Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu *(S.W)*. Pia namshukuru yeye Mhe. Mwenyekiti, kwa taarifa yake aliyoitoa.

Idara ya Misitu
Mheshimiwa mimi nazungumzia suala la Kituo cha Misitu kiliopo Chaani Masingini, kituo kile kilikuwa kina misitu mingi sana, wananchi walikuwa wanatumia kwa kupata mbao, majengo ya kujengea, pamoja na kuni za kupikia.

Mheshimiwa sasa hivi msitu ule umekuwa haupo kama zamani. Kwa hivyo, naiomba serikali eneo lile mwanzo kabla kupandwa miti ya kawaida lilikuwa na mikarafuu hivyo, basi ningeomba serikali eneo lile likapandwa hiyo hiyo mikarafuu.

Mheshimiwa ukurasa 36 kuhusu kilimo cha mpunga cha umwagiliaji maji. Kwa kweli nawapongeza viongozi wa wizara

hii kwa jitihada zao kubwa wanazozichukuwa kwa kushughulikia suala la umwagiliaji maji. Lakini sasa kuna kilicho cha asili cha mpunga kwa kutumia msimu wa mvua kilimo ndio watu huanza kupanda mwezi wa Oktoba, lakini ndio kwanza wananchi wanalimiwa ambapo Mei uwe umeshamaliza kupanda kwa mbegu kama vile:

- Ringa
- Kidicho
- Chale ya makonde
- Supa na kadhalika.

Kwa hali hiyo naiomba serikali iwapitie wakulima hawa wanaolima mabonde kwa kutumia mvua ya mwaka na masika ili wajuwe utaratibu wao unapoanza.

Niunge mkono taarifa hii kwa asilimia mia moja ahsante.

Mhe. Khamis Juma Mwalim: Naipongeza Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa ripoti nzuri iliyosheheni mambo mbali mbali kwa ajili ya kujadiliwa na kuishauri Serikali.

Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali:

Naipongeza Afisi hii kwa kusimamia usajili wa biashara na mali kama vile usajili wa nyaraka, usajili wa alama za biashara na usajili wa kampuni, ni vyema Taasisi hii ikaengeza jitihada ya kutoa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa usajili wa biashara na mali, kwani imebainika kuwa baadhi ya wajasiriamali wanatengeneza bidhaa za aina mbali mbali lakini wanashinwa bidhaa zao kuzitia alama za biashara hali ambayo wajanja wachache inapelekea bidhaa zao kuziiba na kuzitia alama za biashara *(Trade Mark)* kama vile wao ndio wamiliki halali wa

bidhaa hizo. Hivyo elimi inahitajika kwa wajasiriamali hao ili waweze kupata kipato zaidi.

Mhe. Spika, naunga mkono hoja asilimia kwa mia.

Mhe. Ali Khamis Bakari: Naomba wizara ya Fedha iharakishe pesa za mfuko wa jimbo ili tuweze kutatua matatizo ya wananchi.

Lakini pia bei za wafanyabiashara wa maduka ya chakula Vijijini, bei kubwa wanakomowa wananchi, vile vile Kitabu kimetaja shughuli za uanikaji dagaa tu hali ikizungumza uanikaji mwani, mapendekezo yangu elimu itolewe juu ya uanikaji mzuri wa mwani ili mwani uwe mzuri na kuengezwa bei.

Mhe. Mussa Ali Mussa: Mhe. Mwenyekiti, mimi mchango wangu kwa Wizara ya Kilimo ni kwa upande wa zao la Mwani, kwa kweli ni kusema wananchi wangu wanapoteza nguvu nyingi faida ni ndogo sana, ni vyema zao hili nalo likanunuliwa na Serikali, kama vile karafuu.

Mhe. Mwenyekiti kuwepo wadudu wanaoharibu zao hilo na kuwapa hasara wakulima zao hili la mwani Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa zao la mpunga ukurasa wa 36 zao la mpunga zao hili Mhe. Mwenyekiti, ni zao maarufu na ni muhimu sana kwa wananchi wa Zanzibar, lakini changamoto zake ni kutegemea mvua za mwaka, sasa ni lazima Wizara ya Kilimo na Serikali ibadilike na kutumia kilimo cha umwagiliaji maji.

Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mhe. Rashid Ali Juma: Naomba kuchangia kwa maandishi kwa kuipongeza Kamati. wajumbe wote kwa utendaji wao na

mashirikiano pamoja na watendaji wa Wizara zote tatu. Hii imeonesha wazi utekelezaji wa Ilani ya CCM 2015/2020.

Kwa utendaji huo naona Wazi na matumaini makubwa ya kuinua uchumi, kuongea mapato kupitia biashara na kilimo, kwa ripoti hii naamini hoja zitapungua sana 2028.

Mhe. Tatu Mohammed Ussi: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweza kuchangia ripoti hii ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi kwa mwaka wa Fedha 2017/2018.

Niipongeze kamati hii kwa kazi nzuri waliyoifanya lakini pia niwapongeze watendaji wa Wizara hii kwa kazi nzuri waliyoifanya kwa kushirikiana na Kamati hii kwa lengo la kufanikisha ripoti hii.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Fedha na Mipango ukurasa wa tisa kifungu 2.10 Benki ya Watu wa Zanzibar *(PBZ)* changamoto tawi la *PBZ* Mkoani, nakubaliana na changamoto zilizotajwa na kamati zilizomo katika Benki hii changamoto hizi zipo na zinahitaji kuchukuliwa hatua.

Naanza na Changamoto kukosekana kwa uzio katika kituo cha Mkoani suala hili linahitaji kuchukuliwa hatua kwa sababu wahalifu wakati wowote wanawaza kuingia na kufanya hujma, ingawaje walinzi wapo laikini walinzi nao ni binaadamu.

Upungufu wa vitendea kazi ikiwa ni pamoja na usafiri, kwa watendaji wake, Mhe. Mwenyekiti, suala la usafiri ni muhimu kuangaliwa kwa jicho la huruma kwani wafanyakazi hawa wanaishi mbali na kituo chao cha kazi hivyo wanahitaji kupatiwa usafiri.

Mhe. Mwenyekiti, kituo cha Mkoani hakina usawa wa jinsia ni kweli katika kichuo hicho hakuna mfanyakazi mwanamke walioko wote ni wanaume, hivyo nashauri awepo na mfanyakazi mwanamke kwa sababu wanaume unapofika wakati wa swala wanaondoka kwenda msikitini na badala yake huduma husita mpaka warudi, lakini akiwepo mwanamke wakiondoka ataendelea na huduma kwani wakati mwengine *ATM* inakuwa haifanyikazi na wateja hulazimika kukaa kusubiri huduma hivyo akiajiriwa akiwepo mwanamke ataendelea na huduma bila ya wateja kupoteza muda.

Mhe. Saada Ramadhani Mwenda: Mhe. Spika, kwanza naanza na kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati hii kwa kuwasilisha ripoti hii iliyojaa ufanisi wa kulijenga taifa kimaendeleo ya nchi yetu Zanzibar. Lakini piya niwapongeze wajumbe wako wote waliofanya kazi hii kwa uwiyano.

Mhe. Mwenyekiti kwanza tawi la Biashara la Kimataifa Nchini Dubai, ni kweli na mimi naunga mkono kamati, kwa kuweza kuajiri mfanyakazi mzalendo kutoka huku nchini kwetu, haiwezekani mtu awekwe kwenye mali kama hiyo wakati hana utaifa na huko biashara hiyo inakotoka binaadam atabaki kuwa binaadamu, hizi karafuu zinashuka soko utajuwaje kama anafanya uzaifu anachanganya na karafuu za nchi nyengine ambazo zisizo na ubora utajuaje huwezi kujua.

Naendelea ukurasa wa 5 mamlaka ya uwekezaji Vitega uchumi *ZIPA*, Mhe. Mwenyekiti, hawa wawekezaji wanaokuja hapa nchini wanapokuja wanakuwa watii sana chochote watakacho ambiwa wanakuwa wanakubali, masharti wanayopewa ila tu wakishapata wanakuwa na usumbufu mkubwa hussan wakipata upande wa bahari, wanakuwa wanawatesa wananchi wetu.

Kwa hivyo naomba Serikali au Wizara husika wanapowapa viwanja wawe wanawapitia kuona yale matumizi wanayotumia nikweli, wana kwenda sambamba na hiyo mikataba yao nakushukuru Mwenyekiti.

Naunga mkono ripoti hii asilimia mia kwa mia ahsante.

Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi.

Ukodishwaji wa Mashamba ya Serikali ya Mikarafuu Pemba Mimu wa Mwaka 2017.

Mhe. Mwenyekiti, nashauri mashamba haya yakikodishwa wapewe kipaumbele wale wanaoyashughulikia haya mashamba kwa sababu wameshughulikia mashamba kwa muda mrefu, kwa sababu inaonekana hao waliokodishwa hawajalipa hadi leO, sasa kwa nini wanaoshughulikia wasikodishwe wao.

Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 33 kifungu 4,7,1 Uzalishaji wa zao la mwani.

Mhe. Mwenyekiti, changamoto ya bei ndogo ya zao la mwani, nashauri Serikali iangalie bei ya mwani kwani mwani una kazi kubwa ya kuushughulikia, hivyo Wizara ya Biashara iongeze bei ya mwani ili kuwapa moyo wakulima wa mwani.

Mhe. Naunga mkono ripoti hii asilimia mia moja.

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini: Mhe. Mwenyekiti, hongera kwa ripoti nzuri naikubali kwa asilimia mia moja.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu juhudi Nam.5 *page* 28, jadweli lichambuliwe zaidi lioneshe kwa kila kundi la shamba. Tuchapishe majina yote kwa mashamba 1452.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwanza naomba nichukue fursa hii kumshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati na Kamati yake kwa kazi nzuri sana waliyoifanya na nataka tuwaahidi tu kwamba mwezi wa 9 majibu pamoja na hoja zilizotolewa Waheshimiwa Wawakilishi tutazijibu kwa ufanisi mkubwa sana.

Mhe. Mwenyekiti, sikutaka niseme maneno mengi, isipokuwa kuna mambo matatu nimeona niyatolee ufafanuzi kidogo tu.

La kwanza limesemwa sana suala zima la fedha ambazo zimekodishwa mikarafuu na watu hawajalipwa. Nielezee hatua za serikali zizochukua. Kabla sijaelezea hatua niseme tu kwamba mwaka 2013 mashamba yote ya serikali yalikodishwa kwa shilingi milioni mia moja na kumi na saba na sabini. Mashamba 14 yalikodishwa kwa shilingi hamsini na tano milioni. Mashamba 15 yalikodishwa kwa sabini na mbili milioni na mashamba 16 yalikodishwa kwa shilingi thalathini na sita milioni. Mwaka 2017 hizo fedha ambazo zimelipwa ni bilioni moja mia mbili na kumi na tatu.

Kwa hivyo tunaona tofauti kubwa ya kazi iliyofanyika ya kuweza kuyabaini mashamba na kujua kwamba serikali ilikuwa inapoteza mapato kwa kiwango kikubwa. Naomba tumshukuru sana Rais wetu kwa kuliona hili na aliunda hata Kamati ikiongozwa na Mhe. Dkt. Sira Ubwa Mamboya, Mwakilishi na MBM kuangalia mashamba ambayo yamehodhiwa kinyume cha utaratibu na

hatimaye yakaibuliwa na ndiyo matokeo haya mnayoyaona yametokea.

Mhe. Mwenyekiti, nasema kuna kazi kubwa imefanyika kipindi kirefu kabisa mashamba haya yalihodhiwa kinyume cha utaratibu, watu wakayaficha na viongozi wengine wameshiriki katika hilo na serikali sasa imeyaibua na tutaendelea kufanya kazi vizuri. Pamoja na kazi hiyo iliyofanywa, hivi juzi tumefanya kazi nyengine na kupata taarifa kuna mashamba mengine 57 ambayo yamefichwa, tumeyabaini na tunajua sasa nani na nani anayo na taarifa itakwenda kwenye Kamati ambayo imeundwa na serikali kuyasimamia mambo hayo. Kwa hivyo nasema juhudi ya serikail kubaini rasilimali za nchi zinafanyika na nawahakikishia Waheshimiwa tutambaini kila mmoja ambaye amehodhi rasilimali za serikali kinyume cha sheria na hatua zitachukuliwa.

La pili niseme tu kwamba katika kubaini mambo hayo Rais ameunda Kamati ikiongozwa na Waziri wa Biashara na Viwanda, Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais Tawala za Mikoa na mimi mwenyewe nilikuwa mjumbe kuangalia ukodishaji mzima na Mhe. Said Soud Said samahani nilikuwa nimemsahau, kuangalia tasnia nzima hii ya watu walikodi mikarafuu na ambao hawajalipa. Nakuhakishieni wananchi na Waheshimiwa tutakapokuja karibuni tutatoa taarifa kwenye serikali na hatimaye tutaiwasilisha taarifa hiyo katika mwazi wa 9 kikamilifu. Serikali imewafatilia lakini mapato yanayopatikana makubwa kutokana na usimamizi mzuri uliofanywa hilo jambo la kwanza nataka niliseme.

Lakini la pili lilizungumzwa sana suala la wakulima wa mwani kwamba hawapati bei nzuri. Ni kweli baada ya kugundua hilo serikali tumeona ni vizuri tuanzishe viwanda ambavyo vitasaidia. Nataka nilishukuru sana Shirika la FAO kwa kutupatia mashine mbili, moja imeshafungwa na moja inafika kesho, naamini kabisa

hiyo tukianza kuzalisha wenyewe bidhaa zinazotokana na mwani ndiyo jibu la bei ya mwani. Bei ya mwani kwa kutegemea soko la nje tu tukauza roho, siyo jibu hata kidogo. Bahati nzuri tulikuwa tuna mazungumzo na Waziri wa Kilimo kutoka China alikubali mwezi wa tarehe 5 Machi, anafika hapa na timu yake kuangalia ni namna gani wataanzisha viwanda vya mwani ili waweze kununua mwani wao kwa sababu una wanunuzi wakubwa wa mwani ule ambao lakini utakuwa *process* sio huu ambao tunaufanya, hizo ndio hatua ambazo serikali inachukua.

Mhe. Mwenyekiti, lakini nataka nimshukuru tena Mhe. Rais kwa kuweza kutupatia matrekta ya kutosha sasa kwa kuweza kufanya kazi. Tumepata matrekta kutoka Libya yale matrekta bahati mbaya ulitoka msaada tokea marehemu Mhe. Gadafi yuko hai, yakaa bahati mbaya pale Dar-es-Salaam muda mrefu yakapigwa na mvua yakaharibika sana, yakaibiwa vitu, baadae wakatwambia mnayataka tukenda kuyaangalia tukayapima tukaona kwa kweli matrekta matatu tukiyatengeneza tunaweza tukapata matrekta.Yote kumi sasa hivi yako tayari na yako mashambani na yanafanya kazi vizuri na mengine tena kumi juzi tena Rais ametupatia yanafanya kazi tuna matrekta ishirini tukijumlisha na yale ishirini na moja tunayo arubaini na moja yanafanya kazi vizuri kwa shamba tunategemea kazi itakwenda vizuri, nataka nimshukuru Mhe. Ris kwa kazi nzuri aliyoifanya.

Ahadi yetu Mhe. Mwenyekiti, ya kuhakikisha kabisa kama miaka mitatu ikifika hali ya chakula itakuwa nzuri bado iko pale pale na wananchi wasiwe na wasiwasi serikali iko makini tutafatilia masuala yote ambayo wenzetu wametukaribia.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja naomba wajumbe tusubiri mwezi wa tisa tulete majibu rasmi. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Nakushukuru sana Mhe. Waziri wa Kilimo sasa naomba nimwite Mhe. Waziri wa Fedha na Mhe. anayekaimu Wizara ya Viwanda na yeye ajiandae.

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba nichukuwe fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii na mimi kusema machache ya kuchangia hoja hii lakini vile vile kutoa ufafanuzi katika baadhi ya maeneo.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati Mhe. Yussuf Hassan Iddi Mwakilishi wa Jimbo la Fuoni na niwapongeze na kuwashukuru wajumbe wote wa Kamati hii, Kamati ya Fedha, Bishara na Kilimo kwa mashirikiano mazuri ambayo wanatoa katika wizara yetu Wizara ya Fedha na Mipango. Lakini vile vile niwapongeze na kuwashukuru kwa ripoti nzuri sana waliyoitoa ambayo imetoa fursa kwa waheshimiwa wajumbe kuichangia na kama ilivyo kawaida Mhe. Mwenyekiti, majibu kamili tutayatoa mwezi wa Septemba.

Lakini leo namba niseme machache sana na kwa mnasaba wa kutoa ufafanuzi kwenye baadhi ya maeneo na moja ni suala la mapato na kwenye suala la mapato Mhe. Mwenyekiti, nichukuwe fursa hii kumshukuru sana Rais Dkt. Ali Mohamed. *(Makofi)*

Namshukuru kwa miongozo yake anayotupatia ambayo inatusaidia sana katika suala zima la kuimarisha ukusanyaji wa mapato hapa nchini, ukweli kwamba mapato yameongezeka sana, yameongezeka kwa karibu mara tatu ya kile kima ambacho tumetakiwa kukusanya hapo nyuma na kwa mwezi wa Januari tumefanya vizuri zaidi.

Kwa hivyo, nichukue fursa hii kumshukuru Mhe. Rais lakini vile vile niwashukuru sana TRA, niwachukuru ZRB na watendaji wote wanaohusika kwa shughuli za ukusanyaji wa mapato. Lakini pia niwashukuru walipa kodi wenyewe kwa sababu bila ya

mashirikiano na walipa kodi, wafanya biashara, wawekezaji na wananchi kazi hii haitofanyika katika kiwango kizuri kama inavyofanyika.

Lakini pamoja na pongezi hizi niseme na nikiri kwamba bado tuna fursa ya kuongeza mapato tunachokikusanya ni kiwango kikubwa lakini bado *potential* iko kubwa sana, sasa tusilegeze kamba katika hili. Wananchi, wafanyabiashara, wawekezaji sote tufanye kazi kwa mashirikiano ili kuweza kuimarisha mapato na kukuza uchumi katika nchi.

Mhe. Mwenyekiti, kuna mambo yamezungumzwa na moja ni suala la msongamano katika benki yetu ya PBZ, hili limeshazungumzwa mara nyingi na tumejaribu kulitokea ufafanuzi. Naomba nielezee kwamba PBZ inajitahidi sana kwanza kuweka taratibu za watu kulipia kutumia simu zao za mkononi. Lakini vile vile kuna utaratibu wa kubadilisha mfumo mzima kwa maana ya ile *core banking system* ili itakayoweza kuhudumia wateja wengi zaidi kwas ababu iliyopo sasa imewekwa zamani na ilikuwa ina kiwango cha kuhudumia wateja wachache.

Lakini vile zipo juhudi ambazo zinafanywa kwa mfano kuongeza idadi ya *ATM* lakini kwenda masuala ya *internet bank* haya yanafanywa na masuala ya mazingatio ya kuanzisha *Visa Card* na *Master Card* nayo hayo tutayatolea ufafanuzi kwamba ni miongoni mwa mipango ya benki hii katika kuimarisha shughuli zake.

Lakini kuna suala jengine hapa ambalo ningeomba sana kamati ningemuomba sana Mhe. Mwenyekiti wa kamati kwamba zipo taarifa ambazo zimetolewa humu hasa za ukusanyaji wa mapato ningeomba hizo tuziangalie vizuri zaidi, kwa sababu katika mwaka wa fedha 2017/2018 tulipanga kukusanya *trillion* moja, bilioni thamanini na saba nukta tatu na mapato ya ndani ni bilioni

mia sita sabini na tano nukta nane. Lakini kwenye ripoti hii kwa bahati mbaya imeandikwa ni *quillion* moja bilioni hamsini na tisa nukta nne na pia mapato ya ndani bilioni mia sita arubaini na tisa nukta nne ambazo kwa kweli si sahihi na zile ambazo tuliziripoti wakati tunawasilisha bajeti ya serikali.

Lakini pia nimpongeze sana Mhe. Hassan Khamis Hafidh (Diaspora) na nakubaliana naye kimsingi kwamba pamoja na juhudi za kuongeza mapato lazima usimamizi wa matumizi ya mapato hayo uimarishwe hilo nakubalibana nalo na ndio maana Serikali imekuja na Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Serikali sheria nambari 11 ya mwaka 2016. Sasa kwenye sheria hii sasa kazi ni kwetu kusimamia utekelezaji wa sheria hii na sisi kama wizara sasa hivi tunasimamia kwanza kuimarisha ile Kamisheni kwa maana ile idara iliyoundwa. Lakini vile vile kutoa mafunzo kwa watendaji wote wanaohusika na masuala ya ununuzi na uondoshaji wa mali za serikali, mafunzo usimamizi wa sheria na kuimarisha utendaji wa kitengo chenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, haraka haraka suala la utaratibu wa magari ya biashara na mzigo nalo lilizungumzwa sana hapa niseme tu kwamba hili lilitokana na marekebisho ya sheria, Sheria ya Ushuru wa Stempu ya mwaka 2017 ambayo tumeipitisha katika Baraza hili na ndani ya sheria ile tumesema tuunganishe zile kodi ambazo zilikuwa zikitozwa na *TRA* na *ZRB* sasa iwe ni mahala pamoja tu pakutozea kodi hii. Sasa ni kweli kuna malalamiko Mhe. Mwenyekiti, na niseme kwamba malalamiko hayo yanafanyiwa kazi na hasa kwenye kiwango na pale tukihisi kiwango ni kikubwa zaidi basi *Inshaallah* tutahakikisha kwamba kiwango hicho kinapunguzwa kabla ya kufika mwaka 2018/2019.

Naomba niseme mengine madogo sana Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu majibu kamili tutayatoa Septemba lakini lile suala la ununuzi wa meli ya mafuta kuna mjumbe alisema ni vyema fedha

zile zingekwenda katika miundo mbinu ya mafuta kule Mangapwani. Hili Mhe. Mwenyekiti, hii ni miradi miwili tofauti na serikali inajua hili unajua umuhimu wa Mangapwani kuwa na miundo mbinu lakini vile vile na ununuzi wa meli ya mafuta, hiki ni kisiwa na kisiwa lazima tuwe na meli lakini pamoja na hayo serikali hivi sasa na Mhe. Rais mwenyewe tunajua hivi karibuni alitembea eneo la Mangapwani kwamba ziko taratibu katika ujenzi wa miundo mbinu katika eneo hilo kwa hivyo, ni miradi miwili ningeomba sana tusiichanganye miradi hii.

Mhe. Mwenyekiti, naona unakaribia kugonga kengele yako naomba nikubaliane na hoja hii kwa asilimia mia moja na Insha'Allah Mwenyezi Mungu akitujaalia majibu kamili tutayatoa mwezi wa Septemba naomba kupokea hoja hii. *(Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana nakushukuru Mhe. Waziri wa Fedha Dkt. Khalid sasa naomba nimwite Balozi Ali Karume Mhe. Waziri anayekaimu Wizara ya Biashara na Viwanda.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji (Kny. Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko): Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nikushukuru sana kwa kunipa fursa hii kwani nimeingia kidogo kwenye Baraza lako Tukufu kwanza kabisa kwa niaba ya Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko nitaanza kuwashukuru Mwenyekiti na Kamati kwa kutengeneza ripoti nzuri sana na ripoti hii itafanyiwa kazi na wizara na majibu rasmi tutaleta mwezi wa tisa tunapokutana tena katika Baraza lako tukufu.

Kwa hivyo nina mambo mawili matatu tu ambayo nilikuwa nataka niyagusie kwa leo. Kwanza suala la hiki kitengo cha mezani na vipimo ni suala muhimu sana katika mambo ya biashara lazima tuangalie sana mambo ya mizani na vipimo

kwasababu tunaogopa mambo ya kupunjiana, hilo linashughukiwa na linafanyiwa kazi.

Pia kuna hili suala la bei la bidhaaa kuwa zinapanda bei kila wakati hasa wakati wa mwezi wa ramadhani hili suala linajulikana na kwa mwaka huu tutachukua hatua za ziada za kuhakikisha tu kwamba kabla ya mwezi wa ramadhani kufika, tutakuwa tunakwenda kupeleka watu wetu wachunguze bei ya bidhaa zilivyo na wakati ukifikia mwezi wa ramadhani tuje kuwakuta watu ambao wanauza bidhaa zile zile kwa bei kubwa itabidi tuwafanyie uchunguzi na kuwauliza tujewe kwanini wanaongeza hizo bei na kama kuna *justification* ya kuongeza hizo bei ambayo zitakubalina na wizara hili tutawajulisha wananchi. Lakini kama watafanya hivyo kwa udanganyifu wizara itasimamia suala hilo na kuhakikisha kwamba bei zao wanazishusha au watahatarisha leseni zao za kufanya biashara. *(Makofi)*

Jengine katika hili limezungumziwa suala la hadaa za biashara sote tunajua kwamba kila mfanyabiashara duniani huwa anataka mapato yake yaongezeke, faida ya iongezeke na saa nyengine wanatamani kidogo kudanganya danganya lakini kwenye hilo nataka nikumbushe tu Baraza lako tukufu Mhe. Mwenyekiti, kwamba hivi karibuni tumepitisha sheria nzuri sana hapa ambayo itasimamia mambo haya tunategmea kwamba katika muda sio mrefu Mhe. Rais atatia saini sheria ile na itaanza kutumika, na itakapoanza kutumika itatumika kwa nguvu zote za kisheria.

La tatu hapa nilitaka niwajulishe wajumbe wa Baraza lako tufuku Mhe. Mwenyekiti, kwamba katika hili suala la biashara ya mwani nimeona kwamba kuna haja ya kuongeza thamani watalamu wanaita *value addition* na tumepata msaada kutokana na mashirikiano yetu na *UNIDO* hawa ni *United Nations Industrial Development Organization* wametupatia vifaa na mashine ndogo

ndogo za kusanifu mwani, vifaa hivyo vitatolewa hivi karibuni kwa wananchi.

La nne na la mwisho kwa upande wa ZSTC hili suala Mhe. Mwenyekiti la watoto wadogo kufanyishwa kazi limekuwa sio tatizo la kitaifa tu Mhe. Mwenyekiti, limekuwa ni tatizo la kimataifa na sisi Tanzania kwa kuwa ni wajumbe wa Umoja wa Mataifa ni wananchama huko wa Umoja wa Mataifa tunatakiwa tufate hii sheria na Mhe. Waziri anayehusika na sekta hiyo ya kazi yaani *labor* anayajua hayo na anayafuatilia kwa ukaribu sana.

Kwa hivyo, kuna hili suala la kusema kwamba *Internal Labor Organization* ambayo iko chini ya *United Nation* imeagiza kwamba watoto waliokuwa watoto wadogo wende shule sio wakafanyishwe kazi. Kwa hivyo hilo tutalisimamia na kuna mjumbe mmoja mheshimiwa mmoja alishauri tu kwamba wakati huu ni wakati wa kuchuma karafuu kule Pemba basi shule zifungwe, ili watoto waende wakazichume karafuu mimi nasema hili wakalifikirie tena. Kwa sababu watoto walioko katika umri wa chini ya miaka kumi na nane kazi yao kubwa na kazi yao ya kwanza ni kwenda skuli wakapate ujuzi ili watakapo kuja wakaanza kazi watapata kuchangia uchumi bora zaidi kuliko kwenda kupanda mikarafuu na kuanguka, wakati hawajafikia umri wa kufanyakazi.

Kwa hivyo, nataka nimalizie kwenye hilo kama wizara itashughulikia masuala haya yote changamoto zote hivi na ushauri wote uliotolewa tutaufanyia kazi na ikifika wakati wa kuleta ripoti rasmi tutaikabidhi hapa na kuiwasilisha kwenye Baraza lako Tukufu. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Waziri sasa naomba nimwite mtoa hoja Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo.

Mhe.Yussuf Hassan Iddi (Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo): Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa nikushukuru kwa kunipa nafasi hii jioni ya leo kwa ajili ya kufanya majumuisho kwa hoja ambayo nimeitoa pale asubuhi.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa niwashukuru wajumbe wote waliopata nafasi ya kuichangia ripoti yetu hii ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo na wale ambao hawakupata kuchangia moja au nyengine lakini wameridhia ripoti yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yetu hii ya Fedha, Biashara na Kilimo ambayo tumeiwasilisha leo asubuhi imepata kuchangiwa na wajumbe ishirini na nane. (Makofi)

Kwa ruhusa yako Mhe. Mwenyekiti, naomba niwataje wachangiaji hao kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Ali Suleiman Ali
2. Mhe. Suleiman Makame Ali
3. Mhe. Bahati Khamis Kombo
4. Mhe. Ali Khamis Bakari
5. Mhe. Hassan Khamis Hafidh
6. Mhe. Masound Abrahman Masoud
7. Mhe. Mussa Foum Mussa
8. Mhe. Hidaya Ali Makame
9. Mhe. Miraji Khamis Mussa
10. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
11. Mhe. Dk. Makame Ali Ussi
12. Mhe. Hamza Hassan Juma
13. Mhe. Hamad Abdalla Rashid
14. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu
15. Mhe. Rashid Makame Shamsi
16. Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi

17. Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango
18. Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji

Hao Mhe. Mwenyekiti ndio walipata nafasi ya kuweza kuchangia moja kwa moja yaani mubashara, lakini pia wapo waliochangia kwa maandishi.

1. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame
2. Mhe. Juma Ali Khatib
3. Mhe. Nassor Salim Ali
4. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa
5. Mhe. Tatu Mohamed Ussi
6. Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma
7. Mhe. Mussa Ali Mussa
8. Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini
9. Mhe. Simai Mohammed Said
10. Mhe. Waziri wa Habari, Utalii na Michezo

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli michango ya waheshimiwa wajumbe michango yao, maoni yao, mapendekezo yao ni mazuri na sisi kamati kwa kweli tumefarijika sana. Michango hii kwa kweli sisi itatusaidia katika kutekeleza majukumu yetu ya kamati, lakini pia waziri wote watatu Mhe. Hamad Rashid wamechukua michango hii, Mhe. Waziri wa Fedha wamechukua michango hii pamoja na Kaimu Waziri kwa sababu waziri husika wa Biashara, Viwanda na Masoko na yeye vile vile amechukuwa michango, hii na kwa kweli sote kwa pamoja waziri na sisi kamati tunashirikiana na pamoja kuhakikisha kwamba yake yote ambayo waheshimiwa wajumbe ambayo mmeyatoa basi tutayatekeleza ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa kanuni 108 fasili ya 15 inawataka waheshimiwa mawaziri imewapa muda waheshimiwa

mawaziri kuyachua maoni yetu haya ya kamati kuyafanyia kazi na baadae kuweza kuleta majibu yaliokuwa sahihi na mazuri zaidi. Tuwaombe basi waheshimiwa wajumbe tuwe na subira tuwape muda mawaziri wetu hawa ili wakayafanyie kazi na baadaye katika kikao cha Septemba waweze kuyatoa.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, niruhusu nizungumzie mambo matatu kama ifuatavyo. La kwanza kabisa ni kuhusiana na suala la ukodishwaji wa karafuu tuwaombe sana serikali na kwa bahati nzuri katika wizara zote tatu hili jambo linawahusu. Wizara ya Biashara linawahusu, Wizara ya Kilimo linahusu na Wizara ya Fedha linawahusu, wakae pamaoja watizame tumejikwaa wapi kwa sababu waswahili wanasema kujikwaa si kuanguka. Tumejikwaa wapi na tutafute njia ili katika msimu unaokuja haya yaliotokezea mara hii basi yasije yakatokezea tena, tunaomba mawaziri wetu tunajua mawaziri wetu ni wasikifu na wako makini zaidi natumai mtakaa pamoja ili kutafuta njia ya kulitafutia ufumbuzi hili suala la ukodishaji mikarafuu na wale ambao mpaka sasa hawajalipa basi waweze kulipa ili pesa hizi zirudi serikalini.

Lakini jambo la pili ambalo nataka nilizungumze Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yake ni kuhusiana na suala la msamaha ya kodi kwa wafanyabiashara hasa katika kipindi cha ramadhani baadhi ya wajumbe wamechangia hoja hii. Ni kweli misamaha serikali inatoa misamaha kwa nia njema lakini wananchi hawafaidiki na misamaha hii.

Tuwaombe sana Wizara ya Fedha, Wizara ya Biashara ikae kwa pamoja ifanye utafiti na itizame namna gani misaada hii inayotolewa kwanini haiwanufaishi wananchi. Ukiangalia na hasa katika kipindi hivi sasa hivi tunaelekea katika mwezi mtukufu wa ramadhani nadhani imebakisha miezi michache. Tuangalie kwa nini bei ya kipindi hiki kabla ya ramadhani zinakuwa ziko chini lakini kipindi cha ramadhani zinakuwa juu. Mfano halisi katika

kipindi hiki ukenda boksi la tende ka kilo kumi unaweze ukapata kwa elfu thelathini na mbili, thelathini na tatu lakini katika kipindi cha ramadhani elfu thelathini na tano na wananchi wanajiuliza kwa nini? misamaha imetolewa, kodi imepunguzwa lakini bado bei imepanda badala ya kushuka chini.

Kwa hivyo hatujachelewa Wizara ya Fedha, Wizara ya Biashara tukae pamoja na wafanya biashara wetu ili kuweza kulitatua tatizo hili na wananchi wetu waweze kupata nafuu hasa katika kipindi kile cha mwezi mtukufu wa ramadhani. *(Makofi)*

Suala la mwisho ambalo nimekusudia kulizungumza kuhusiana na *data* ambazo Mhe. Waziri wa Fedha amesema kidogo zimekosewa, kwa kweli sisi kamati hatuna vyanzo au *source* za *data* zetu *source* za *data* zetu ni kutokana na taarifa ambazo mnatupa. Tumelichukuwa hili Mhe. Waziri tutaliangalia ili tuone tumeteleza wapi lakini kwa kweli hatuna sehemu ya kuzipata *data* isipokuwa taarifa zenu ambazo tunapokea kila robo mwaka, lakini tumelichukua tutapokutana katika vikao vyetu vile basi tunaangalia namna gani ya kuweza kuziboresha na *data* zetu ziwe sahihi zaidi.

Mwisho kabisa Mhe. Mwenyekiti, nimalizie kwa kuwapongeza Mawaziri wote na Manaibu Waziri wote wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa namna mnavyotekeleza Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015/2020 matumaini yetu kwamba tukifanya kazi vizuri kwa kasi hii basi ikifika mwaka 2020 wananchi wengi watakiunga Chama chetu cha Mapinduzi na tutapata ushindi wa kishindo katika uchaguzi unaokuja. *(Makofi)*

Baada ya maelezo hayo Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli niwashukuruni sasa sisi kamati kwa kweli tumefarika sana na ushauri mlotoa tumeuchukua na tutaufanyia kazi, baada ya

maelezo hayo ahsanteni sana, nawashukuruni sana naomba kutoa hoja.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara Waheshimiwa Wajumbe hoja imetolewa na imeungwa mkono sasa naomba niwahoji wanaokubaliana na hoja hiyo, wanaokataa, wanaokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Waheshimiwa wajumbe na mimi nichukuwe nafasi hii kuwashukuru sana wale wote waliochangia katika ripoti hii, lakini pia shukrani za pekee ziende kwa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo pamoja na serikali kwa jumla najua tayari wameipokea na wataifanyia kazi itakapofika mwezi wa tisa basi wataleta majibu wanayostahiki.

Waheshimiwa wajumbe naomba niakhirishe kikao hiki mpaka Jumatatu saa 3:00 asubuhi siku ya tarehe 19/02/2018 nawashukuru sana.

(Saa 1:41 usiku Baraza liliakhirshwa mpaka Jumatatu tarehe 19/02/2018 saa 3:00 asubuhi)